ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Hamad Masoud Hamad	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ole.
9.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Kuteuliwa
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Magogoni
13.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Donge.
14.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Kiembesamaki
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Gando
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la MaMakunduchi
18.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Jang'ombe
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Omar Othman Makungu	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
29.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
30.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
31.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
32. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
33.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
34. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
35.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
36.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
37.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

38.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
41.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
42.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
43.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
44.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
45.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
46.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
47.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
48.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
49.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
50.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
51.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini
52.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
53.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad	Jimbo la Chambani
54.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Jimbo la Mpendae
55. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Nafasi za Wanawake
56.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
57. Mhe. Mussa Khamis Silima	Jimbo la Uzini
58.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
59.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake

60.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo
61.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
62.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Rashid Seif Suleiman	Jimbo la Ziwani
64.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
65.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
66.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
67.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
68.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
70.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
71.Mhe. Salum Amour Mtondoo	Jimbo la Bububu
72.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
74. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	Jimbo la Dole
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
78.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
79.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Ibrahim Mzee Ibrahim **Katibu wa Baraza la Wawalishi**

Kikao cha Kumi na Moja – Tarehe 1 Julai, 2011

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 118

Vijana Wanaojiunga na JKU Kupatiwa Nafasi za Ajira

Mhe. Shadya Moh'd Suleiman – Aliuliza**:-**

Miongoni mwa makusudio ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ya kuwapeleka vijana katika Kikosi cha JKU ni kupata mafunzo ya uaskari. Imebainika kuwa vijana wengi wanaomaliza mafunzo hayo hawajapata nafasi ya ajira katika vikosi vyetu, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Polisi.

(a) Je, Mhe. Waziri ni sababu zipi zinazopelekea Serikali kuwachukua vijana ambao hawajapata taaluma hii zinapotokea nafasi za ajira kwa upande wa vikosi mbali mbali.

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwapatia ajira vijana hawa zinapokuja nafasi hizi, ili kulinda hadhi ya kikosi hiki pamoja na kuwatia moyo vijana wetu ili wazidi kujiunga kwa idadi kubwa.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 118 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU) kisheria imeruhusiwa kuwapokea vijana waliomaliza elimu ya lazima kwa ajili ya kuwapatia mafunzo ya shughuli za amali pamoja na kuwapatia elimu ya uzalendo kwa taifa lao kwa kipindi cha miaka miwili kwa waliomaliza kidato cha 4 na mwaka mmoja kwa waliomaliza kidato cha 6 na kuendelea. Kijana yeyote mwenye sifa hiyo ana haki ya kujiunga na JKU iwapo atataka na JKU ina wajibu wa kumpokea kwa mafunzo hayo. Lengo la kujiunga na JKU si kutoa ajira bali ni

kumsaidia kijana kupata elimu ya manufaa na ujuzi yaani mafunzo ya amali *(skills)* kwa lengo la kujiajiri mwenyewe baada ya mafunzo hayo, pia kumjengea hisia za uzalendo (utaifa).

Mhe. Spika, utaratibu ulioanzishwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa kuingizwa kwa ajira ya watumishi wa taasisi zote za Ulinzi na Usalama ufanyike kwa vijana waliomo katika makambi ya JKT (Tanzania Bara) na JKU (Zanzibar) unatoa fursa kwa vijana walio kwenye makambi hayo kupewa nafasi ya kwanza katika ajira hizo. Hata hivyo, ajira katika taasisi hizo inahitaji vile vile kufikia sifa ambazo zimewekwa na kila taasisi. Sifa kubwa muhimu ni kuwa na elimu ya kuanzia kidato cha 4 na kuendelea pamoja na umri usiozidi miaka 23. Vijana wote ambao wanakuwa na sifa hizo wana uwezekano wa kuchukuliwa na taasisi za Ulinzi na Usalama.

(b) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tayari imo njiani kuiwezesha JKU kuchukua vijana wengi zaidi na kuwabakisha makambini kwa kipindi chote cha mafunzo ili kuweza kupata mafunzo yanayostahili na hatimae kufikia sifa zinazohitajika na taasisi zinazoajiri.

Ili kulinda hadhi ya kikosi hiki kama alivyoeleza Mhe. Mwakilishi, pamoja na kuwatia moyo vijana ili wazidi kujiunga kwa idadi kubwa Serikali inatoa kipaumbele kwa vijana waliopo makambini. Tatizo nafasi huwa ni chache na vijana wapo wengi.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nimuulize Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri amezungumzia neno ajira na vijana. Je, Wizara yako inategemea kutoa ajira kiasi gani kwa mwaka huu wa fedha 2011/2012.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, ni hivi karibuni tu vikosi vyetu vilikuwa na ajira ndogo ya kuziba mapengo kwa wale wastaafu. Bado sijaweza ku-*establish* hasa nafasi zile zilizoombwa kwa mwaka huu wa fedha. Lakini hata hivyo, tunatathmini kwanza hali ilivyo kwenye majeshi yetu tuone wapi pana mapungufu gani na baadae tutaweza kusema hasa twende vipi na ajira zetu.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba sasa ni miaka mitatu tokea walipowaweka vijana pale JKU kwa tamaa ya kwamba zitatoka ajira za jeshi na waajiriwe na bado wamelemaa tu.

Lakini la pili tumekuwa tukielezwa kwamba ajira za jeshi na polisi ni ajira za Muungano na huwa zinagaiwa nafasi hizi ni za Tanganyika na nafasi hizi ni za Zanzibar. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba hata zile nafasi za Zanzibar sasa zinachukuliwa na watu kutoka Tanzania Bara kwa kutumia ujanja.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, nakubaliana nae kwamba kweli kwenye makambi yetu wapo vijana wa miaka mitatu na zaidi. Hii kama nilivyosema inatokana na uchache wa nafasi inabidi kidogo wakae zaidi na kadri nafasi zinavyotokezea basi sisi tunajitahidi kuwatoa.

Mhe. Spika, swali lake la pili Mhe. Mwakilishi ameeleza kwamba hayo yanatokezea mimi sikatai. Sasa kama ametueleza sisi tutaingia ndani tufanye uchunguzi. Lakini la msingi nafasi zikija zinatawanywa mikoani na sio siri zinatangazwa ndani ya redio kila kijana mwenye sifa aende kwa Mhe. Mkuu wa Wilaya wanaandikishwa wanafanyiwa usaili wanachukuliwa na vipimo. Lakini sasa kama hayo kayasikia Mhe. Mwakilishi mimi namshukuru kwa kunipa taarifa hiyo tutaifanyia kazi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru sana kunipa fursa na mimi kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, sasa hivi mtindo uliopo katika nchi yetu atakubaliana na mimi Mhe. Waziri kama zinapokuja ajira katika vikosi vya ulinzi kama jeshi, polisi au JKU wale makamanda wa vikosi wana mtindo wa kuwachukua ndugu zao na kuwaleta.

Kwa mfano, ikiwa ajira zinaelekea Pemba au hapa Unguja, lakini hutolewa vijana aidha kutoka Dar es Salaam na mikoa mingine na wakaja kule wakapata ajira kupitia mgongo wa eneo lile.

Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kama suala hili linafanywa. Je, ni haki kufanya hivyo. Kama si haki je, yeye kama Waziri wa sehemu hii atasimamia vipi kuhakikisha kama vijana wanaopata ajira ni wale wanaotoka katika mitaa ile.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Spika, Mhe. Mwakilishi aliyoyaeleza ni kweli kwamba tumepata malalamiko hayo sikanushi yapo. Lakini kama nilivyomjibu Mhe. Abdullla Juma Abdulla sasa tumeyasikia rasmi na tutasimamia vizuri.

Kama nilivyoeleza tunajitahidi nafasi zile wale makamanda wakija wanakwenda kimikoa na nafasi zinagaiwa kimikoa na wilaya na wanatangaza hasa redioni jamani nafasi za jeshi zipo. Kwa hiyo, wanapokwenda kule wanafanya vipimo na wanafanya usaili.

Lakini sasa haya uliyoyasema kwamba makamanda wana watu wao wanawaleta kwa pembeni, basi kama serikali tumesikia tutafuatilia na tutasimamia vizuri.

Nam. 167

Kuazishwa *Account* ya Pamoja

Mhe. Omar Ali Shehe - Aliuliza**:-**

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kifungu cha 133 na 134 kimeainishwa kuundwa kwa Tume ya Pamoja ya Fedha kati ya Serikali mbili ya SMT na SMZ kadhalika kuanzishwa kwa *account* ya pamoja kati ya Serikali hizo.

Kwa kuwa Tume ya Pamoja ya Fedha imeanzishwa na kufanya kazi zake kwa siku nyingi na kutoa mapendekezo yake kwa Serikali zote mbili juu ya namna ya kugawa mapato yatokanayo na shughuli za Muungano.

(a) Je, SMZ kwa upande wake imefanyiaje kazi mapendekezo ya Kamati hiyo.

(b) Ni mapendekezo gani ambayo hadi sasa yameshafanyiwa kazi na Serikali zote mbili.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo - Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 167 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Lakini kwanza naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa kifungu cha 133 cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kinatamka kuanzishwa kwa Akaunti ya Pamoja ya Fedha. Kifungu hicho kinaelezea kuwa fedha yote itakayochangwa na Serikali mbili kwa kiasi kitakachoamuliwa na Tume ya Pamoja ya Fedha itawekwa kwenye akaunti ya pamoja. Fedha zitakazochangwa ni kwa madhumuni ya shughuli za mambo ya Muungano.

Mhe. Spika, kutokana na matakwa ya kifungu hicho cha Katiba pamoja na Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha, Tume imetoa mapendekezo ya msingi yafuatayo kwa Serikali zote mbili (SMT & SMZ).

(i) Vigezo vya kugawana mapato na jinsi ya kuchangia gharama za Muungano. Pendekezo hili limewasilishwa tarehe 29/8/2006.

(ii) Mwongozo kuhusu Akaunti ya Fedha ya Pamoja itakavyokuwa inaendeshwa ikiwa ni sehemu ya Mfuko Mkuu wa Serikali ya Muungano. Pendekezo juu ya mwongozo huu limewasilishwa Septemba, 2009.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo kwa heshima kubwa sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:

(a) Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Baraza la Mapinduzi imeyafanyia uchambuzi wa kina na kuyajadili mapendekezo hayo na hatimae kutafuta Mshauri Mwelekezi kuishauri ipasavyo Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Ushauri wa Mwelekezi umezingatia utaratibu bora unaotumika katika nchi zenye mfumo wa Muungano kama wa kwetu. Maoni ya SMZ yako tayari.

(b) Mhe. Spika, kama nilivyoelezea katika maelezo yangu ya utangulizi. Lengo la kuundwa Tume ya Pamoja ya Fedha ni kuzishauri Serikali zetu mbili juu ya kuchangia gharama za Muungano na namna ya kugawana mapato ya Muungano, pamoja na kushauri juu ya namna bora ya uanzishwaji na uendelezaji wa Akaunti ya Pamoja ya Fedha. Hata hivyo, niliyoyataja katika utangulizi ndio mapendekezo ya msingi na tayari SMZ imeshayafanyia kazi. Kinachosubiriwa ni kwa upande wa SMT kuyafanyia kazi na kutoa maoni yao.

Mhe. Spika, maoni ya SMZ na yale ya SMT yatajadiliwa katika kikao cha pamoja kwa lengo la kufikia muafaka wa pamoja.

Mhe. Omar Ali Shehe: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametwambia ni kweli kwamba tume ipo na imeshapeleka mapendekezo yake serikalini tangu mwaka 2006.

(a) Kwa kuwa sasa hivi ni zaidi ya miaka 6 tangu tume kupeleka mapendekezo yake serikalini. Je, ni sababu zipi zilizopelekea kwamba serikali hadi sasa haijachukua hatua.

(b) Kwa kuwa hili ni suala la Kikatiba na kwa kuwa Marais wetu wameapa kuilinda Katiba yule wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Je, Mhe.

Waziri huoni kuwa kutokutekeleza kipengele hichi ni kwenda kinyume na Katiba waliyoapa kuilinda Marais wetu.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, nimeeleza katika jibu langu la msingi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshakamilisha maoni yake. Kwa upande wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yalipowasilishwa katika Baraza la Mawaziri ilibainika kwamba takwimu zilizotumika zimepitwa na wakati. Hivyo, Tume ya Pamoja ya Fedha ilitakiwa kwenda kurekebisha takwimu zile ili waje na *up to date statistics* kwa maana ya kwamba uchambuzi wa kina uweze kufanyika. Sisi kwa upande wetu tumepata ripoti hiyo ya pili ambayo sasa ina takwimu za karibu zaidi.

Mhe. Spika, kwa upande wa swali lake la pili nataka nimwambie tu Mhe. Mwakilishi kwamba Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba yoyote ile, ili iweze kutekelezwa vyema vifungu vyake ni muhimu kuwepo kwa sheria na kanuni za kuongoza utekelezaji wa vifungu vile. Kifungu hiki kilichozitaka serikali zetu mbili kuanzisha akaunti ya pamoja kimefuatiwa na kifungu cha tume, kuundwa kwa tume na kuundwa kwa sheria ya tume. Tume hiyo imetoa kazi ya kueleza utaratibu muafaka kuanzisha na kuiendeleza akaunti ya pamoja. Ripoti yao imewasilishwa serikalini mwaka 2009 kama ni mwongozo na serikali tayari imeshaipitia vile vile. Tunasubiri wenzetu ili tuweze kuweka maoni yetu pamoja na ya kwao, ili akaunti hiyo iweze kufunguliwa, hatuna muda mrefu akaunti itafunguliwa.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa ripoti ya *JFC* tayari imeshafanyiwa kazi kwa muda mrefu na SMZ na mapendekezo yake kuwasilishwa. Kwa kuwa muda wote huo wenzetu wa SMT hawajaweza kuifanyia kazi ripoti hiyo. Kwa kuwa SMT waliirejesha tena ripoti hiyo eti kwa visingizio kwamba imeshapitwa na wakati.

(a) Je, Mhe. Waziri kutokana na hali inavyoendelea juu ya kuanzishwa kwa akaunti hiyo ya pamoja. Huoni kwamba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haioneshi juhudi yoyote ya kulimaliza jambo hili hasa ukizingatia kuwa wao ndio wanaofaidika zaidi kutokana na fedha za Muungano.

(b) Kutokana na hali inavyoendelea. Huoni sasa iko haja kwa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi na ile Kamati ya Fedha na Uchumi ya Bunge pamoja na Mawaziri wa Fedha wanaohusika kukutana pamoja ili kulimaliza jambo hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwamba hata Serikali ya Muungano bado inaonesha juhudi ya kutaka kulimaliza suala hili. Wiki mbili zilizopita tu Mhe. Waziri Mkuu alijibu swali kama hili Bungeni na akawahakikishia Wabunge kwamba si muda mrefu suala hili la kufunguliwa kwa akaunti ya pamoja litamalizika.

Mhe. Spika, pili wazo la Mhe. Mwakilishi la kutaka Kamati ya Fedha ya Bunge na Kamati ya Fedha ya Baraza la Wawakilishi pamoja na Mawaziri wa Fedha wa Zanzibar na wa SMT kukaa pamoja kujadiliana juu ya jambo hili sio wazo baya na mimi sina matatizo na wazo hilo. Wakati itakapokuwa kunahitajika hivyo basi na mimi nalikaribisha. Ni imani yangu kwamba kwanza tukikaa pamoja tutaweza kuibua mambo mengine ya ziada mbali ya hili na tutaweza kwa umoja wetu na udugu wetu kuyatafutia ufumbuzi.

Mhe. Subeit Khamis Faki: Mhe. Spika, nakushukuru kunipa fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Mhe. Spika, Tanzania ni nchi mbili ambazo zimeungana Zanzibar na Tanganyika na kufanya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nchi hizi baada ya kuungana zilikubaliana kuunda mfuko wa pamoja kwa ajili ya maslahi ya nchi zote mbili. Sasa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatakiwa ichangie mfuko huu kwa pamoja, lakini kule wenzetu wanatumia fedha zile zile za Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuchangia.

Je, hatuoni hii kama kwa upande mmoja tunapigwa kwa fimbo yetu. Kama tunapigwa kwa fimbo yetu serikali inatwambia nini kuhusu suala hili.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo: Mhe. Spika, kwanza nataka nimhakikishie Mhe. Mwakilishi hakuna serikali hata moja inayochangia hadi hivi sasa katika akaunti hii kwa sababu ule utaratibu wa kuchangia Serikali ya Muungano bado hawajatoa maoni yao. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeshaweka maoni yake mpaka maoni ya pande mbili yatakapopitishwa na kukubalika ndio utaratibu wa kuchangia katika akaunti hii utakapoanza.

Hivi sasa kilichopo ni kwamba mapato ya Muungano yanayopatikana kupitia vianzio vya Muungano vilivyopo Zanzibar yanabakia na kutumiwa Zanzibar na yale ya Muungano yanayopitia vianzio vya Tanzania Bara yanabakia na kutumika Tanzania Bara.

Nam. 3

Vyumba vya Maabara katika Skuli za Sekondari

Mhe. Rashid Seif Suleiman – Aliuliza**:-**

Bila ya shaka vyumba vya maabara katika skuli za sekondari vina umuhimu mkubwa katika juhudi za kuongeza ari na mwamko wa wanafunzi wetu kupenda masomo ya sayansi.

(a) Je, kuna idadi gani ya vyumba vya maabara katika skuli zetu za sekondari.

(b) Je, Wizara imeajiri Wasaidizi wa Maabara *(Laboratory Assistants)* wangapi katika kuzihudumia maabara hizo.

(c) Je, kuna watumishi ambao wako masomoni. Kama wapo ni wangapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali – Alijibu**:-**

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 3 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Spika, ni kweli kuwa vyumba vya maabara katika skuli za sekondari vina umuhimu mkubwa katika kuongeza ari na mwamko wa wanafunzi wetu kupenda masomo ya sayansi.

(a) Mhe. Spika, skuli zote za sekondari za Serikali 198 zina vyumba vya maabara

(b) Wizara haijaajiri Wasaidizi wa Maabara *(Laboratory Assistants)* kutokana na kutokuwepo kwa wataalamu waliosomea fani hiyo. Hata hivyo, wizara inawatumia baadhi ya walimu wa masomo ya sayansi kufanya kazi za kuhudumia maabara. Walimu hawa wamepatiwa mafunzo kazini juu ya utunzaji wa maabara hizo.

(c) Wizara haina watumishi walioko masomoni wanaojifunza kada hii.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Mhe. Spika, baada ya majibu yasiyoridhisha ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Spika, kwa kuwa

niliuliza idadi ya vyumba vya maabara na alisema tu skuli zetu zina vyumba vya maabara. Ningependa kujua idadi ya vyumba vya maabara.

Mhe. Spika, swali (b) kuhusiana na Wasaidizi wa Maabara *(Laboratory Assistants).* Je, Mhe. Waziri haoni kwamba huu ni usumbufu kwa walimu na ukosefu mkubwa kwamba maabara zetu haziajiri wasaidizi watakaowasaidia walimu katika ufanisi wa kazi ile. Sisi wengine ikiwa tulikuwemo katika kazi hiyo.

Lakini swali © kwa kuwa somo la sayansi ni somo la vitendo na Wizara inapiga kelele kwamba hakuna walimu wa sayansi, wanafunzi wanafeli somo la sayansi. Je, Mhe. Waziri haoni kwamba uendeshaji wa elimu wa namna hii ndio unaosababisha kila siku wanafunzi wakafeli sayansi, walimu wa sayansi hawapatikani tena na mwisho hili somo litafikia kuwa halisomeshwi tena hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, nadhani Mhe. Mwakilishi hakunisikiliza vizuri nilipokuwa najibu swali mama au tayari alikuwa na swali lake kaliweka aniulize. Nilijibu kuwa skuli zetu 198 za serikali zote zina vyumba vya maabara. Kwa hivyo, hapo hesabu inakuja kama tuna vyumba vya maabara 198.

Lakini Mhe. Spika, suala la kutokuajira wasaidizi wa maabara. Mhe. Spika, pia nilieleza kuwa hatujaajiri wasaidizi hao kutokana na kuwa hatujapata hao wasaidizi. Kwa hivyo, tunatumia walimu wetu ambao tunao na hao walimu sio kuwa tunawatumia tu, lakini wanapata mafunzo kazini ili waweze kuhudumia maabara hizo.

Mhe. Spika, wizara inaamini kuwa mfumo wa elimu unaimarika ingawa tunachangamotonyingi za hapa na pale. Fursa za elimu ambazo zinaongezeka za wanafunzi wetu kuingia katika vyuo vya eliku ya juu, ni dhahiri kuwa elimu yetu haijadumaa wala haijadumaa wala haijadumazika isipokuwa tunaimarika.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuongezea majibu ya nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe anataka kujua vyumba vya maabara ni vingapi katika skuli yetu.

Mhe. Spika, naomba kumjibu kwamba katika skuli 198 kuna skuli zina vyumba viwili vya maabara, kuna skuli zina vyumba vitatu vya maabara na kuna skuli zina vyumba vinne kwa sababu wengine wanakuwa na maabara ya kompyuta. Sasa kwa idadi kamili hiyo itabidi asubiri tumletee kwa maandishi vyumba vyote vya maabara katika skuli zetu ni vingapi.

Pili, katika ilani yetu ya chama cha Mapinduzi, tumekusudia kwamba safari hii kuimarisha elimu na kwa sababu hiyo ndio imechukuliwa hii hatua ya kujenga skuli mpya pamoja na kuchukua hatua ya kuagizia vifaa vya maabara kwa ajili ya skuli zetu. Ni kweli tunalo tatizo la watumishi wa maabara katika skuli zetu zote. Tumekubaliana na SUZA kwamba hii tuichukuwe kama ni changamoto, tuanze kufundisha watu wa kuhudumia maabara zetu. Tunaye mmoja ambaye ameshakwenda masomoni Nairobi na akirudi tunakusudia kumtumia aanze kutoa mafunzo hayo kwa ajili ya maabara zetu. Kwa hivyo, tutawaomba walimu wakubali kuchukua, maana hii nafasi ya maabara kwa hivi sasa walimu wengi wanakuwa hawaitaki, wanataka wawe walimu tu, lakini hawataki kufanya kazi katika maabara. Kwa vile tuna vijana ambao wanamaliza kidato cha sita tunaweza kuwafundisha masuala haya na wakawa wanafanyakazi katika maabara katika skuli zetu, ahsante sana.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, je wizara ina mikakati gani ya kupunguza idadi ya wanafunzi wanaofeli hasa masomo ya sayansi, kwa kuzingatia kwamba vifaa vya maabara ni vichache sana katika maskuli.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, wizara ina mikakati ya kupunguza wanafunzi wanaofeli hususan masomo ya sayansi. Kwanza ni kwa kuongeza idadi ya walimu wanaosomesha masomo hayo ya sayansi.

Mhe. Spika, pia ni ujenzi wa skuli hizi za kisasa ambazo tunajenga skuli 21. Skuli zetu hizi zikimaliza zitakuwa na vifaa vyote vinavyotakiwa na kutakuwa na maabara. Kwa hivyo, wanafunzi wetu wataweza kusoma masomo ya sayansi kwa vitendo.

Jengine Mhe. Spika, ni kuwahimiza na kuwahamasisha wanafunzi kuyapenda masomo ya sayansi. Kwa sababu kumekuwa na dhana kubwa kwa wanafunzi kuwa masomo ya sayansi ni magumu, kwa hivyo wanakuwa hawashawishi. Muhimu ni kuwahimiza wanafunzi ili kuweza kusoma masomo ya sayansi. Madhali vifaa vya maabara vitakuwepo, basi naamini wanafunzi wetu watapasi kwa wingi masomo hayo ya sayansi.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri utakubaliana na mimi kwamba skuli nyingi za zamani tukiacha hizi mpya zinazojengwa za

kisasa hazina maabara kabisa. Kwa mfano skuli yangu ya Gamba pale haina maabara hata kidogo na hakuna hata kifaa kimoja kinachoweza kutumika katika kufanya *practical*.

Je, Mhe. Waziri, pamoja na kwamba wizara yako ya elimu ina mpango mzuri sana wa kuimarisha somo la sayansi kwa kujengwa skuli 21. Una mpango gani wa dharura wa kuweza kuzisaidia zile skuli zetu za asili ambazo kwa hivi sasa naona zinataka kudharauliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ni kweli Mhe. Spika, kwamba skuli zetu nyingi hazina walimu wa kutosha na maabara ambazo zimekamilika, yaani nakusudia zina vyumba vya maabara lakini havina vifaa vya maabara.

Ni kweli Mhe. Spika, baadhi ya skuli zetu zina vyumba vya maabara lakini havikukamilika. sawa. Sasa. Haa! Samahani Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waziri atasaidia.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, jibu analijua Naibu Waziri wangu hakuna wasi wasi wowote, lakini pengine kaliweka upande tu, lakini analo pale pale alipo.

Mhe. Spika, ni kwamba katika skuli za zamani ambazo zinazo vyumba vya maabara, lakini hakuna vifaa vya maabara. Hivi karibuni Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ilichukua hatua ya kununua vifaa vya maabara, lakini kwa sababu ilionekana kwamba havitaenea katika skuli zote vya kutosha, basi viliwekwa katika TC. Skuli zile zilitakiwa zinapokuwa zinataka kufanya mazoezi wale wenye haja wakachukuwe vifaa wakatumie katika skuli zao.

Hata hivyo, tunao mpango wa kununua vifaa vya maabara kwa ukamilifu na kuvisambaza katika skuli hizi ili tuwe tunavyo hasa pale pale katika zile maabara zetu za maskulini. Kwa hivyo, huo mpango tunao, mbali ya hizo skuli zetu 21 tunazojenga, lakini mfuko wa pili ni huo wa kununua vifaa vyetu sisi wenyewe vya maabara, kuweka katika skuli zetu za zamani. Kwa wale ambao wako karibu na hizi skuli za zamani, kwa sababu kila panapojengwa hii skuli hii mpya basi karibu yake pana skuli ya zamani, hao ndio watafaidika zaidi kwa sababu ni miguu mitatu au minne mpaka kuingia katika skuli ya zamani akapata vifaa pale na wakapata kufanya mazoezi ya kutosha. Ahsante sana Mhe. Spika.

Nam. 115

Uanzishaji wa Viwanda vya Kusindika Mazao,
Wilaya ya Kaskazini "A"

Mhe.Ussi Jecha Simai – Aliuliza:-

Ahsante Mhe. Spika, kabla sijauliza swali langu naomba nifanye marekebisho madogo. Katika kifungu cha pili na mstari wa pili neno 'wilaya hizo' lisomeke katika wilaya hiyo na siyo hizo. Mhe. Spika, baada ya marekebisho hayo naomba sasa swali langu namba 115 lijibiwe.

Wananchi wa Wilaya ya Kaskazini "A" ni wakulima wazuri wa mboga mboga kama vile Tungule, Bilingani, Mchicha, Nyanya chungu n.k na hupata mavuno mazuri kila mwaka, lakini mavuno hayo hupotea baada ya muda mfupi na matokeo yake hulazimika kuuza mazao yao kwa hasara.

Je, Serikali haioni kama ipo haja ya kuanzisha Viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao katika Wilaya hizo, ili kuwapa wakulima uhakika zaidi wa kuuza mazao yao na kujiongezea kipato chao.

Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjbu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 115 kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Spika, wizara yangu imeona umuhimu wa kuwa na huduma ya usarifu wa mazao ili kuongeza thamani ya mazao na kupunguza upotevu wa mazao. Mradi huo tayari umeshaanzishwa kwa msaada wa Serikali ya Jamhuri ya watu wa Korea ya Kusini. Kwa kupitia Mradi huu, wakulima watapata fursa ya kupata mafunzo juu ya usarifu na watahamasishwa kuanzisha miradi yao ya usarifu wa mazao.

Mhe. Spika, katika juhudi za serikali yetu kuleta mageuzi ya kilimo, kwa kauli mbiu ya nchi yetu, (MAPINDUZI YA KILIMO) uongezaji wa thamani wa mazao yetu ni muhimu sana, juhudi zitaendelezwa kushajihishwa wawekezaji kuwekeza katika viwanda vya kusindika matunda na usarifu wa viungo. Nakushukuru Mhe. Spika.

Nam. 66

Mafunzo ya Kuwawezesha Wananchi Kiuchumi

Mhe. Salmin Awadh Salmin – Aliuliza:-

Ahsante sana Mhe. Spika, kabla ya kujibiwa swali langu naomba kufanya marekebisho kidogo. Kwenye mstari wa chini kuna neno 'kwa mwaka huu wa fedha' lisomeke kwa mwaka 2010/2011. Katika swali (b) kwenye neno 'mwaka huu' basi lisomeke kwamba ni mwaka huo. Baada ya marekebisho hayo, naomba sasa suala langu nambari 66 lijibiwe.

Katika suala la kuwawezesha wananchi kiuchumi, Serikali imelenga kuwaongezea uwezo zaidi wanawake na vijana kwa kuapatia mafunzo katika fani za biashara, kilimo, uvuvi na usarifu wa viungo. Vile vile serikali imepanga kutoa mikopo yenye thamani ya TZS. 120 Millioni katika mwaka huu wa fedha.

(a) Je, Mhe. Waziri katika utekelezaji wa mambo haya ni wanawake na vijana wangapi waliopatiwa mafunzo hayo, kwa kuzingatia mchanganuo wa kijinsia na kimajimbo.

(b) Ni kiasi gani cha fedha kilichokopeshwa kwa mwaka huu wa fedha kati ya fedha zilizolengwa.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: (Kny: Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako ninaomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 66 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika kuwawezesha wananchi, kiuchumi, wizara yangu katika mwaka huu wa fedha wa 2010/11 imewapatia mafunzo jumla ya wananchi 93 (wanawake 57 na wanaume 36), miongoni mwao wakiwemo vijana 47. Wananchi hawa waliopatiwa mafunzo wametoka katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba. Kwa bahati mbaya hatuna taarifa hapa mkononi zinazotoa uchambuzi wa kimajimbo, lakini uchambuzi huo kimkoa ni kama ifuatavyo:-

Mjini Magharibi watu 10, Kaskazini Unguja watu 18, Kusini Unguja watu 7, Kusini Pemba watu 50 na Kaskazini Pemba watu 11.

(b) Katika mwaka huu wa fedha wa 2010/11 hadi kufikia Machi, 2011, Wizara imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Milioni sitini na laki tatu (T. Shs. 60,300,000/=) kati ya Shilingi Mia moja na Ishirikini (T. Shs. 120,000,000/=) zilizopangwa kutolewa.

Mhe. Salmini Awadh Salmini: Ahsante Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Mhe. Waziri alipokuwa akijibu swali langu alisema kwamba hakuna takwimu zinazoonesha kimajimbo na mimi nilitaka kujua kimajimbo. Lengo langu ni kujua ni namna gani wananchi wanaweza kufaidika kimajimbo badala ya kimikoa. Swali langu liko hapa.

Je, Mhe. Waziri kuwachukuwa na kuwawezesha vijana na kinamama kimkoa, huoni kwamba unaweza kusababisha watu wakafaidika sehemu moja katika jimbo moja, badala ya kufaidika wananchi wote wa Zanzibar kwa kupitia majimbo yao.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: (Kny: Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, nakubaliana na yeye kwamba ukichukua kimkoa linaweza likatokea hilo tatizo la kuwa unaweza ukachukua vijana wa sehemu moja.

Hata hivyo, kwa kuwa hii kazi ndio kwanza tumeianza ushauri wake tutauchukua na tutaangalia kuona tunaeneza hii mikopo katika maeneo yote.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Je, Mhe. Waziri anaweza kunieleza kwa upande wa Pemba ni vijana wangapi waliofaidika na mafunzo hayo, wakiwemo wanaume na wanawake.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: (Kny: Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, katika jibu langu mama nilisema kwamba Pemba ni watu 61 wameshafaidika na elimu hii. Ila uchambuzi wa wanawake wangapi na wanaume wangapi hiyo sinayo.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Je, Mhe. Waziri atakubaliana na mimi kwamba masharti ambayo ameyaweka ili wananchi kupata mikopo hiyo ni magumu sana kiasi kwamba vijana na kina mama wanashindwa kutimiza masharti hayo na hivyo kukosa fursa ya kupata mikopo hiyo.

Je, Mhe. Waziri, wizara haioni kwamba ipo haja ya kuregeza masharti hayo ili wale walengwa wapate mikopo hiyo.

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: (Kny: Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Spika, maana ya kuweka mafunzo ni kwa sababu tunataka hawa vijana wawe wajasiriamali kweli kweli. Wasiwe wanachukua mikopo lakini hawajui jinsi ya kuitumia, hawajui kurejesha. Iwe wao wanajua kuchukua mikopo na wakati mwengine wanakwenda kununulia tasi kula, mkopo haurudi wala hauzalishi ndio maana tukawa tunawafundisha. Haya mafunzo yatawafanya vijana hawa wayaone haya masharti sio magumu. Hivi sasa wanayaona magumu kwa sababu tuko chuoni, lakini baadae wakishazowea watajua kuwa mafunzo sio magumu na watatekeleza *Inshaallah*.

Nam. 25

Huduma Katika Uwanja wa Ndege wa Zanzibar

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) - Aliuliza:-

Uwanja wa Ndege wa Zanzibar sasa umekuwa ni uwanja wenye hadhi ya Kimataifa lakini kumekuwa na baadhi ya matatizo katika jengo la uwanja huo ikiwemo uduni wa baadhi ya huduma, kama vile vyoo na viyoyozi.

(a) Je, ni lini vyoo vya uwanja huo vitakuwa na maji muda wote.

(b) Ni tatizo gani hasa linalosababisha kukosekana kwa maji katika vyoo hivyo.

(c) Ni kwa nini sehemu ya kusubiria abiria inakuwa haina viyoyozi na kusababisha joto kwa abiria wanaosubiri kuondoka.

(d) Je, ni lini Serikali itaweka viti vya kutosha kwa abiria wanaoondoka ili kuondosha usumbufu kwa abiria kusimama hasa wakati ndege zinapokutana nyingi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye kifungu (a), (b), (c) na (d) kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Katika maeneo ya Uwanja wa Ndege wa Zanzibar kumekuwa na tatizo la hali ya kupanda na kushuka kwa kiwango cha umeme, kunakopelekea usumbufu na hata kuharibika kwa mitambo yetu na kukosekana kwa huduma ya maji, hatua ambayo hupelekea upungufu au ukosefu wa maji, au kukatika katika maeneo haya. Hali hii ya kupanda na kushuka kwa kiwango cha umeme imekuwa ikisababisha mitambo ya aina mbali mbali, ikiwemo mitambo ya kusukuma maji kushindwa kufanya kazi vizuri na mara nyengine kusababisha kuharibika mitambo ile.

Ni hivi karibuni tu mtambo wa kusukumia maji katika kisima kiliopo uwanja wa ndege uliharibika na kusababisha upungufu wa maji katika jengo la abiria. Hata hivyo, Wizara yangu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) waliweza kuifanyia matengenezo mashine hiyo, na hivi sasa inaendelea kufanyakazi vizuri na huduma ya maji yanapatikana kama kawaida maeneo ya uwanjani hapo.

Baada ya maelezo yangu hayo, sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a/b) Mhe. Spika, vyoo vya Uwanja wa Ndege Zanzibar vimekuwa na maji wakati wote isipokuwa pale ambapo kunatokezea matatizo katika mtambo wa kusukumia maji kushindwa kufanyakazi zake vizuri kama ilivyo kawaida.

(c) Sehemu ya kusubiri abiria inavyo viyoyozi ambavyo hutumika kupunguza joto katika sehemu ile. Hata hivyo, napenda nikiri kwamba viyoyozi hivyo vinazidiwa na idadi ya watu na hivyo huduma hiyo huwa ni dhaifu.

(d) Mhe. Spika, eneo la kuondokea abiria katika Uwanja wa Ndege Zanzibar linavyo viti vya kutosha kulingana na ukubwa wa sehemu husika. Usumbufu wanaoupata abiria kusimama hasa wakati ndege zinapokuwa nyingi unatokana na udogo wa eneo hili la kuondokea na si suala la uhaba wa viti katika sehemu ile.

Hali hii inatarajiwa kuondoka baada ya kukamilika kwa ujenzi wa jengo jipya la abiria na shughuli za kuhudumia ndege na abiria za Kimataifa kuhamishiwa katika jengo kwa vile kutakuwa na nafasi ya kutosha ya kuweka viti na kuongezwa huduma nyengine muhimu.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando): Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi na mimi nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali moja dogo la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo. Katika majibu yake Mhe.

Naibu Waziri alisema suala la maji linatokana na kupanda na kushuka kwa umeme katika uwanja wa ndege pale.

(a) Je, Atakubaliana na mimi Mhe. Naibu Waziri kwamba kuna jenereta pale lina zaidi ya mwaka ambalo ni kubwa na lenye kutosheleza umeme wa kutosha kabisa halijaungwa mpaka leo. Hiyo ni sababu inayosababisha kwamba umeme usipatikane katika uwanja wa ndege ule.

(b) Kwenye sehemu ya kukalia abiria kwa ajili ya kuondoka, viti vinakuwa kidogo kutokana na kuwa abiria ni wengi. Kumekatwa vibanda vingi mule ndani vya biashara zaidi. Je haoni hii ndio chanzo kinachosababisha eneo lile kuwa finyu. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, ni kweli nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba katika uwanja wa ndege lipo jenereta, jenereta lile matumizi yake ni pale ambapo umeme utakuwa umezimwa. Matatizo tuliyoyaeleza hapa yanatokana na kupanda na kushuka kwa umeme wenyewe na sio kuzima kwa umeme. Kwa hivyo, pale umeme utakuwa umezima jenereta lile tutalitumia na tunaamini kuwa litasaidia kuongeza nguvu za umeme katika mitambo ya kusukumia maji.

Mhe. Spika, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba katika eneo la kusubiria abiria kuna vibanda vingi, eneo lile lina vita 144 na watu wanaosubiri wanatakiwa waendane na idadi hiyo. Sote kwa pamoja naomba tukiri kwamba abiria wanaokuja pale ni wengi, wanazidi idadi ile husika na vibanda vile sio sababu wala kikwazo kinachopelekea watu kusimama kwa kukosa viti. Eneo lile limelengwa kulingana na idadi hiyo na ukubwa ule. Masuala ya biashara katika viwanja vya ndege ni jambo la lazima na ambalo haliepukiki.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Ahsante Mhe. Spika, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo. Mhe. Spika, hali ya uwanja wa ndege wa kimataifa unatokana na mambo mengi, mbali ya haya ambayo yametajwa hapa.

(a) Je, Mhe. Waziri huu utaratibu uliobuniwa hivi sasa wa kuufanyia *partition* hasa lile eneo la nje kwa njia ile ya mabati, hatuoni kwamba imeharibu zaidi badala ya kuboresha mazingira katika eneo lile kiasi ambacho inaleta joto jingi sana kutokana nay ale *material* iliyotumika.

(b) Mhe. Spika, tuliwahi kuuliza katika Baraza hili kwamba uwanja wa ndege wenye hali ya kimataifa pia unataka uwe na

udhibiti wa watu wanaotumia maeneo mbali mbali ikiwemo eneo la VIP. Pamoja na jibu la Mhe. Waziri wakati ule kuwa imechukuliwa hatua ya kudhibiti hali hii, agizo lile linaonekana kusua sua katika utekelezaji wake. Sijui Mhe. Naibu Waziri atatuambia nini kuhusu hili ili kuzidi kukiimarisha kiwanja chetu ili kiwe kweli na hadhi ya kimataifa ambapo matumizi yake yanalingana na viwango vilivyowekwa kimataifa.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, madhumuni makubwa ya kufanya *partition* nje ya jengo la uwanja ni kupunguza msongamano wa watu wanaoingia ndani. Malengo makubwa ni kwamba wale watu ambao watakuwa wanasubiri ndege kuondoka. Kwa mfano ndege inaondoka saa 8:00 amefika uwanjani muda wa saa 6:00 baada ya kuingia ndani na kwa kuwa tuna udogo wa eneo au upungufu wa viti, basi mtu yule atasubiri kule nje.

Mhe. Spika, siamini kwamba *partition* ile itaharibu mazingira au itatuharibia taswira ya nchi yetu. Naamini malengo yale ni kwa ajili ya kupungua usumbufu na mrungikano wa watu ndani wale ambao wanastahiki kusafiri watafanyiwa *check* na huduma nyengine za muhimu pale pale watakapokuwa wanasubiri nje.

Mhe. Spika, ni kweli Mhe. Waziri alitangaza msimamo na utaratibu mzuri kwa matumizi ya eneo la watu mashuhuri. Nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba mpaka muda huu bado agizo lile lina legalega. Lakini kulega lega huko kunatokana na sababu. Mhe. Spika, eneo hilo la watu mashuhuri ni eneo muhimu. Kwa hivyo, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano tumeona ni vyema tukashirikiana na taasisi nyengine katika kupanga utaratibu mzuri ikiwemo kuwatambua watu, kuandaa utaratibu wa vitambulisho na vitu vyengine ili tusije tukasababisha usumbufu na matatizo mengine hapo mbele.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Mhe. Naibu Waziri utakubaliana na mimi kuwa sehemu ya kuchukulia mizigo ikawekwa viti ili wananchi wanaosubiri mizigo kuondosha usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, sikubaliani na mawazo yake.

Nam. 92

Uuzaji wa Fukwe

Mhe. Ashura Sharif Ali – Aliuliza:-

Uvuvi ni kati ya ajira za wananchi wanaoishi karibu na bahari na mara nyingi wananchi hao hutumia fukwe za bandari kuegesha vyombo vyao. Kwa kuwa sasa maeneo mengi yanauzwa na kutumika katika shughuli za kitalii.

(a) Je, serikali haioni kufanya hivyo ni kusababisha usumbufu kwa wananchi hao?

(b) Je, serikali haioni kuwa kuendelea kuuza fukwe za bandari sehemu ambapo wavuvi hutumia kuegesha vyombo vyao na kufanya mauzo pamoja na manunuzi ya samaki ni kuwanyima wananchi hao ajira zao binafsi?

(c) Je, serikali itachukua hatua gani, ili kuhakikisha kuwa sehemu chache zilizobaki zinalindwa na wananchi waepukane na usumbufu huo?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 92 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, serikali haijauza ardhi katika maeneo ya fukwe kwa Wawekezaji, bali inachofanya ni kuyakodisha maeneo hayo kwa mikataba maalum. Aidha, maeneo ya fukwe yanabaki kwa matumizi ya wananchi wote.

(b) Kama nilivyoeleza hapo awali kwamba fukwe zitabaki kuwa ni mali ya wananchi, wananchi wana haki ya kuzitumia fukwe kwa shughuli zao za kiuchumi na kijamii. Aidha, sheria inawakataza Wawekezaji na mtu yeyote yule kujenga nje ya mita 30 kutoka mahala yanapofikia maji makuu.

(c) Mhe. Spika, serikali itaendelea kutetea maslahi ya wananchi wake katika uwekezaji utakaofanywa, ili wananchi waepukane na usumbufu wa aina yoyote. Suala la msingi ni kuwaelimisha wananchi kuingia ubia na Wawekezaji badala ya kuchukua fidia au kuuzwa.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika kwa kunipata fursa ya kuuliza swali la nyongeza.

(a) Je, kwenye mikataba hiyo ya ukodishwaji kimo kipengele kinachotoa fursa kwa wawekezaji kujenga ndani ya fukwe?

(b) Ikiwa kama halimo au halimo ni lini serikali itaanza kuwavunjia wale wawekezaji waliojenga maeneo hayo ya fukwe pamoja na *jetty*?

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, rudia swali lako.

Mhe. Ashura Sharif Ali: Ahsante sana Mhe. Spika.

Ikiwa kama halimo au halimo ni lini serikali itaanza kuwavunjia wale wawekezaji waliojenga maeneo hayo ya fukwe pamoja na *jetty*?

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, wizara kwa kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar italishughulikia suala hilo wakati wowote inapohitajika.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kuwa madai ya uvamizi wa fukwe yamekuwa yakitolewa siku hadi siku, yaani kila siku wananchi wanalalamikia juu ya tabia ya wawekezaji kujenga kwenye fukwe.

Vile vile hata jana Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati alizungumzia kuhusu suala la uvamizi wa eneo la fukwe hapo Maruhubi. Kutokana na kwamba serikali hadi sasa imeshindwa kusimamia nidhamu ya matumizi ya fukwe.

Je hivi sasa serikali inaweza kutanga rasmi wananchi wachukue hatua mikoni, ili kudhibiti ujenzi wa *jetty* kwenye fukwe? *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, kwa kweli tukiangalia sisi wenyewe wananchi ndio tunaofanya mambo haya, kwa sababu ya kusema hivi yeye Mhe. Mjumbe ni kweli hayo mambo anayajua, lakini tunatakiwa tuelimishe jamii sisi wenyewe. Kwa mfano, wale wanaoishi karibu na sehemu za fukwe waweze kuchukua utaratibu pamoja na kufuatilia, ili haki zetu hizi zisitutoke.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri ameeleza kwenye majibu yake kwamba serikali haijauza fukwe, hivyo fukwe ni kwa

ajili ya wananchi wote wakiwemo akinamama, ambao huwa wanapanda mwani pamoja na kuvua chaza.

Kwa kweli kwenye fukwe zetu hizi shughuli za kitalii zimekuwa akhasi na kupelekea vitendo ambavyo vinaleta ushavishi na hatimaye kupelekea kwenye maambukizi ya UKIMWI.

Je, kuendelea kuiachia kama ilivyo Sekta ya Utalii na sehemu zile wananchi wanaendelea kuzitembelea, sasa ile dhamira ya kudhibiti janga la UKIMWI katika nchi yetu tutaifikia?

Mhe. Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, naomba niweke sawa kwa Waheshimiwa Wajumbe walioulia maswali kuhusu dhana nzima ya uwekezaji. Kwa ufupi ni kwamba Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo haihusuki na masuala ya uwekezaji, isipokuwa inahusika na utoaji wa leseni au vibali vya kufanya shughuli za kitalii na wala sio ujenzi katika fukwe. Kwa hiyo, naomba lieleweke hivyo.

Mhe. Spika, kama nilivyoeleza awali ni kwamba suala la utalii ni upanga wenye sehemu mbili ambazo zote zinakata, kwa maana kuna faida na hasara. Lakini pamoja na hivyo, tunaweza kuutumia kwa ufanisi kabisa. Kwa mfano, hata mafuta tutakapochimba mafuta basi kuna hasara na faida kwa masuala ya mazingira.

Kwa hivyo, ni kwamba sisi tunayo mikakati mizuri ya kurekebisha hii hali nzima ya utalii hapa, ndio maana tumesema hatutaki kufanya kosa kwa Pemba, kwa sababu Pemba nako tunataka kuweka masuala ya utalii, lakini tunataka kufanya uangalifu wa hali ya juu.

Tunakubali kwamba kweli kuna makosa ambayo tuliyafanya, hivi sasa tumo katika hatua hiyo ya kwanza ya kuhakikisha utalii huu uwe wenyewe wanufaa kwa Wazanzibari, yaani uwe unajali silka na mila za Wazanzibari.

Vile vile napenda kuwaeleza wazee kupitia kwako Mhe. Spika, kwamba sisi tumeweka sehemu za utalii kule pwani, ili watu wasiwe wanakwenda ovyo ovyo kule na ndio maana tukaweka mbali na watu. Lakini tunajua kitua ambacho kiko ndani ya jamii, sasa sirahisi binadamu kumzuia kiasi hicho.

Hata hivyo, tunajaribu kuzipitia sera upya, kwa sababu sheria pamoja na kanuni zote zipo, lakini bado hazijatekelezwa kikamilifu. Kwa hivyo, tumo njia kwa ajili ya kuweka sera mpya kabisa za utalii huu ambao tunautaka sisi. *(Makofi).*

Nam. 31

Ujenzi wa Hospitali ya Wagonjwa wa Akili, Pemba

Mhe. Rashid Seif Suleiman – Aliuliza:-

Ule mpango wa wizara wa kujenga Hospitali ya Wagonjwa wa Akili, Pemba umefikia hatua gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya – Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 31 kama ifuatavyo:-

Mhe. Spika, taratibu za kumpata Mkandarasi wa ujenzi wa Mrengo wa Afya ya Akili (*Mental Wings*) – Wete Pemba tayari zimekamilika. Mkandarasi aliechaguliwa ni Kampuni ya *STANCE TECHINIC ENGINEERS* na kazi za ujenzi zimeshaanza, ambapo kwa mujibu wa mkataba, ujenzi huo utachukua wiki arobaini (miezi kumi) hadi kukamilika kwake.

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri napenda kumuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa wananchi ambao wenye wagonjwa wa akili kutoka Pemba wanasumbuka sana na usafiri na hivi sasa ni muda mrefu hali zimekuwa ngumu hata za hao wenyewe kusafiri.

Je, Mhe. Waziri anawaeleza vipi wananchi, kwamba wategemee kuanzia ile Hospitali ile itafanyakazi, pamoja na kwamba alivyosema ujenzi ule utachukua muda wa wiki 40, lakini kuanza kazi inategemewa kuanza lini?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kazi itaanza mara tu ujenzi utakapokamilika. *(Makofi)*

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza kama hivi ifuatavyo. Mhe. Spika, tukiacha mbali majaliwa ya Mwenyezi Mungu *Subuhanahu Wataala* kwamba huwajaalia viumbe wengine kuwa na ugonjwa huu wa akili.

(a) Ni sababu zipi nyengine za kidunia ambazo zinasababisha ugonjwa huu wa akili, kwa sababu kila siku tunawaona wagonjwa wapya majiani?

(b) Unguja kuna idadi gani ya wagonjwa hawa?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, kwa kweli kama alivyosema Mhe. Mjumbe kuwa majaaliwa ya Mwenyezi Mungu ni moja ya sababu. Lakini pia kuna sababu nyengine ambazo husababishwa na binadamu kama vile madawa ya kulevya, uvutaji wa bangi, tunaamini kurogana kupo na mimi sina uhakika, lakini watu wanaamini hivyo. *(Makofi)*

Sababu nyengine maisha yakiwa magumu, yaani *frustration*, kudhalilishana kimaisha pia nako kunamfanya mtu aharibikiwe na akili. Kwa hivyo, tukitaka hayo yapungue, kwa sababu ni mzigo mkubwa na hivi sasa ni watu wengi ambao wanaugua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, wagonjwa wa akili hatuwezi kusema ni idadi gani, kwa sababu wanaingia na kutoka. Kwa mfano, kuna wanaoingia na kupona kabisa na kurudi na wengine wanakwenda na kurudi. Kwa hivyo, ukisema uweke idadi ya inakuwa ngumu, isipokuwa idadi ya walioingia hiyo inaweza kupatikana, lakini ni kusema hivi sasa wapo wangapi wakati wengine watakuwa wameshapona na hilo nitashindwa. Lakini kwa wale walioingia kwa mwaka basi hilo naweza kukupatia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi: Mhe. Spika, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa wagonjwa wa akili Pemba wapo na wanaendelea kuwepo na kwa sababu hospitali hii inayotarajiwa kujengwa bado haijamalizika na itamalizika baada ya wiki 40.

Je, Mhe. Naibu Waziri hivi sasa wagonjwa wa akili Pemba kutokana na usumbufu wa kuwasafirisha kuja nao Unguja, wizara yako ina mpango gani wa kuwaekea sehemu mbadala kabla ya kumalizika kwa jengo hili?

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, mgonjwa wa akili anahitaji aina maalum ya matibabu na wala sio suala la kumchukua na kumfungia pahala, kwa kweli kuna mambo mengi ambayo yanahitajika. Kwa hivyo, ili mgonjwa yule atibike inabidi aweke katika utaratibu uliopo, dawa zilizopo pamoja na uangalizi wa aina yake. *(Makofi)*

Sasa kwa Pemba nafasi hiyo hatuna, hiyo utaratibu uliopo wanapopatikana wagonjwa kama hao inabidi wasafirishwe na waletwe Zanzibar kwenye Hospitali ambayo ina wataalamu pamoja na yale mahitaji yote wanayotakiwa kuyapata. Kwa hivyo, Pemba itaweza kufanya hivyo pale tu patakapokuwa na hospitali ambayo hiyo inayojengwa Wete na ikimalizika watapata huduma zinazostahiki. *(Makofi)*.

Nam. 59

Uvamizi wa Ardhi Vitongoji

Mhe. Saleh Nassor Juma – Aliuliza:-

Kwa kuwa ardhi ya Makaani iliyopo Jimbo la Wawi katika Kijiji cha Vitongoji ni muhimu kwa ajili ya kilimo, mifugo pamoja na uchimbani wa mawe kwa ajili ya kujengea na biashara, jambo ambalo ni muhimu sana kwa ajili ya maisha ya watu na maeneo hayo. Kwa kuwa wafanyabiashara, wanasiasa pamoja na watendaji wa serikali tayari wamevamia maeneo hayo, kwa ajili ya uwekezaji na hatimaye wanawanyanyasa wananchi pale wanapoitumia ardhi hiyo katika shughuli za kilimo na ufugaji.

(a) Je, serikali inafahamu kadhia hiyo?

(b) Na kama inalifahamu tatizo hilo serikali ina mpango gani wa kuwaokoa wananchi hao wanyonge dhidi ya unyanyasaji huo?

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati – Alijibu:-

Mhe. Spika, ahsante kwa idhini naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 59 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Spika, ni kweli kuwa eneo la Vitongoji linatumiwa na wananchi wa taasisi nyengine kwa shughuli za kilimo, mifugo na shughuli za kiuchumi na kimaendeleo. Wizara yangu inafahamu kuwa eneo hilo halijavamiwa na wanasiasa, wafanyabiashara pamoja na watendaji wa serikali, lakini badala yake imepangiwa matumizi mazuri ya ardhi.

(b) Mhe. Spika, wizara yangu haipendelei kuwanyanyasa wananchi wake katika matumizi yoyote ya ardhi katika eneo la Vitongoji, yapo maeneo yaliyotolewa kwa shughuli za ujenzi wa Chuo Kikuu Huria, eneo kwa ujenzi wa Kituo cha Mayatima, eneo kwa uchimbaji wa kifusi lililopewa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano pamoja na eneo jengine lililopimwa viwanja na kugaiwa wananchi.

Mhe. Spika, penye vipando na mali za wananchi katika eneo lolote kati ya matumizi hayo, wanapaswa kulipwa kama taratibu za nchi zilivyowekwa huo sio unyanyasaji.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Spika. Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri ameeleza katika majibu yake kwamba kuna maeneo ambayo serikali imayapanga kwa matumizi maalum, ambapo maeneo hayo tokea enzi za wazee wananchi wa Vitongoji walikuwa wakiyatumia kwa ajili ya maisha. Kwa kweli mpaka hivi sasa Masheha pamoja na kamati zao wanaendelea kuzitoa sehemu hizo kinyemela kwa wafanyabiashara na ushahidi upo.

Je, kwa kuendelea kufanya hivyo, Mhe. Spika si kuwadhalilisha wananchi wa maeneo hayo?

Je, kama wataendelea kuondosha katika maeneo yale wananchi wa Vitongoji, siku moja wakiamua kwenda kwa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais ofisini kwake na sahani, vijiko pamoja na watoto wao kwa ajili ya kuomba chakula, hawataeleweka vibaya?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, kwanza nampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyatoa yale ya msingi. Kwa hivyo, napenda kueleza kwa kifupi sana kwamba ardhi zote ni ardhi llhaliya, yaani zile ardhi tupu ziwe za maweni, gesini hizi zote zimetangazwa tokea mwaka 1964 kwamba ni ardhi za serikali.

Kwa hiyo mtu yeyote anayekwenda kuitumia ardhi ile wakati serikali haijaipangia, basi mtu huyu anayo haki ya kuitumia na wala si kuweka vipando vya kudumu, isipokuwa ni vipando vya kupita. Mhe. Spika, serikali inapopanga mipango yake na kutaka kuitumia ardhi ile mtu ambaye yupo pale anaondolewa kwa mujibu wa utaratibu, yaani analipwa fidia kwa vipando vyake na yeye anatafuta eneo jengine kwa ajili ya kujisaidia na shughuli zake.

Mhe. Spika, huo ndio utaratibu wa serikali unaotumika kwa maeneo yote ambayo serikali inahitajia ama kumpa mwekezaji au kujenga kituo chochote cha serikali kwa manufaa ya taifa hili. Kwa hivyo, huo si unyanyasaji na neno hili limetumika kisiasa na pengine angetumia ni usumbufu na mengine, lakini unyanyasaji lina maana kubwa sana. Kwa maana hiyo, nchi au serikali hii hakuna anayetaka kumnyanyasa mwenzake.

Sasa tukubaliane kwamba matumizi ya ardhi anayoizungumza Mhe. Mjumbe imetengwa kwa ajili ya matumizi ya kitaifa, ambayo Mhe. Naibu Waziri ameyataja na hayo sote tunakubali ni matumizi sahihi. Kwa kweli wananchi walipoondolewa walilipwa fidia na wako wengine ambao wamepimiwa maeneo mengine kwa ajili ya kutumia kwa haja zao kama vile kilimo na kadhalika. Mhe. Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuulizwa swali moja la nyongeza. Kwa kweli nakubaliana na majibu ya Mhe. Waziri kuwa ardhi llhaliya ni mali ya serikali, lakini pasipo na watu hapana serikali kwa hiyo ni mali ya wananchi ni kabidhi ya serikali, maana yake ifanyekazi kwa maslahi ya wananchi.

Mhe. Spika, kwa mujibu wa taarifa za manung'uniko wakati alipokuwa akijibiwa Mhe. Saleh Nassor Juma ameniambia kwamba wananchi katika hayo maeneo ambayo aliyokuwa akiyazungumza tokea zamani walikuwa wakilima, yaani hata kabla ya Mapinduzi.

Kwa hivyo, kama ilikuwa kunakuja mageuzi kwa maslahi ya uchumi wa nchi, kwa nini hawakushauriwa wananchi mwanzo na kupewa sehemu nyengine pamoja na fidia na badala yake utaratibu unaokwenda ni kama Mhe. Mjumbe alivyouliza? Hilo ni swali la mwanzo.

Pili kwa mujibu wa swali ni huwa ardhi hii imevamiwa na wanasiasa, watendaji wa serikali pamoja na wafanyabiashara, yaani ni makundi matatu. Kwa hivyo, ninaomba kujua kila kundi limevamia kwa shughuli gani na kweli wizara ilihusika hiyo nafasi?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, serikali isingeweza kulizuia eneo kwa muda mrefu sana wakati bado serikali haijakuwa tayari kulitumia, ndipo lilipoliacha eneo lile kwa matumizi ya wananchi kwa ajili ya kupata riziki zao. Lakini inapofika wakati serikali inataka kulitumia, basi mipango mizuri inapangwa na wananchi wanarifiwa, penye fidia wanalipwa fidia na halafu eneo lile serikali inalichukua kwa lengo la kulitumia kwa faida ya taifa.

Mhe. Spika, kuhusu swali (b) namuomba Mhe. Mjumbe arejee.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe rudia swali.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Spika, swali mama linasema kuwa eneo hilo limevamiwa kibiashara, kisiasa na watendaji wa serikali, yaani ni makundi matatu tofauti. Kwa hivyo, naomba kujua kila kundi limevamia kwa mradi gani wa maendeleo, mpaka serikali ikatoa hayo maeneo na kweli serikali ilihusika kutoa maeneo kwa kila sekta ambyo imetajwa humu?

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, eneo linalozungumzwa halikuvamiwa na mwanasiasa, mfanyabiashara na wala mtu mwengine yeyote. Hivyo, eneo hilo limechukuliwa na serikali, kwa ajili ya kuligawa kwa Chuo Kikuu Huria na Wizara ya Miundombinu na

Mawasiliano, ili wapate nafasi ya kuchimba kifusi kinachotumika kwa ujenzi wa barabara, ambapo barabara hizi ni kwa faida ya taifa.

Mhe. Spika, kama eneo hilo bado halijatumika liko tupu, basi Mzanzibari yeyote anaweza kulitumia eneo hilo kwa faida yake, kwa ajili ya kulipatia riziki na wala huo si uvamizi. Kwa kweli katika kijiji kuna kuwa na Uongozi wa Kijiji, kama vile Sheha, Widani na kadhalika. Hivyo, haiwezekani eneo lichukuliwe na Diwani au Sheha wote wamenyamaza na halafu tulalamike kuwa eneo hilo limevamiwa, hapana. Kwa hivyo, eneo hilo halikuvamiwa na mwanasiasa wala na mkubwa, isipokuwa eneo hilo limechukuliwa na serikali

UTARATIBU

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, Kanuni za Baraza ibara ya 59(3) ukurasa wa 39 Mambo Yanayofaa na Yasiyofaa Kuzungumzwa, Mhe. Spika naomba kunukuu kidogo.

Kanuni za Baraza ukurasa wa 39 ibara ya 59(3) kinasema hivi:-

> "Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani, atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha tu na Spika au Mjumbe mwengine yeyote anaweza kumtaka Mjumbe huyo anayesema atoe uthibitisho kwa usemi wake unaohusika".

Sasa katika kuweka *hansard* sawa Mhe. Spika, maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya Chuo Kikuu Huria wala lile lililotengwa kwa ajili ya kifusi sio eneo ambalo ninalolizungumzia, isipokuwa ni ardhi ya Makaani ambayo imeanza Diko la Vumba mpaka sehemu za Makoba ambalo liko kwenye *Costal Plane* ambako kuna Hoteli inayoitwa Mbuyu Mkavu pamoja na maeneo mengine.

Kwa kweli wamechukua wafanyabiashara, watendaji wa serikali pamoja na wanasiasa na wala sio maeneo hayo. Mhe. Spika, sina tatizo na eneo ambalo linachimbwa kifusi wala lile ambalo limetengwa kwa ajili ya Chuo Kikuu Huria, kwa sababu eneo hilo tayari limeshalipwa fidia. Sasa maeneo ambayo ninayozungumzia ni hayo na wala sio haya aliyoyasema Mhe. Waziri. Ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Mjumbe, anasema kwamba maeneo unayoyajibu Mhe. Waziri ni tofauti na yale maeneo aliyouliza katika swali hili. Sasa kama hivyo ndivyo, basi nafikiri jambo la msingi ni kufuatilia maeneo hayo ambayo ameuliza Mhe. Mjumbe kwa kushirikiana na Mjumbe mwenyewe

pamoja na viongozi kama vile Masheha na wengine, ili kuona kwamba je upo uvamizi huo au laa. Kwa hivyo, kama upo huo uvamizi umefanywa na nani kama alivyouliza Mhe. Mjumbe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, nadhani nielekeze hivyo, ili tuweze kuondoa hili tatizo. Mhe. Waziri kuna zaidi.
Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati: Mhe. Spika, nakubali ushauri wako. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunashukuru na tunaendelea.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato ya Wizara ya Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala kwa Mwaka wa Fedha 2011/2012

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Ussi Jecha Simai: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kama ifutavyo. Kabla ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwa wazima wa afya, lakini pia kutujaalia amani na utulivu katika nchi yetu jambo ambalo ni faraja kwetu na linatusaidia katika kuendesha mambo yetu bila ya matatizo.

Lakini la pili nampongeza Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Katibu Mkuu, Wakurugenzi pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara hii kwa juhudi kubwa ambazo wamezifanya za kuandaa hutuba hii nzuri na kufikia hadi hivi sasa kuwa katika majadiliano nayo.

Mhe. Spika, mimi moja kwa moja nitaanza ukurasa wa 28 mpaka 31 Chuo cha Utawala wa Umma kwanza nakipongeza Chuo kwa juhudi kubwa ambazo wamezifanya hadi kufikia kufundisha kozi mbali mbali katika chuo hiki. Katika Chuo hiki nimeona fedha ambazo zimetendwa hapa kwa ajili ya kazi za maendeleo Shs. 385,490,000. Kutokana na matatizo ambayo Chuo hiki kinapambana nayo hasa ya majengo, chuo kilikuwa kikichukua gharama kubwa sana kwa kukodi majengo kwa ajili ya kuendesha shughuli zake, kwa hivyo katika hili mimi naiomba serikali kifungu ambacho kimeingiziwa chuo hiki ni kidogo, kwani chuo hiki kinakabiliwa na ujenzi wake ulioko pale Tunguu.

Mhe. Spika, naiomba serikali kwa hapa ingeliongezea angalau kifungu kidogo kwa ajili ya kusaidia ule ujenzi na kile Chuo mwaka ujao wa fedha

kikaanza kufanya kazi ili wanafunzi wetu wapate nafasi nzuri lakini pia na wafanyakazi wetu.

Mhe. Spika, sasa nitazungumzia suala la mishahara ya wafanyakazi kwanza niipongeze Wizara kwa juhudi kubwa waliyochukua ya kufanya mapitio na hatimae kuongeza mishahara kwa asilimi 25% hili ni jambo la kushukuriwa, pamoja na nyongeza hizi ambazo zimeingizwa kwa wafanyakazi wetu jambo ambalo linatushangaza na kutushtusha kwa sasa ni muda mrefu ambao nyongeza hizi zitaanza kuingizwa na wafanyakazi wetu watapata. Siku zote tunaambiwa tuige lakini katika kuiga tuige mambo mazuri katika awamu zilizopita huu mfumo tumeurithi na huu mfumo kwa kweli sio mzuri na kuna haja serikali yetu ya awamu ya saba kubadilika na kuanza tu pale ambapo mishahara inaingizwa katika bajeti sasa ianze kutumika kwe mwezi unaofuata huu ndio utaratibu mzuri sana.

Mhe. Spika, kwa haraka haraka niingie katika suala la ajira kwa sasa tuna Wizara yetu ambayo inashughulikia masuala ya uajiri kwa jumla kuna jambo moja ambalo linanishangaza na sijapata kusikia duniani suala la walimu, kwa kuwa walimu sasa hivi serikali yetu labda imeona hawana umuhimu mkubwa mimi naweza kuthubutu kusema hivyo kwa sababu tuna walimu wengi ambao wamesoma ngazi ya cheti, lakini hata wale wea diploma pia nao wapo na inasemakana kwamba watakaoajiriwa watu 80 ni wale ambao wamesoma mafunzo ya sayansi ya diploma. Kwa hivyo mimi naomba na naishauri Wizara pamoja na serikali pamoja na kwamba tunavyodhani sisi walimu tunao wengi wa kutosha kwa madarasa madogo, lakini jambo hili mimi naona bado tunayo matatizo ya walimu katika sehemu zetu mbali mbali za maskuli na hasa hawa walimu wa ngazi ya chini.

Kwa hivyo mimi naiomba serikali kupitia hapa kwa kuwa walimu hao hakujawekwa mpango mpaka hivi sasa wa kuajiriwa basi kwa kuwa tuna Wizara maalum hii hapa, mimi ninavyoamini na ninavyofahamu kwamba walimu ni watu muhimu sana katika dunia, kwa hivyo pamoja na kwamba hatutaki kuwaajiri katika skuli zetu zilizopo basi mimi nahisi serikali ingelifanya utaratibu kwanza wa kuwachukua walim hawa ambao wamesoma kozi za ualimu na kuingizwa katika kada nyengine za serikali kwa ajili ya kuwanusuru wao pamoja na taifa kwa ujumla.

Kwa sababu mimi ninavyoamini na ninavyojua kwamba walimu ni watu muhimu mbali ya kuwa walimu hao hawatopelekwa skuli , lakini watakapofanya kazi katika sehemu nyengine watatusaidia na watasaidia taifa kwa ujumla, siku zote tumekuwa tukiona Mhe. Spika, kazi ngumu sana katika taifa kwa mfano masuala ya uchaguzi na mambo mengine huwa wanachukuliwa walimu. Lakini leo tunasema kwamba walimu hawa hatutowachukua na sijui serikali itawafanya nini walimu hawa.

Kwa hivyo nashauri serikali iwachukue walimu hawa watatusaidia mbali na kufundisha watakapokuwepo maskulini kwa kuwa hatuna nafasi hizo za kuwaajiri sasa , basi mimi nahisi tuwachukue katika sehemu nyengine watatusaidia katika hiyo hiyo kazi ya kufundisha pengine katika mambo mengine.

Mhe. Spika, nisichukue muda mrefu nimalizie hapa mpaka Mhe. Waziri atakapokuja katika kitabu hiki nimeona kuanzia mwaka 2007 mpaka hivi sasa kwamba mfumo wa mishahara ambao ulikuwa unalipwa ni kuongeza pamoja na maposho pamoja na mishahara kwa pamoja, jambo hili limelalamikiwa sana hata mimi nilipokuwa mfanyakazi wa serikali nilikuwa nalalamika sana kwamba jambo hili limepelekea Wakurugenzi na Makatibu Wakuu kuonekana kwamba wanachukua kiwango kikubwa cha fedha. Sasa Mhe. Waziri atakaposimama hapa labda atueleze je hawa Wakurugenzi na Makatibu Wakuu labda nao wamo katika huu mfumo mpya wa sasa au ni wafanyakazi wa kawaida tu.

Mhe. Spika, nakushukuru ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Rashid Seif Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kutupa uhai, uzima na toufiki ya kuzungumza katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, ikiwa serikali inaambiwa ina kiwili wili na moyo basi moyo wa serikali ni wizara hii, kwa sababu kazi ya moyo ni kukusanya ule mtiririko wa damu uliokwisha chumwa ule na kupeleka katika mishipa yote iliyopo kwenye kiwili wili na halafu kukusanya ule ambao ni taka taka na kupeleka katika sehemu nyengine na kutoa. Kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri kwanza napenda nimshukuru kwa hotuba yake fupi, nzuri, inayoeleweka na inayokwenda na wakati.

Lakini pia kwa sababu ni Wizara mpya na ilileta sheria mpya kwa hivyo namuomba sana Mhe. Waziri akumbuke maneno ya sasa ndio Mwanasheria wetu Mkuu wa Serikali na tunae humu ndani, aliposema kwamba t uanze kwanza halafu tutajiona tulipoweka kasoro, tulipokosea tuweze kukubali kujisahihisha na kuendelea mbele, hilo ndio la mwanzo Mhe. Spika.

Lakini la pili Mhe. Spika, tuje katika kitabu hiki ambacho Mhe. Waziri ametuletea alisema hapa moja katika majukumu makubwa ya kusimia utendaji wa watumishi wa umma ili kuwahudumia wananchi kwa kiwango cha juu, ufanisi na kuimarisha utawala bora nchini, kwasababu kimeingizwa kitendo cha utawala bora sio tu watumishi wa umma wafunzwe utawala bora. Lakini hasa wasimamiaji wao, sitaki kwenda mbali lakini tuchukue

kifungu kimoja tu cha wataalam waliotambua utawala bora kitu kinachoitwa *responsible* maana yake nini, ni mwananchi kutekelezewa haja yake katika wakati muafaka na ile haja yake.

Sasa waheshimiwa watumishi wao sio wananchi wakubwa wao ni wale wakubwa wao wa kazi wananchi kwao ni mtu aliyepita tu, na wakati hii inaitwa *public service* yaani huduma ya umma. Kwa hivyo naomba kwamba funzo la mwanzo kwa Wizara hii ambayo inapaswa kulitoa ni kuwafahamisha watumishi wote wa umme kwamba ni nani hasa mteja wao, isiwekuwa kazi anayopewa na bosi wake tu ndio anayoijali lakini akija mawananchi anamtizama kwa jicho la kwamba kama hamfahamu.

Mhe. Spika, tunapokwenda maofisini mambo mawili tu ndio yanayokusaidia ukaribu wako na yule anayefanya kazi ikiwa pengine ni jamaa yao au jirani yako au ukubwa wako wa cheo popote ulipo, tuseme ukweli hayo ndio mambo yanayosaidia katika utumishi wetu wa umma mwananchi wa kawaida haonekani kwamba ana nafasi katika kuhudumikiwa katika maofisi yetu mengi, Kwa hivyo ikiwa lipo jambo ambalo wanataka kutunzwa watumishi wetu ni kuwa nani hasa mteja wao hilo la mwanzo Mhe. Spika,.

Lakini la pili ni kuhusu uwajibikaji mimi nasema bila ya kuwajibishwa hawazi kuwajibika yoyote, kwa sababu ikiwa hakuna adhabu yoyote ya kazini kwa mujibu wa jambo alilolifanya sio kwa mujibu wa matakwa ya bosi wake, basi sio rahisi kuwarekebisha wafanyakazi wetu. Sasa hapa nakuja kwenye ile Tume ya Utumishi kwa sababu nataka niiunganishe kabisa, mimi nineangalia tume ya Utumishi ya Kenya mipaka yao ni mizuri sana kwa sababu wanasema wao sio kwamba wanangojea ipelekwe kesi, wao kazi yao ni mfululizo daima wanatizama muundo wa utumishi na namna gani wanavyofanya kazi. Kwa hivyo kila wanapokutana wanakuwa wanatathmini juu ya muundo wa utumishi na namna unavyofanya kazi wapi panakosea na kwa nini kesi nyingi zinakuja upande huu huku.

Kwa mfano kuna kesi nyingi wakuu wa kazi wanawashtaki watu ni kwa sababu ya wao wale au kuna kitu kimekosewa au kuna wananchi wanaripoti kwamba hawati huduma za kutosha kwani kuna kitu gani kilichokosekana, kwa hivyo mimi nafikiria kwamba tungeangalia vile vile hii tume ya Utumishi serikalini ingeangalia na vigezo vya nchi nyengine katika Jumuiya ya Afrika ya Mashariki ili ikaona kwamba je, ule uwezo wao walionao au kazi wanazozifanya zinakwenda sambamba na hii Jumuiya ya Afrika ya Mashariki au laa.

Mhe. Spika, tukija katika hiyo hiyo Tume ya Utumishi pamoja na wizara yenyewe kuna zile kanuni za mfanyakazi wenzetu wanaita *condom contract* zile ni muhimu sana, mfanyakazi yoyote aweze kuona kwamba utaratibu wa

kazi ni huuna yeye anapaswa kufanya hili na hili na akifanya hivi atapatiwa *promotion* hii akifanya hili atapatiwa adhabu hii. Hili ni muhimu sana tuwe nalo wenyewe zamani ikiitwa G.O *General Order* ilikuwa wakuu wa kazi hawapati tabu, linapotokezea jambo tu yeye anafungua kitabu cha G.O anaangalia, sasa kwa sababu tunasema tunaangalia upya uzuri tuwe nacho tokea mwanzo tuweze kuwapatia kila mmoja.

Lakini Mhe. Spika, katika kila wizara sasa hivi kuna Idara ya Utumishi na uendeshaji kama hivi kama sijakosea, kwa sababu kuna Idara ya Mipango na Sera kuna Idara ya Utumishi na Uendeshaji, mimi ningefikiria kwamba Idara hizi kwa sababu ni maarufu katika kila Wizara zikaunganishwa moja kwa moja na Wizara hii ili yale yanayofanyika miongoni mwa watumishi yakaratibiwa sawa sawa na Wizara hii. Kwa sababu kila wizara inayo hii idara ya utumishi na uendeshaji sasa ukitizama zile kama ni Mkurugenzi utaona kaangukia moja kwa moja kwenye mambo ya utumishi serikalini, sasa Wizara hii ingeungana na zile moja kwa moja wakawa wanafanya kitu kilichokuwa na mwelekeo mmoja. Hilo jnengine.

Lakini nikija katika hizi Idara Mafunzo na Maendeleo ya Rasilimali watu halafu kuna Idara ya Mipango na Rasilimali watu, sasa mimi ningelitoa mawazo yangu nimesoma hapa na majukumu yao nimeyaona lakini naona hawa wanaweza wakaja kufanya kazi moja ya mwengine, sasa ingelikuwa mapema ifanyike. Lakini jambo moja humu ambalo halikutajwa humu ni kwamba sisi tunacho kitengo cha elimu ya juu, kuna bodi ya mikopo ya elimu ya juu, kuna Wizara ya Elimu, kuwe na *coordination* basi mbona haikutajwa hapa baina ya kurugenzi hizi mbili au Idara hizi mbili na hawa ndio watakapojua kwa sababu hawa ndio wanaopeleka watu nje.

Kwa mfano Mhe. Spika, vyuo vyetu vinatoa watu wa aina moja tu sasa hivi, lakini mimi nilipiga kelele sana hapa kwamba sehemu ya ufundi bado imepewa sehemu ya uzito mdogo sana, tumeona kwa sababu watu tuna maradhi mbali mbali kwa hivyo maeneo ya udakitari yamepewa uzito, lakini hakijulikani kinachotokea huko miongoni mwa viwanda kwa hivyo ufundi umepewa uzito mdogo sana, sasa katika kujenga hizi rasilimali watu tuone kwamba *field* zote ambazo tunazihitaji sisi zinapata watu. Bila ya hivyo tunaweza kuwa na watu wa aina fulani ni wengi sana lakini fani fulani hakuna kabisa, sasa hapa ndio panapotakiwa ule uratibu na kuviwezesha hivyo vyuo vyetu na kusema aa sasa lazima kutokana na mahitaji ya utumishi sasa muendeleze na fani hizi.

Kwa hivyo mimi nafikiria moja katika kazi kubwa ya hizi Idara mbili hizi za Uendelezaji Rasilimali watu bado ni *coordination* na vyuo vikuu, *coordination* na Wizara ya Elimu, *coordination* na Idara ya Elimu ya Juu

pamoja na wengine wote ambao wanatoa fursa za kwenda kusoma nje au ndani ya nchi, katika elimu za juu.

Mhe. Spika, baada ya kupata zile kanuni za kazi jambo muhimu ni kufuatwa hapa kazi zimeharibika kwa sababu mtu anajua yeye hatopimwa kutokana na kazi yake, atapimwa kutokana na kujuana kwake sasa hapo ndio zimeanza kuharibika kazi. Hapa zamani pakichapwa kazi kweli lakini ulipoanza kupanda cheo na kupewa fursa ni kutokana na kujuana kwake hapo ndio palipoanza kuharibika, kwasababu wengine wakajiona aa madhali sisi hatujulikani basin a sisi tunafanya hivi hivi kwa sababu atakayekepewa ni furani, kama tunaanza basi tuanze upya wote waone kila mmoja aone kwa kiyoo na ndio utawala bora unavyosema kwa sababu kuna kioo hapa *transparence* ionekane.

Halafu anasema katika hizo nyanja za utawala bora ni kuweka usawa na kuingizwa kila mtu kwa hivyo mtu akiajiriwa tu katika utumishi tayari ameshaingia katika utumishi wa serikali, kama anatoka wapi , anavaa kofia au havai yote haya yasijaliwe utizamwe utendaji wake wa kazi. Kwa mfano Mhe. Spika, katika kanuni zilizopita likizo bila ya malipo ilikuwa ni haki ya yule mfanyakazi akiona kwamba yeye anataka kuomba likizo bila ya malipo anaomba, lakini sasa ikatumiwa kumtia adabu yule mfanyakazi anapewa likizo bila ya malipo jambo ambalo ni kinyume kabisa na zile kanuni zinavyosema. Wakati serikali imeweka kifungu chake kwamba inapomuona mfanyakazi wana mashaka nae katika jambo fulani wanapewa nafasi ya kumsimamisha kazi miezi sita na kumchunguza, lakini akishatimiza miezi sita wamwambie una kosa tunakusamehe tunakuachisha kazi, huna kosa rudi kazini.

Lakini hao hao Mhe. Spika, wanapewa likizo bila ya malipo, hao hao wengine wanasitishwa kazi miezi iliyokuwa zaidi ya sita wala hakuna kinachoendelea, kwa hivyo utaratibu wote huu ulikuwa haufuatwi, tupigeni mstari na tunaweza kupiga mstari ili tutengeneza zile kazi kwa sababu kadri utakavyofanya uadilifu na zile kazi zako ndio zinatengenea kwa sababu yule mfanyakazi anatizama hali ilivyo.

Mhe. Spika, utendaji wa kazi kwetu mimi nilizungumza sana hata siku ile niliyopitisha ile sheria ile kwamba tufanye tathmini kwa wafanyakazi wetu kila mwaka, na aandikiwe hasa ripoti mbali ya kumtia moyo yule mfanyakazi lakini itamzuria Ofisa mwengine yoyote kuchezea ule ufanisi wa mfanyakazi kwa sababu inawezekana ikawa hakufanyiwa zile tathmini kwa muda wa miaka minne hajafanyiwa, mwaka wa tano akaja Ofisa mwengine pale kabadilishwa kwa njia moja au nyengine tu akamuona huyu kwa elimu aliyokuwa nayo, kwa ujuzi aliokuwa nao ni tishio kwangu huyu kwa hivyo akamkandamiza makusudi. Ikitakiwa ripoti ya Rasmi yeye anamuandikia

anavyotaka kwa sababu hakuna rekodi yake huku nyuma. Kwa hivyo yeye ile miaka minne ya mfanyakazi mzuri kaichezea bure, lakini kama kuna rekodi ya mfanyakazi kila mwaka inamzuia mtu mwengine kuchezea ile rekodi ya mfanyakazi, kwa sababu ataulizwa miaka mine kafanya kazi vizuri kama hivi wewe mbona unaleta ghafla ripoti hii mbaya.

Lakini kama mfanyakazi hana ripoti a kila mwaka kwanza haimpi moyo yeye mwenyewe kujua kazi zake lakini pia watu wengine wanaweza kuchezea *performance* yake baada ya kutakiwa ripoti, ndio maana wakati mwengine linateuliwa jina nini lakini ndio ameshalitangaza kwa sababu hatukutayarisha sisi zile dondoo za kumpa *performance* yake ya kila mwaka, kwa hivyo katika kujirekebisha kwetu kila mfanyakazi awekewe dondoo zake za uendaji wake wa kila mwaka na ziweko katika faili, ili zikitakiwa aweze kuzipata. Kama Mhe. Rais au Waziri aliyekuja.

Mhe. Spika, tizama saa pale hili jambo linatutia uchungu sana tunataka sana kuambiwa hii nchi yetu ina wafanyakazi wazuri, lakini tunawatengeneza sisi au tunawaharibu sisi.

Mwisho kabisa sisi wengine tunajua ishara, kwa hivyo nataka niseme neno la mwisho kabla sijaunga mkono hoja anasema utawala maana yake ni kufanya amamuzi, kwanza mtawala lazima afanye maamuzi ukikaa tu ofisini hufanyi maamuzi yoyote sio mtawala. Watu wana tatizo hili wewe unasema tutakwenda na tutaona tuko mbioni hufanyi maamuzi yoyote sio mtawala, mtawala anatakiwa afanye maamuzi na kila amuzi unalifanya lina rizki ndani yake wataalam wanasema haidhuru ndio uamuzi. Lakini vile vile anasema hayo maamuzi yanayofanywa ikiwa upo huo utawala yatekelezwe, sasa ikiwa ni mazuri ndio inapokuja maamuzi mazuri, utawala wa sheria sasa ndio unakuwa *good Government* sasa kwa hivyo tunaomba sana Wizara hii kama nilivyosema mimi siangushi maneno yangu huu ndio moyo wa kazi katika wizara zote, mtakavyoongoza wizara ndio zitakavyoongozeka.

Nashukuru sana uamuzi wa Mhe. Rais kuunda Wizara hii kuanzisha Sheria ya Utumishi Serikalini.

La mwisho kabisa naunga mkono bajeti hii kwa vile iliwapa matumaini wananchi kwamba angalau asilimia 25 watapata matumaini. Lakini wamefanya siku nyingi angalau wangewapa mwezi mmoja lakini miezi mitatu.

Mhe. Spika, naunga mkono ahsante sana.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amejujaalia asubuhi ya leo tukiwa

katika hali ya uzima na afya. Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe mwenyewe binafsi ambaye umenipatia nafasi hii na mimi niweze kuchangia mchango wangu angalau mdogo.

Tatu nimshukuru sana Waziri ambaye ametuletea kitabu chake hapa namshukuru yeye pamoja na watendaji wake wote ambao wameweza kutuletea kitabu hiki kifupi lakini kinamaana kubwa sana.

Mhe. Spika, nianze mchango kwa kumpongeza sana Mhe. Rais Dokta Ali Mohammed Shein ambaye ameanzisha wizara hii mpya. Na mwanzo wake unatufurahisha kwa hata sisi wenyewe kwa kuwa yeye mwenyewe binafsi kaianzisha lakini tunamuona katika harakati zake kama tunaweza tukafikia mahala pazuri kwa usimamizi wake.

Mhe. Spika, nianze na Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Wizara hii kama itajipanga vizuri kwa lengo la kuimarisha utawala bora nchini, utawala bora unaweza ukafikia pazuri pamoja na kuwapatia wananchi wake huduma bora ili ile dhana nzima ambayo Mhe. Rais ameipanga tutaweza kuifikia kwa kipindi kifupi.

Mhe. Spika, nianze kutoa wito na mimi katika Wizara hii kwa kuwataka watumishi wa umma tuweze kufanya kazi zetu kwa uwadilifu, bidii na nidhamu za kazi. Tukiyafanya haya naamini tunaweza tukafikia mahala pazuri. Maendeleo ya nchi za wenzetu wambao zimeendelea kwa sababu ya kutumia uzalendo katika nchi na kujituma kwa bidii kubwa ndivyo wakaweza kufikia maendeleo katika nchi yao. Na sisi tukijituma kwa bidii na kwa nidhamu ya hali ya juu tunaweza tukafikia maendeleo kwa muda mfupi sana.

Mhe. Spika, nende katika sehemu ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. kwanza nianze kumpongeza sana mama yetu huyu, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa bidii yake na uhodari wake wanaouonesha niombe tumpe mashirikiano. Sifa hizi hawezi akazipata yeye peke yake bila ya kuwa na ushirikiano mkubwa. Tuongeze ushirikiano, tuweze kumsaidia mama huyu aweze kufanya kazi zake kwa vizuri sana.

Vito wangu kwa wale maodit ambao wanapita kufanya kazi za ukaguzi wa mahesabu. Niwaombe wafanye kazi zao kwa uwadilifu mkubwa na kuacha kughilibika kwa kikombe cha chai utakachokaribishwa ukifika pale au kupewa zawadi mbali mbali ili tuweze kutimisha wajibu wetu ipasavyo, tuweze kunusuru fedha nyingi za serikali ambazo zitakuwa ni tegemeo kwa wananchi wetu kufaidika katika maendeleo ya nchi yao.

Mhe. Spika, nikitoka hapo nende sehemu ambayo imeelezewa Ukimwi, nami niigusie kwa sababu kila kitabu kinachokuja kinalizungumzia hilo. Inaonekana hili limepewa kipaumbele sana na ndio maana likawa linaelezwa.

Mhe. Spika, Ukimwi hautooondoka kwa kuandika sana kwenye vitabu wala hautoondoka kwa kuimba nyimbo nyingi ambazo zinazohusiana na ukimwi. Hili ni janga, tujunusuru nalo basi kwa kuheshimu sana ndoa zetu lakini kupiga vita yale yote ambayo yanapelekea vishawishi vya kupatikana zinaa kwa wingi.

Mhe. Spika, niipongeze tena sana hii Wizara kwa ajili ya kutoa nyongeza ya watumishi. Hapa kidogo wenzangu wamesema ni kweli nyongeza imepatikana na wafanyakazi wamefurahi, lakini ile ngoja ngoja ndio itakayokuwa inaongeza matumbo. Nimuombe Mhe. Waziri basi achangamke kwa sababu roho zimeshaingia matumaini.

Mhe. Spika, niende katika Idara ya Nyaraka ambayo ni Idara muhimu sana. Nimuombe Mhe. Waziri aitupie jicho sana kwa kuona anawapatia wafanyakazi wa Idara hii vifaa muhimu vya kisasa ili kuweza kuhifadhi zile kumbukumbu zetu na sio kama ilivyo sasa zinapotea ovyo na kusambaratika ovyo na baadaye inakuwa ni usumbufu kwa wananchi anapopotelewa na kumbukumbu yake kwenye kuifata pale, ataikuta haipo.

Mhe. Spika, niendelee na mchango wangu katika ajira. Nimeombe Mhe. Waziri kuangalia sana upande wa ajira za mahoteli. Inaelekea wawekezaji wetu kwa sasa wanajishughulisha sana kuchukua wafanyakazi kutoka sehemu zao wanazotoka na kuwakosesha haki wale wananchi wetu ambao tulitegemea wakipata ajira wataipunguzia serikali mzigo.

Mhe. Spika, nimuombe waziri aliangalie sana hili, kwa sababu kwa sasa vijana tunao ambayo tayari wameshasoma katika Vyuo vya Utalii. Awaangalie kwa jicho la huruma ili waweze kufaidika na ule uwekezaji ambao umewekwa katika nchi yao.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu ni mdogo tu, niombe kuitakia kheri Wizara hii ambayo imebeba majukumu mengi. Mwenyezi Mungu aweze kuwafanikisha waweze kuyafikia yale yote ambayo wameyalenga hasa ikiwemo elimu kwa wafanyakazi ambayo itakuwa ndio changamoto kubwa ya kuondoa matatizo yetu. Wakipata elimu hii na hisi wataweza wakatutumikia vizuri na wakawatumikia wananchi wa taifa hili kwa vizuri ili ile dhana nzima ambayo imekusudiwa ikawaza kupatikana.

Baada yakusema hayo Mhe. Spika, mimi kwa niaba yangu na kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini naunga mkono hoja asilimia mia juu ya mia.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante sana Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie hotuba hii ya Wizara ya Nchi, Afiri ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, kwa kuanzia nimshukuru Mhe. Waziri wa Wizara Mhe. Haji Omar Kheri pamoja na watendaji wake wote wakiongozwa na Katibu Mkuu Joseph Meza kwa kazi nzuri waliyoifanya na hatimaye kutuletea kitabu hichi cha hotuba ambacho kipo *shot* lakini kipo *clear*.

Mhe. Spika, mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria chini ya uongozi wa Mheshimiwa Mwenyekiti wetu ambaye ni Mhe. Naibu Spika, sitokuwa na mengi ya kuchangia kwa sababu mengi tumeshachangia kule kwenye kamati.

Mhe. Spika, kwa kuanzia naomba na mimi niungane na wenzangu kwa kumpongeza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesababu za Serikali. Ni kweli kabisa Idara na Taasisi nyengine za Serikali ipo haja ya kufika pale na kuiga mfano wa ofisi ile. Nimpongezi mama huyu pongezi nyingi sana kwa kuwajiri vijana na ndio maana kazi wanayoifanya pale mpaka ofisi hii inapigwa mfano kwamba hakuna afisi yenye utaratibu mzuri kama ofisi ile.

Mhe. Spika, wazee tunawapenda, wanahekma na busara lakini hekma zao na busara wazitumie kutuonesha sisi vijana njia za kupita na kufanya kazi. Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu asilimia nyingi ya wafanyakazi ni vijana. Kwa ushahidi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu yupo pale juu na *front line* yake kama utawatizama wote ni vijana. Aliyekuwa nao ndio wakubwa, huko ofisini ana utitiri wa vijana kama sisi, lakini wanafanya kazi za kupigiwa mfano. Naomba na wizara nyengine zisinyime nafasi vijana, viwapatie nafasi vijana wafanye *wanders* kama wanazozifanya kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Mhe. Spika, nikitoka hapo naomba niingie katika maslahi ya wafanyakazi. Nampongeza sana Rais kupitia Wizara hii kwa kuwaona watumishi wa umma na kuwaongezea asilimi 25 ya mshahara, japo kwamba watu wanapiga kelele kwamba Oktoba ni mbali. Naomba wavumilie kwani haraka haraka haina baraka, Oktoba haiko mbali, mishahara yao itaongezwa na vipato vyao vitanyanyuka.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Rais kwa kuonesha kwamba Chama cha Mapinduzi kinapoahidi kinatekeleza. Mhe. Spika, kupitia ilani ya Chama cha

Mapinduzi Mhe. Rais aliahidi katika kampeni zake kwamba atanyanyua mishahara na hivi leo hotuba hii imeshaeleza tayari asilimia 25 ya mshahara imeshaongezwa. Kupitia Baraza hili naomba wanachama wetu waendelee kutuunga mkono hili la mshahara dogo tu kuna makubwa yanakuja tumewaahidi Mhe. Spika, tutawatekelezea.

Kwa hayo machache Mhe. Spika, nilishaunga mkono hoja katika Kamati lakini kwa mara ya pili tena naunga mkono hoja mia kwa mia. Ahsante.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Kwanza nikushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikatoa mchango wangu mdogo katika Wizara hii ya Utawala Bora na Utumishi wa Umma.

Mhe. Spika, nataka nimpongeze swahibu yangu, rafiki yangu kwa kuweza kupewa jukumu hili na kuweza kuhakikisha maadili ya utumishi yanazimamiwa na haki na maslahi ya wafanyakazi wetu anayasimamia kwa vizuri.

Mhe. Spika, mimi kwanza nataka nianze kumpongeza Mhe. Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na watendaji wote wa wizara hii kwa kupewa majukumu haya mapya. Tunawaombea Mwenyezi Mungu awajaalie kila la kheri katika kazi zao hizi ili wananchi waweze kupata mafanikio makubwa.

Mhe. Spika, mimi nataka nianze kama walivyomalizia wenzangu. Niipongeze Afisi ya Mkaguzi na Mdhibiti wa Hesabu za Serikali kwa kazi nzuri waliyoifanya ambapo Mhe. Spika, katika kila mwaka hapa tukija hatujaona kasoro za watendaji wa Afisi hii isipokuwa wanatupa mwanga mkubwa sana hasa Kamati yetu ya *PAC* wanapochukua zile ripoti na wanapotuletea ripoti hizi. Tunawaombea Mungu na wao awajaalie wazidi kuendelea na kazi zao nzuri.

Mhe. Spika, nikiendelea nije katika Chuo cha Utumishi wa Umma. Nataka niwapongeze sana kwa kazi zao nzuri ambazo wanazozifanya, na kuweza kuwasomesha wafanyakazi wetu ili kuwa na taaluma ya kazi zao lakini vile vile kuwa na maadili mazuri katika usimamizi wa shughuli zetu.

Wenzangu wamezungumza sana kuhusu Idara hii, mimi nilikuwa nataka nitoe pongezi tu. Isipokuwa nilikuwa nataka kuongelea zaidi katika chuo chetu cha Utumishi wa Umma kinachojengwa pale Tunguu. Kile chuo naona kimekuwa kinasinzia pale hasa ndio shina la kuweza kutoa hao watendaji wazuri. Hii wizara ili iweze kufanikiwa katika majukumu yake basi nadhani pale ndio kwenye chimbuko la uwajibikaji huo.

Nilikuwa naomba sana ingawa hapa tumeelezewa katika bajeti ya mwaka huu imeombewa karibu shilingi milioni 855.490. Fedha hizi shilingi milioni 47 zimekwenda katika kazi za kawaida na shilingi milioni 385 katika kazi za maendeleo. Katika kazi za maendeleo sijajua kwamba hizi ndizo zimetengwa kwa ajili ya hichi chuo au vipi. Hili kidogo nilikuwa nataka Mheshimiwa aje anisaidie ufafanuzi. Kama kwa kumalizia kile chuo hizi fedha bado nahisi ni kidogo hazitoshi, chuo chetu nina wasi wasi kitaendelea kusuasua wakati wafanyakazi wetu tunahitaji wapate taaluma iliyokuwa bora.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nataka nije katika ukurasa wa 36 kifungu cha 89 ambacho kinazungumzia nyongeza ya asilimia 25 ya mshahara. Mimi kwanza nataka nimpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Hili aliliahidi alipokuwa akifanya kampeni zake za uchaguzi kwamba atahakikisha anaangalia mslahi ya wafanyakazi wote wa serikali. Mimi hapa kidogo nilikuwa nina mawazo tofauti pengine na wenzangu. Wenzangu wengi sana wamepongeza kwa hii asilimia 25 ambayo iliyoongezwa lakini bado nyongeza hii ni ndogo. Tena nyongeza hii ni ndogo sana sana sana.

Mhe. Spika, tukiangalia tunaposoma hotuba zetu za Bajeti Kuu ya Serikali tunaambiwa kwamba uchumi wa Zanzibar umekuwa kwa asilimia karibu 6.5, ukiangalia halisi jawabu ndio inakuja kama hii.

Mhe. Spika, mimi nataka nitoe mifano na nitajaribu kutoa mifano nijaribu kutoa mifano kwa nini kima chatu cha mshahara bado kipo kidogo sana. Bado tukiangalia ikiwa sisi ndio wawakilishi wa wananchi ambao sisi ndio tunapanga Wazanzibari watakula nini kwa mwaka mzima na Wazanzibari watakosa nini kwa mwaka mzima. Nikiangalia asilimia 25, sisemi kama hiyo ndio hesabu sahihi, mfanyakazi wa serikali sasa hivi kama anapata TShs 100,000/- ina maana sasa hivi atapata TShs 125,000/-. Hapa sijui tumechukua vigezo gani vya kuweza kuongeza kima hiki cha mshahara. Unaposema unaongeza kima cha mshahara ina maana unaongeza uwezo wa mwananchi katika kutumia ile *purchasing power* yake inakuwa kubwa.

Mhe. Spika, mimi kwa bahati nzuri hapa Barazani ni mkongwe kidogo. Ninakumbukumbu za nyuma na nitajaribu kuziainisha zile kumbukumbu zangu za zamani na hizi kumbukumbu za sasa hivi. Mwaka 2006 bei ya mchele ilikuwa shilingi 450 kwa kilo moja ambapo mtu akipata TShs 45,000/- ana uhakika wa kununua kilo 100 za mchele, polo kubwa la mchele au polo mbili za mchele.

Mhe. Spika, mwaka 2011 kilo ile ile ya mchele tuliyokuwa tunainunua kwa TShs 450/- sasa hivi tunainua kwa TShs 1200/-. Hapa zimeongezeka karibu TShs 800/-. Kukiangalia kwa ki *percentage* kutoka Shs 450/- mwaka 2006

sasa hivi tuko Shs 1200/- ina maana karibu asilimia 110 imeongezeka kwa asilimia 24, mwananchi baada ya kwamba tumemuongezea mshahara, tumempunguzia mshahara.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri aje atueleze amejaribu kutumia vigezo gani, au wataalamu wake wamempa vigezo gani mpaka akatwambia mshahara unaongezeka kwa asilimia 25. Nadhani hili jukumu hasa la kutangaza kima cha mshahara bora angeachiliwa Waziri wa Fedha. Mhe. Waziri rafiki yangu, swahibu yangu nitamuonea bure kwa sababu yeye hakusanyi bali yeye anakigawa kile alichogaiwa. Mhe. Waziri wa Fedha mimi nakuomba mwakani uje wewe utwambie na uwe wewe ndio unaeongeza kima cha mshahara.

Mheshimiwa tumeshakushauri sana kwa bahati nzuri yupo swahibu wangu Mhe. Waziri wa Fedha tunakwambia sisi kama Wawakilishi wa wananchi kuna fedha nyingi serikali bado hazikusanywi. Sisi tumeapa hapa kwa katiba mbili bado katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kwamba inatakiwa kufanyiwa marekebisho wakati bado Katiba ile ni nzuri sana kwa Zanzibar hasa katika masuala ya mapato.

Mhe. Spika, Katiba hatuifuati, siku zote mimi nasema Bandari ni suala la Muungano lakini utaratibu wa ukusanyaji wa mapato Bara wanakusanya zao na sisi tunakusanya zetu. Tunakosa mapato mengi Zanzibar. TRA ni suala la Muungano Bara wanakusanya zao na sisi tunakusanya zetu, tunakosa mapato mengi Zanzibar.

Sisi kwa kuwa tumeapa tutalinda Katiba, tunazitaka serikali zetu mbili zifuate Katiba. Mambo ya kusema tusubiri mpaka mwaka 2014, mimi lugha hii siielewi. Mimi nimepigiwa kura mwaka jana, mwaka 2014, nataka niende kwenye kampeni niwaoneshe wananchi wangu kwamba uchumi umekuwa na maslahi yao yamekuwa. Leo mwaka 2014 ndio Katiba tunategemea itafanyiwa marekebisho kama wananchi wataridhia ifanyiwe marekebisho. Ina maana tuendelee kusafa mpaka mwaka 2014. Madhumuni ya kuapa kwa katiba zile mbili maana yake nini. Vyenginevyo Mhe. Spika, sisi tuape kwa Katiba moja ya Zanzibar. Kwa sababu Katiba ya pili hatuitekelezi na nadhani ndio maana Mwenyezi Mungu anatuchapa bakora.

Mhe. Spika, sisi Katiba yetu ya Muungano imejaa nyama kwa maslahi ya Zanzibar. Ndio maana tukawa siku zote tunapiga kelele kwamba hizi rasilimali zilizokuwepo Zanzibar. Ndio maana ikawa siku zote tunaisukuma serikali tuchimbe hayo mafuta kama tumeyapata sawa, tumeyakosa sawa lakini tujue kwa sababu ndio *resources* ambazo zipo ndani ya nchi. Lakini haya mafuta hatujachimba, hatujayaona lakini bandari hatuzioni na mambo

ya anga kuwa ni mambo ya muungano. Hakuna mgao wowote ambao sisi tunaupata. Kuna sheria imeundwa mwenzangu kazungumza pale kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano kifungu cha 133, kimeeleza wazi wazi. Kutaundwa tume ya pamoja ambayo itashauri serikali mbili. Imeshauri tume ile, imepeleka mashauri mara ya mwanzo yamefumbiwa macho, imepeleka mashauri mara pili bado serikali zinakaa.

Mhe. Spika, kwa kweli mimi hapa sitaki niipongeze serikali, kwa sababu haitimizi wajibu wake. Wajibu wa serikali kwanza tutekeleze Katiba tukishakuteleleza Katiba sasa tena tutakuja kusema kwamba je, hii tunayo tunaweza tukaongeza. Lakini bado serikali zetu na hasa Serikali yetu ya Zanzibar kuna mapato ambayo tunayafumbia macho kwa upande wa pili wa muungano matokezeo yake tunakosa fedha.

Mhe. Spika, nimetoa mfano mmoja tu wa mchele nakuja suala la mafuta. Mafuta dizeli mwaka 2005/2006 tulikuwa tunanunua lita moja Shs 1158/- mpaka 1160 mwaka 2010 ilikuja mpaka 1567 imeongezeka karibu kwa asilimia 50. Leo nimekwenda kwenye kituo cha petroli nikakushanya data hizi bei ya petroli mbele ya diseli inauzwa Shs 2075/- wakati mwaka 2005/2006 ilikuwa ni Shs 1158/-ina maana hapa imeongezeka karibu kwa asilimia 80.

Mzanzibari hapa baada ya kuinuka kiuchumi anakwenda chini kiuchumi. Ndio maana sisi tunapouliza pale tunapoambaiwa kwamba uchumi umekuwa. Tunauliza uchumi umekuwa wa nani na vigezo vya wataalamu hapa sisi wana siasa ndio tunapokuwa hatukubaliani navyo. Leo wale wafanyabiashara wakubwa wakijenga magorofa, serikali ikijenga magorofa, ikijenga barabara ndio kigezo kwamba uchumi umekuwa. Sawa, lakini jumba alilojenga ni Turki au Abdul-Satar au Bombe-Bazar, samahani kwa kuwataja watu majina yao hapa. Lakini natoa mifano kwa wale watu wanaojenga majumba makubwa. Inachukuliwa *average* ile inafanywa na yule Mzanzibari wa chini mlalahoi kijijini anaambiwa na yeye pato lake limekua. Limekuwa wapi na kwa kigezo hichi?

Mhe. Spika, hapa sasa hivi ukiangalia sitaki mimi niseme kwamba mshahara wetu umeongezeka kwa asilimia 25, mshahara wetu umepungua kwa asilimia 60. Leo hii pesa ambayo ananunulia dizeli lita Shs 2075 ina maana mwaka 2005/2006 ilikuwa kwa 1158, ndio kaongezewa huyu, kapunguziwa.

Mimi nawaomba wataalamu hasa wa Waziri wa Fedha, mimi mara nyingi namtayarisha kabisa Waziri ili anapokuja akatwambia uchumi umekuwa basi atwambie kwa kitaalamu uchumi umekuwa hivi na hivi. Asije akatwambia king'ambu ng'ambu, Kikwamtipura Kwamtipura, atwambie uchumi

umepungua hivi. Hapo ndio nitakubaliana nayeye vyenginevyo hapa nitakuwa simuelewi.

Mhe. Waziri kwa kweli amejitahidi lakini kama nilivyosema huu mzigo aliyoubeba sio wake kwa sababu yeye hakusanyi pesa. Pesa anakusanya mwengine yeye anatangaza mshahara.

Nakuja bei ya gari, maana mimi nazungumza Kikwamtipura Kwamtipura. Bei ya gari leo mwananchi wangu wa Kwamtipura inamuia vigumu. Kwa mfano leo mwaka 2011gari ile ile aliyokuwa anaipanda kwa shilingi elfu moja leo anaipanda kwa shilingi elfu mbili, nauli imeongezeka kwa asilimia mia moja na wakati mshahara umeongezeka kwa asilimia 25.

Mhe. Spika, Nungwi tulikuwa tunapanda shilingi 1500 saa hivi ni shilingi 2000 imeongezeka kwa asilimia karibu 25. Chwaka nauli ilikuwa ni shilingi 800 sasa hivi ni shilingi 1300 kwa hesabu za haraka haraka hapa imeongezeka karibu kwa asilimia 60. Kwa hivyo, nikichukulia vigezo hivi ndio maana nikasema mimi nitachukua vigezo vya Kwamtipura kwa sababu ndio tunavyoishi navyo siku zote.

Mhe. Spika, kwa kweli ndio maana hapa tukasema kwamba bado hali za wananchi wetu ziko duni sana, lakini tujiulize kwa nini ziwe duni sana hatuna *resource* sisi za kukusanya. Kwa hivyo, Mhe. Spika, chochote tutakachokuwa tunakizungumza hapa basi wananchi wetu tutakuwa tunawadanganya na hatuwatendei haki, tunatakiwa tuzungumze ule ukweli.

Mhe. Spika, mimi bado nasisitiza tena kwamba tujaribu kuangalia zile rasilimali ambazo zimo ndani ya Katiba tuzitekeleze, zile rasilimali zilizokuwemo nchini mwetu tuzitekeleze vyenginevyo Mhe. Spika, tutakuwa tunakuja hapa tunapiga kelele lakini wananchi wetu hatuwasaidii hata kidogo.

Mhe. Spika, mimi leo nilisema sitaki niseme sana kwa sababu ninavyosema nahisi kwamba sijawasaidia sana wananchi wangu, na mimi kuwasaidia wananchi wangu ni kuhakikisha kwamba kile kipato chao kinaondoka pale walipo na kinasogea mbele. Mhe. Spika, leo sisi wawakilishi wa wananchi hapa tunaambiwa sisi ndio twenye mapesa mengi, lakini sisi ndio tunaoshuhudia umasikini uliokithiri kwa watu wetu. Mtu anakuja anakwambia Mheshimiwa nigaie japo elfu 2000 nikapate angalau chakula na watoto. Kwa hivyo, hali za wananchi wetu huko nje ni ngumu sana, mimi kitu ambacho ninachokiomba serikali ina programu nyingi tena nzuri sana tulisema katika bajeti kuu ya serikali, mwaka huu kitabu kimekuwa kizuri sana, lakini kwa nini rasilimali zilizokuwepo kwanini tunaishauri serikali zizikusanye hawatiki.

Mhe. Spika, hakuna sababu kama kuna rasilimali zinazokusanywa pande mbili za Muungano watu wakae wafungue Katiba inasema vipi. Mimi utaratibu wa kusema Zanzibar makusanyo ya *TRA* tukusanye sisi na Bara wakusanye wao sitaki. Kwa mfano, mimi nasema tunakosa mapato mengi sana kwa bandari kwani bandari ya Dar es Salaam sasa hivi ukiangalia imejaa makontena, meli zinakaa nje bandarini kwa muda wa mwezi nzima haijapata ukuta kufunga. Kuna wale wafanyabiashara wa nchi za Burundi, Rwanda na nchi nyengine wanahamisha meli zao sasa hivi wanashushia Mombasa. Hivyo, kama bandari ingelikuwa ni suala la Muungano basi wenzetu wa Bara meli nyingi zingelikuja kuteremshia hapa. Lakini kwa sababu bandari sio suala la Muungano, *TRA* sio suala la Muungano wao wanaona bora yale mapato wayakose lakini na sisi Zanzibar tuyakose.

Mhe. Spika, kutokutekeleza Katiba tunajimaliza tusiwadanganye wananchi wetu hapa sisi sio masikini. Mhe. Spika, meli zinazokuja pale Bara laiti kama zingelikuwa zinakosa kufunga gati kwa sababu ya foleni basi zingekuja kufunga Zanzibar kwani bandari ya Zanzibar ingekuwa ina makontena mengi, kazi zingeongezeka. Leo vijana wetu wanakwenda pale kwa kazi ya vibarua basi anakaa siku tatu hajapata kazi anaambiwa njoo siku ya tano wakati huku nyumbani ana mke, watoto na wajukuu.

Mhe. Spika, kwa kweli kama ingekuwa wanaziruhusu kuja hapa Zanzibari kwanza bandari ya Zanzibar itapata pesa, kodi pia itakuwa inalipwa Zanzibar hivyo kama *TRA* ni moja kwa nini tusikubaliane. Waheshimiwa Wajumbe mimi bajeti ya mwaka ujao suala la *TRA* kama serikali haijatupa jawabu kamili basi sikubali, bora nitakapokuwa mkorofi nitaendelea kuwa mkorofi lakini sitoikubali. Mhe. Spika, tufuate Katiba ili bandari tuifanye suala la Muungano kwani mapato mengi sana tunayakosa. Hii ina kuja kwa sababu gani? Ni kwa sababu ya choyo tu hakuna kitu chengine.

Mhe. Spika, mimi juzi nilizungumza hapa sasa hivi kutokana na kwamba Zanzibar kuna wafanyabiashara wengi ambao wanapeleka mizigo yao Bara, kule wanaekewa vikwazo wanalipa mara mbili yake, hapa ingawa tunasema tumeshakubaliana katika vikao lakini ukija huku hakuna kinachofanyika. Mhe. Spika, kama ingelikuwa *TRA* tunaifuata kama Katiba ni suala la Muungano basi ingelikuwa ukishanunua gari yako hapa unakwenda nayo Bara unapita mpaka Burundi labda ndio utahojiwa huko Burundi. Lakini leo kutokana na kukiuka Katiba hatuzifuati Katiba zetu ambazo tumeapa matokeo yake tunawahangaisha wananchi wetu, wafanyabiashara wa Zanzibar wanakimbia. Leo tunamsubiri Mhe. Mazrui akija na bajeti yake ya Wizara ya Biashara amesema ataanzisha viwanda vingi lakini wote watakimbia kwa sababu hapa vilikuwepo viwanda na watu wamekimbia wamekwenda kufungua Bara kutokana na kero ya bandarini.

Mhe. Spika, haya ninayoyasema mimi kama ingelikuwa yanatekelezwa basi wenzetu wa Bara mapato yangekuwa yanaongezeka na Zanzibar pia mapato yangeongezeka. Mhe. Spika, kabla hujanambia nitulie mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Kwamtipura kwa kuwa hakusanyi yeye angekuwa anakusanya yeye mapato nisingeunga mkono, lakini yeye ameambiwa alete tu utaratibu wa mgawanyo Mhe. Spika, naunga mkono hotuba hii kwa shingo upande kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Spika, mimi kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha asubuhi hii kukutana humu kuendelea na shughuli zetu za kawaida za Baraza. Mhe. Spika, pia nikupongeze wewe kunipa nafasi hii kusema machache ambayo nataka kusema leo.

Mhe. Spika, mimi katika hotuba hii sina mengi sana wala sina makubwa ya kuyaeleza, lakini kwa kuwa huko nyuma kidogo nilikuwa mfanyakazi na mimi sitokosa la kusema. Mimi nianzie kwa pencheni wanazopatiwa wastaafu wetu baada ya kumaliza muda wao wa kazi.

Mhe. Spika, wako watu wastaafu walioitumikia nchi hii kwa muda mrefu kwa juhudi zao kubwa lakini pencheni zao ni ndogo mno. Nadhani hii inalipwa kulingana na mshahara wa mtu uliokuwa, watu waliotumikia huko nyuma kwa kuwa mishahara haikuwa kama ilivyo leo wako baadhi ya watu wanapata pengine shilingi 5000, 10,000, 15,000 au 20,000. Mimi wako watu ninaowajua wanapata shilingi 5000 mtu anakaa Kengeja katika jimbo langu anaifuata shilingi 5000 Mkoani ndiko inakolipwa pencheni hii. Mhe. Spika, kutoka Kengeja hadi Mkoani anatumia shilingi 2000 kwenda na kurudi, ina maana akenda kule yeye anakwenda kufuata shilingi 3000.

Mhe. Spika, mara nyengine kama amechelewa inabidi aifuatilie Chake Chake na nauli ya kwenda na kurudi Chake Chake ni shilingi 4000 kwa hiyo kenda kufuatia shilingi 1000. Kwa hivyo, wastaafu hawa bado hawajaangaliwa na serikali kwa jicho la huruma, ningemuomba Mhe. Waziri na watumishi hawa waliitumikia serikali wakati huo na wao pencheni zao ziongezwe ili angalau waweze kumudu maisha yao ya siku kumi kama sio ya mwezi mzima. Kwa sababu wafanyakazi halisi hawamudu maisha yao kwa mwezi mzima, pamoja na hiyo asilimia 25 serikali iliyowaongezea lakini bado hawawezi kumudu maisha yao. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri na hawa awaangalie kwa jicho la huruma kwa sababu wameitumikia serikali na sasa hawana uwezo tena wa kujitafutia ajira nyengine yoyote.

Mhe. Spika, pia nizungumzie juu ya uwekaji wa kumbukumbu, mara nyingi baadhi ya watumishi unapokwenda katika sehemu zao wanazofanyia kazi

wanapotaka kumbukumbu zao huwa kwa kweli ni mtihani hazipo. Mhe. Spika, uwekaji wa kumbukumbu bado haujafikia katika cha sasa kinachohitajika. Kwa hivyo, wizara hii ina jukumu la kuhakikisha kuwa kumbukumbu za kila mfanyakazi zinakaa kulingana na hali ya sasa ilivyo. Vile vile kuna baadhi ya wafanyakazi mimi nimeitumikia serikali kwa muda mrefu kidogo, lakini nilithibitishwa kazini baada ya kutumikia zaidi ya miaka 15 na *GO* kwa siku hizo zilikuwa zinamtaka mfanyakazi athibitishwe kazini baada ya miaka 2. Lakini kwa kukosa utaratibu mzuri kuna watu wanastaafu bila ya kuthibitishwa kazini na wanapotaka mafao yao wanapata matatizo kwa sababu hawana ithibati kuwa ni kweli kuwa walikuwa watumishi wa serikali.

Mhe. Spika, kwa bahati tumeunda Tume ya Utumishi Serikalini, naipongeza serikali kwa kuweka tume hiyo. Moja katika majukumu yake ni kuhakikisha haki za wafanyakazi, kuwapandisha vyeo, kuwaondolea vizingiti na mengineyo. Kwa hivyo, ili mfanyakazi afanye kazi kwa ufanisi anahitaji kupatiwa mafunzo ndani ya kazi, anahitaji kupatiwa *course* mbali mbali. Lakini kuna baadhi ya wafanyakazi tokea mafunzo ya awali anafika kustaafu hajapata mafunzo mengine yoyote ya kujiendeleza katika kazi yake. Kwa hivyo, wafanyakazi hawa huwa wamedumaa pale pale walipo hawaendi mbele isipokuwa wanarudi nyuma. Mhe. Spika, kwa kuwa wizara hii hii ni moja katika kazi yake ningeomba kwa wafanyakazi wote kwa wakati tofauti waweze kupatiwa mafunzo na *in service training* mbali mbali kwa ajili ya kazi zao.

Mhe. Spika, nije kwenye maslahi ya wafanyakazi zaidi kwenye likizo. Mhe. Spika, kwa muda mrefu mara nyingi wafanyakazi wetu wanapokwenda likizo huwa wanakwenda likizo kavu. Sikusidii kuwa wanakwenda likizo bila ya malipo lakini ni kwamba hawapewi ile huduma ya likizo. Mfanyakazi inavyotakiwa alipwe posho la likizo yeye kama ni mwanamme alipwe mke wake na watoto wanne wapewe linalokidhi kwenda katika nchi yoyote katika nchi za Afrika ya Mashariki. Hapa kati kati mtindo wa serikali ni kuwa wanampa mtu likizo na hatimae wanatafuta shilingi 20,000 au 30,000 unaambiwa hii ndio huduma ya likizo, yeye mwenyewe kutoka Pemba kuja Unguja hizo alizopewa hazimtoshi.

Mhe. Spika, ili kuwapa wafanyakazi wetu likizo na huduma zake ningeiomba wizara hii ilifanyie utaratibu kuwa mfanyakazi anapopewa likizo apewe huduma kamili ya likizo na sio kuwa adokolewe tu pahala na wakubwa kuwa hiyo ni huduma ya likizo. Mhe. Spika, huduma ya likizo ina mpangilia wake na ina watu wa kuwachukua katika likizo.

Mhe. Spika, kwa wizara hii inahusiana na watumishi wa serikali na kuwapatia haki zao, hapo kati kati kulikuwa na wimbi kubwa la wafanyakazi

waliofukuzwa kazi kinyume na taratibu, wengi tu walifukuzwa kazi kinyume na taratibu. Kwa vile iko hii Tume ya Utumishi Serikalini nadhani ingelikuwa vyema wizara hii ikatoa wito kwa hao watu kama bado wako wakaja wakatoa maoni yao katika tume, wakajieleza na kuona kwamba kama wamefukuzwa kisheria basi, lakini kama walifukuzwa kwa ajili ya maonevu basi warejeshwe au walipwe haki zao.

Mhe. Spika, mimi nimalizie kwa kusema kuwa bajeti hii tunaipitisha na inaanza kutumika kuanzia Julai, 2011 na inamalizika Juni, 2012. Lakini hapa Mhe. Waziri hii nyongeza ndogo itaanza kutumika mwezi wa Oktoba, 2010 kwa hiyo hii Julai, Augasti na Septemba hii fedha hii itakwenda wapi kwa sababu tutakapoidhinisha tunaidhinisha kwa miezi 12. Lakini yeye anataka kuanza kulipa kwa miezi 9 hivyo hii miezi 3 ningeliomba aniambie hizi zitakwenda wapi. Mhe. Spika, kama nilivyosema kuwa leo sitaki kusema sana na hasa kwa kuwa haki yangu ya usemaji ndio hiyo iko siku nitakuomba uniongeze wakati hivyo leo naunga mkono hoja hii. Ahsante sana.

Mhe. Fatma Mbarouk Said: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia, pili nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kutayarisha hotuba hii ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Raisi Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, kwanza niende kwenye Idara ya Watawala Bora kwanza nimpongeze Mkurugenzi anayeongoza idara hii. Kwa vile idara hii ina majukumu ya kujenga na kusimamia utekelezaji na misingi ya utawala bora ikiwemo demokrasia ambayo kwa kila mmoja wetu humu tumeitumia kwa kuingia kwenye muhimili huu. Sote tuliomo humu tumeitumia demokrasia kwa kuomba kuchaguliwa na waliotuchagua pia wametumia msingi huu wa utawala bora. Mhe. Spika, mbali na demokrasia misingi mengine ni haki za binadamu, utawala wa sheria, uwajibikaji na rushwa. Haya yote Mhe. Spika, ni mambo muhimu kwa kila mmoja wetu. Mhe. Spika, kila penye ufanisi ni lazima pawe na utawala bora.

Mhe. Spika, kwa vile wenzangu wote wameshachangia kupitia nafasi mbali mbali za wizara hii pia niichangie Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwanza nataka nimpoze *CAG* mwenyewe kwa kuiongoza ofisi hii kwa mafanikio ya kiutendaji na kupunguza kwa kasi kubwa matumizi mabaya ya fedha za umma. Pia Mhe. Spika, nimpongeze kwa kutayarisha muongozo wa kazi ya ukaguzi unaozingatia viwango vya kimataifa.
Mhe. Spika, naomba sana kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 iliyofanya kuwepo kwa ofisi naomba ipatiwe haki zake kamili ndani na nje kwa kuzingatia misingi ile ile ya utawala bora. Mhe. Spika, kwa kuwa

sipendi kuchukua muda wako mwingi na vile nahisi kwamba humu nimekusanya kila kitu kwa upande wangu nasema naomba kuunga mkono hoja hii pamoja na wale walionichagua mia kwa mia. Ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii kuweza kuchangia wizara mpya inayoongozwa na Mhe. Haji Omar Kheir pamoja na Katibu wake mpya na Wakurugenzi wake wapya pamoja na watendaji wengine nawapa hongera sana.

Mhe. Spika, leo sina pongezi kubwa sana isipokuwa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima na nisisahau kumsifu sana Rais wangu Dk. Shein kwa kumchagua Mhe. Haji Omar Kheir hakutia mkono gizani amechagua vizuri sana.

Mhe. Spika, niende kwenye ukurasa wa 20 Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu. Mhe. Spika, huko nyuma kulikuwa na suala moja hapa kuhusu nyumba zile za pembezoni lakini kwa kuwa mheshimiwa alizikuta zile nyumba zimeshajengwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri hebu zile nyumba aziangalie kwa ufanisi kabisa na kama kuna uwezekano wa fungu kama lipo aweze kulinunua ili kuinusuru ile hifadhi ya nyaraka kusitoke watu wakenda kuchukua kinyume na utaratibu. Kwa sababu unajua siku hizi kuna vijana huwa wanaingia tu sehemu za watu wakenda kuiba vitu ambavyo vina umuhimu na kupoteza histria ya nyuma.

Mhe. Spika, kuhusu Tume ya Utumishi Serikalini kwa kweli hapa naomba sana nina *refrence* huko nyuma kwamba kuna kesi nyingi sana zinapelekwa kwenye tume, lakini hawazijibu watu wanapeleka malalamiko yao lakini hayatekelezwi. Mimi mwenyewe nilifuatilia barua aliyopeleka kijana wangu mpaka kufika leo namshukuru sana Dk. Mwinyihaji mwenyewe na amelisema kuwa nitalifuatilia kwa kina. Namshukuru sana Dk. Mwinyihaji kwani yule ni binadamu ana watoto, ana wazee halikadhalika na wengine wanapopeleka barua zao za malalamiko huwa hawajibiwi. Kwa hivyo, mimi naomba kwa makusudi kuwa hili suala liangaliwe tunatakiwa tuwe na tabia za kujibu barua, sio ofisi hii tu hata na ofisi nyengine zinakuwa na tabia kama hizi.

Mhe. Spika, ukija kwenye mishahara inakuwa haifutwi hiki kitu kinanishangaza mimi, kama tutafuatilia kweli yule kijana Said basi nadhani hata mshahara wake uko mpaka leo na wengine wengi tu. Mhe. Spika, namshukuru Mhe. Juma Duni amesema atalifuatilia kwani amesikitika sana, hivyo haya mambo ya tume naomba na wao wawe wepesi wanapoletea zile kesi waweze kuzimaliza au wapeleke barua kwa kesi tunaiweza au hatuiwezi.

Mhe. Spika, kitabu hiki cha Mhe. Waziri nikwambie ukweli kimenipa maajabu kitu kimoja kwani taaluma iliyotoka humu kuhusu suala la mishahara amesema ataongeza asilimia 25. Kwa hivyo, hapa mimi hata nikisema mtaalamu wangu nimtetee nashindwa kutokana na taaluma hii kwani ametuficha kabisa hajaeleza vizuri kuhusu mishahara, sijui mwenzetu ana taaluma ya aina gani. Kwa kweli wajumbe wengi kama mngeangalia hiki kitabu chake kimebana si rahisi sasa hivi kumwambia Mhe. Waziri hivi na hivi, mheshimiwa hapa huoni kitu wala hufahamu kitu. Lakini vile vile anakwambia kuwa atakuwa na tume itaangalia kwa kila siku maslahi ya wafanyakazi, mheshimiwa hongera sana kwa hili.

Mhe. Spika, mimi niseme kuwa mshahara wetu tutakwenda kupewa Oktoba hili kidogo naomba tulifikirie, pamoja na taaluma hii ulioipitisha. Mhe. Spika, Mhe. Waziri haoni hapa kama muda ni mrefu huo kwa nini tusianze kuanzia mwezi wa Julai. Mimi naona Mhe. Waziri naomba kabisa na watendaji wako wakuu hebu tuliangalie hili huko tuko masafa marefu sana. Mhe. Waziri hebu weka mwezi wa Julai uone kama kuna mheshimiwa atakayekupiga buti hapa kwani sisi tunakusikiliza wewe tu hapa na wafanyakazi huko nje wanakusikiliza wewe. Kwa hivyo, naomba ujitahidi utakapokuja hapa mimi sitaki kupiga buti unisaidie suala la kupokea mshahara mpya mwezi wa Oktoba huo utakuwa uko mbali.

Mhe. Spika, jambo la mwisho kuna wafanyakazi wale wanaolipwa kila siku wameshakuwa na miaka mingi sana hatima yao iko wapi hawa. Mhe. Spika, natoa mfano katika Idara ya Misitu wanapata kila aina inayotakiwa lakini ni *daily pay*. Mhe. Spika, kama huyo akiondoka kesho hana kitu kwani hata *ZSSF* hayupo, hana kiinua mgongo mheshimiwa mtu kama huyu tunamuweka wapi. Kwa hivyo, naomba Mhe. Waziri tumuangalie huyu katika mazingira mazuri sana ili tumfanyie mambo yake kamili kabisa ili aondokane na jina la *daily pay*. Kwa hivyo, hilo nimeliona kama nilivyosema kuwa kitabu hiki kilivyokuwa kizuri basi michango yetu inakuwa ni midogo midogo.

Mhe. Spika, watu wangu wa Jimbo la Kitope wameshanikisia jinsi ambavyo ninavyowatetea *daily pay* zao ziondoshwe na wao wawe wa kudumu katika kazi ili waweze kunufaika katika mafao yao ya kiinua mgongo mimi sina tatizo lolote. Mhe. Spika, naunga mkono asilimia mia mbili. Ahsante sana Mhe. Spika.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nikushukuruni kwa michango mizuri na kunisaidia sana kuendesha shughuli hizi, muda uliobaki ni mdogo wacha tuwaache Waheshimiwa Wajumbe mjitayarishe zaidi ili jioni tuje tuwamalize Waheshimiwa wafuatao. Kwa maana hiyo niwaombe wafike

mapema ili baada ya wajumbe hao tumuombe Mhe. Waziri atufanyie majumuisho. Waheshimiwa wenyewe ni:

1. Mhe. Raya Suleiman Hamad.
2. Mhe. Naibu Waziri na Mafunzo ya Amali.
3. Mhe. Salma Mussa Bilali.
4. Mhe. Amina Iddi Mabrouk.
5. Mhe. Salmin Awadh Salmin.
6. Mhe. Naibu Waziri wa Afya.

Kwa hivyo, naomba tujitahidi tufike mapema ili tuweze kuwasikiliza wajumbe hao waliokwishaomba na baada hapo tumuombe sana Mhe. Waziri atupe majumuisho mazuri tukamilishe kazi hii.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hayo naahirisha kikao hiki hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 6:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea naona Mhe. Fatma anachagua kiti anachokipenda. Mhe. Waziri hayupo lakini nimeambiwa atakaimu Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na sisi tuendelee na majadiliano. Kama nilivyotangulia kabla naomba sasa nimkaribishe Mhe. Raya Suleiman Hamad.

Mhe. Raya Suleiman Hamad: Ahsante Mhe. Spika, kwana namshukuru Mwenyezi Mungu na nakuomba radhi sitosimama. Namashukuru Mwenyezi Mungu Mhe. Spika, kutuwezesha tukafika hapa tukawa tuko katika hali ya uzima, nakushukuru na wewe kwa kunipa nafasi kidogo ya kuzungumza machache na mimi katika hotuba hii. Vile vile naiunga mkono hotuba nisije nikasahau kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, ukurasa wa 10 mpaka 11 ndipo nitakapoanzia kwa kuzungumza kwa jumla. Hapa tunayoyazungumza ni maslahi ya wafanyakazi wetu kwa wananchi wote kwa jumla. Nikianza nitaanza katika maslahi ya wafanyakaizi, ni vyema Mhe. Waziri alipoileta hotuba hii sote tulijua kuwa itatusaidia.

Mhe. Spika, katika maslahi ya wafanyakazi tusitizame tu maslahi ya wafanyakazi waliomo katika sekta mbali mbali serikalini hivi sasa na hata

wale wenzetu waliofanya kazi kuanzia miaka ya 1980 mpaka sasa hivi waliitumikia serikali hii kwa juhudi kubwa na uwezo wao na watu hawa walikuwa kipato chao ni kidogo sana na mpaka na mpaka kuweza kustaafu kazi.

Mhe. Spika, watu hawa wamefanya kazi mpaka wamemaliza kazi mtu ana miaka 70 na kiinua mgongo amepata shilingi milioni mbili. Je, pencheni yake itakuwa ni kama shilingi 15 elfu hiyo haijamsaidia, tunaomba maslahi haya waweze na wao kutizamwa katika bajeti hii ili kuweza kupata ufanisi zaidi na waziri na yeye akaweza kupata baraka za watu hawa waliokuwa wakitusaidia. Hata katika watu wetu wa chama cha muasisi wetu Mhe. Abeid Aman Karume watu hawa waliitumikia sana nchi hii, wamo watu wazima waliokuwa wameshamaliza muda wa kutumika hawawezi, lakini bado watu hawa wako nyuma sana kimaendeleo na hatujaweza kuwakumbuka hata kidogo. Naiomba serikali kupitia katika utawala bora watu hawa na wao waweze kuonekana.

Mhe. Spika, utawala bora na haki za binadamu, kuna kilio kikubwa katika sekta za serikali zilizomo katika muundo wake. Mhe. Spika katika sekta mbali mbali tunazopita utawakuta wanaume 20 wanawake ni watatu, pakiwa pana uamuzi mfano wa kupigiwa kura mwanamke pale hapati kitu chochote wanaume nafasi zile wanaweza kuzichukua zote. Tunaomba tupate uwiano katika sekta hizi za kufanya kazi kwenye sekta za umma na sisi tujione, hasa wanawake ndio tunaobeba majukumu makubwa katika nchi hii.

Halafu Mhe. Spika, nikiondoka hapo nije katika uwiyano katika sekta mbali mbali. Sekta nyingi ninazotembelea za wafanyakazi Unguja na Pemba siwengi watu wenye ulemavu kuwa wana ajira, watu hawa kuna watu ambao wamesoma na wana fani mbali mbali na vyetu wanavyo lakini wanaonekana kama watu hawa hawawezi kazi. Kilio chetu kikubwa na malalamiko yetu kwa wanawake, ni kwamba wanaonekana kama hawawezi kufanya kazi, kama hawawezi kutunza siri, kama hawawezi kufanya majukumu mbali mbali wanaonekana ni watu ambao wapo tu wakiwemo pamoja na makundi maalum. Kwa hivyo, tunaomba sekta itutupie macho na ituone.

Nikiondoka hapo nitakuja katika mfano tu wa utawala bora na haki za binadamu. Katika bandari yetu hii hapa ya kusafiria, chelezo inayojengwa kule wanasafiri watu mbali mbali na ni haki zetu, tusisafiri kwa sababu gani na roho zimo, japo tunasota lakini tunasafiri. Mhe. Spika, ukifika pale ni shida sana, pana idhilali ngumu wala hapana haki ya kujua huyu ni nani na huyu ni nani, kuanzia waliokuwa wazima na hata wagonjwa. Mimi nimeshafika pale Mheshimiwa naumbwa na nikashindwa na usafiri ikabidi nibebwe. Tunaomba haki za binadamu pamoja na utawala bora sehemu hizi mzione zikija hizo wizara tutazidi kuzichangia.

Mhe. Spika, Uwanja wa Ndege. Watu kama sisi ambao hatujiwezi nako pia ni mtihani vile vile, tunaomba utawala bora uweze kuona sekta mbali mbali za watu wote. Katika mafanikio haya sisi tunashukuru sana na wenzetu wataweza angalau kujikwamua kiuchumi. Mhe. Spika, hii sekta ya umma ione watu hawa wanatumika na wanamaliza siku zao hawajui wende wapi, wanatumwa, wanafanya kazi, lakini ikimaliza kazi ile pengine kitu wanachopewa ni kidogo tu.

Mhe. Spika, juzi niliona mchezo kidogo ni mfano tu ule ulitolewa. Bwana mmoja ana viwanda vingi sana wakenda watoto vijana kuomba kazi, wengine wakapasua mbao, wengine wanapiga msasa meza zilizochongwa, alipofika pale akasema nyinyi hamfanyi kazi vizuri kwa hivyo mtoke kwenye kiwanda changu. Wale watoto wakadai haki zao pale alitoa shilingi mia tano kuwalipa watoto wawili ili wagawane kila mtu shilingi mia mbili na hamsini na kazi waliyofanya ni kubwa lakini pamato yakawa ni kidogo. Sasa sekta binafsi utawala bora uone kuwa kuna watu wetu wanafanyishwa kazi lakini watu hawa hawana maslahi yoyote nguvu zao zinamaliza kule watakapomaliza hawa watakuwa hawana kitu chochote.

Nikiondoka hapo nije kwa Mdhibiti Mkuu wa Hesabu sa Serikali. Mhe. Spika, kwanza mimi namshukuru yule mama, namshukuru sana tumepata mama mahiri, kijana, anayejua kazi zake. Lakini hapa tumeambiwa kuwa tuna vijana wengi wanaofanya kazi hii, katika uchunguzi wa fedha za serikali mimi nilikuwa katika kamati yako, tunaomba kuwe na udhibiti wa hizi fedha za serikali. Tulipofika pale tuliweza kugundua, pana jina fulani bin fulani amepokea fungu la pesa pale kwa sababu amechukua mfano shilingi milioni moja au laki tano saini yake haipo, wakati mwengine unakuta pana saini jina halipo pameainishwa pesa zilizotoka tu pale, tulipodai risiti tukaambiwa risiti hapana wala kishina chake tukaona ni upotevu mkubwa sana wa pesa za serikali. Tunaomba pawe na usimamizi mzuri, pawe na mafunzo na utaalamu unaweza kupewa watu wetu ili kuweza kujua kazi zao.

Mhe. Spika, mimi sina mengi nilitaka kuunga mkono tu hili bajeti ya Mhe. Waziri. Namuombe Mwenyezi Mungu amjaalie kijana wetu, mwenetu, waziri wetu, amjaalie umahiri na Mhe. Rais amuone kwa jicho la huruma. Kwa sababu yeye ndiye aliyeyabeba mambo yote katika kitabu hiki tunakiona, mna mambo mbali mbali aliyoyabeba na yote sisi tutakuwa tunamtizama yeye basi aongezewe hata kipato chake cha fedha zizidi kuweza kutukwamua na sisi tutakaokuwa hapa. Hata sisi wawakilishi akitufanyia mafunzo Kiwengwa tuko tayari.

Mhe. Spika, baada ya hayo mimi naunga mkono baketi hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii. Kwanza kabisa sina budi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha angalau kwa muda mfupi kusimama kuichangia bajeti hii. Pia nmpongeze Mhe. Waziri kama walivyotangulia wenzangu kwa kutuletea bajeti hii yenye matumaini kabisa yeye pamoja na watendaji wake.

Mhe. Spika, pia nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar wa Awamu ya Saba Dk. Ali Mohammed Shein kwa kuona kuwa iko haja katika serikali yake hii ya Mfumo wa Umoja wa Kitaifa kurejesha tena wizara hii muhimu kutokana na umuhimu wake na kuhakikisha kwamba wizara na idara zake zinatekeleza majukumu yake ipasavyo.

Mhe. Spika, nianze na ukurasa wa saba katika Idara ya Uendeshaji. Katika idara hii kuna suala la ajira hapa, Mhe. Spika, wizara kupitia idara hii ina jukumu la kuhakikisha kwamba sekta zote za serikali zina watendaji sahihi, watendaji hao watapatikanaje? Kwa muda mrefu katika baadhi ya sekta kuna mapungufu ya wataalamu mbali mbali, hivyo tunatakiwa kuwa na mipango maalum ya wahitaji au watumishi ambapo mipango hiyo imo katika kitabu hiki kwenye sekta husika ili waweze kutoa huduma sahihi na kwa wakati unaofaa.

Mhe. Spika, mengi yameshazungumzwa lakini na mimi nitazungumza kidogo kidogo ili kuendana na muda. Ili tuweze kuwa na ufanisi katika sehemu zetu za kazi ni lazima Mhe. Waziri aweke kipaumbele katika sehemu zetu za kazi kwa wafanyakazi kimasomo, lakini wafanyakazi hao anatakiwa awaendeleze katika ile fani ambayo mfanyakazi anayo. Hili litawezekana endapo sera ya mafunzo itaandaliwa katika kulisimamia zoezi la tathmini ya mafunzo ili kuibua mahitaji na mapungufu ya mafunzo au mahitaji ya wataalamu waliokuwepo.

Pia nathubutu kusema kwamba, Mhe. Waziri kama mpango huu atausimamia ipasavyo mafanikio makubwa yatapatikana. Mpango wenyewe ni mpango wa urithishaji, kwa sababu kuna baadhi ya sehemu Mhe. Spika, kuna baadhi ya wafanyakazi wakistaafu ile nafasi ambayo alikuwa anayo inashindwa mtu mwengine wa kuifanyia kazi, ama inaonekana kwamba akistaafu huyu hakuna mwengine ambaye ataweza kuiendeleza ile sekta na hii si kwa viongozi tu, bali hata kwa wafanyakazi wadogo.

Katika ziara zetu za kamati hili tumelikuta Karakana, tumekwenda kule tumeoneshwa mashine ambayo ipo pale inafanyakazi, nzima, lakini mashine ile aliyekuwa anaiendesha amefariki na hivyo mashine ile kwa muda ule

maisha yake imebidi yasite kwa sababu hakuna mtu mwengine ambaye anaiweza. Kuna baadhi ya wafanyakazi ambao wako likizo wakiondoka basi wanaondoka na ujuzi wao baadhi ya mashine zinashindwa kufanya kazi, lakini sasa mfanyakazi kama yule mwenye ujuzi kama atakuwa ana watu sita huku nyuma amewafundisha basi hata kama atakwenda likizo kazi zitaendelea kikawaida. Kama yule mtu aliyefariki ndio imekuwa mashine haifanyi kazi na mwengine yuko likizo na hakufanyiki kazi kwa sababu watumishi hao hawapo.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri suala hili la *succession planning* Mhe. Waziri naomba aliendeleze isiwe limo katika hiki kitabu tu, hili alisimamie ili tuweze kuwa na urithi mzuri wa wafanyakazi wa kuendeleza kazi ambazo zimekusudiwa.

Katika bajeti hii Mhe. Waziri amesema kuna wafanyakazi tayari wamepangiwa kustaafu kwa kipindi hiki. Lakini wafanyakazi hao inawezekana katikayao mia tano na kitu nusu ya hao wakaja wakarejeshwa tena kwa mkataba kwa sababu mbali mbali. Sasa kama mpango huu utakwenda vizuri ina maana wakishastaafishwa wale tutapata nguvu kazi ya vijana wengine kuwaajiri katika sekta zile na tutapunguza hili tatizo la ajira katiak sekta mbali mbali. Lakini huu utaratibu wa kwamba kila wanaostaafishwa wanapewa mkataba miaka miwili miwili vijana wetu na tatizo hili litaendelea kuwepo na itakwua ni usumbufu.

Mhe. Spika, kama nilivyosema kuwa masuala mengi yameshazungumzwa kwa hivyo, nitakuwa sina mengi sana na mwisho nimalizie na suala la wafanyakazi hewa. Mhe. Spika, zoezi hili lilifanywa kipindi cha nyuma kwa mafanikio makubwa na walijulikana wafanyakazi hewa ambao walikuwa wamekufa bado pesa zao zinalipwa, walipata wafanyakazi hao ambao wamehama nchi lakini bado fedha zao zinalipwa na tukapata mafanikio makubwa na pesa zile zikasaidia katika ujenzi wa nchi yetu. Sisemi kwamba bado wangalipo, lakini ninaomba Mhe. Waziri suala hili bado aliendeleze kwa sababu fedha zile au zile nafasi ambazo tunafikiria bado zipo kwa wale wafanyakazi ambao wanalipwa zitajulikana na tutapata kuajiri vijana wengine wenye sifa na ambao wanakosa haki zao za kimsingi za ajira kutokana na kusema kuwa tunao wafanyakazi na wafanyakazi wenyewe ni hewa na zile fedha zitatumika kwa mambo ya maendeleo mbali mbali ya nchi yetu.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya wanawake wenzangu wa Mkoa wa Kusini naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia pumzi za kuweza kusimama

hapa mbele ya Baraza lako tukufu nikiwa mzima na afya njema. Lakini pia nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa nikushukuru wewe Mhe. Spika, kwa kuweza kunipatia nafasi hii jioni ya leo na mimi niwe mmoja wapo kwa kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, pia nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake wote kwa kukaa chini na kuandaa hotuba hii ambayo ina lengo la kuwasaidia wafanyakazi kwa ujumla.

Mhe. Spika, nianze basi kwa kuingia moja kwa moja katika ikitabu chetu hiki nije katika ukurasa wa 20 kwenye Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu ya Taifa. Mimi nipongeze kwa dhati kabisa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwanza kwa kujua umuhimu wa uwekaji wa nyaraka na utunzaji wa nyaraka. Bila ya utunzaji na uwekaji mzuri wa nyaraka basi hata serikali inaweza kuyumba katika ufanyaji wake wa kazi. Kwa hivyo, nichukue nafasi hii kuipongeza serikali kwa kuona upo umuhimu wa kuweka idara hii.

Mhe. Spika, labda niende moja kwa moja katika lile jengo ambalo lipo pale Kilimani jengo ambalo ndilo lenye utunzaji wa nyaraka zetu. Mhe. Spika, jengo lile kwa kweli pahala pake palikuwa pazuri sana na hapo zamani sisi tulipokuwa wadogo katika eneo lile ilikuwa kupita kule nyuma tunaogopa kwa jinsi ya lile jengo lilivyokuwa limetulia, hakuna majengo, hakujavamiwa na nyumba ovyo, lakini Mhe. Spika, kinyuma na hayo sasa hivi basi ukipita sasa roho inaweza ikakuuma Mhe. Spika. Kwa sababu nyaraka zote za serikali siri na nyengine za dhahiri, lakini kwa sasa hivi lile eneo lipo pahala ambapo hapana usalama wa nyaraka zetu.

Mhe. Spika, labda nimuombe Mhe. Waziri ajitahidi sana kama itawezekana ajaribu kulipa nyumba ambazo watu wanaishi pale awalipe ili tuweze kupata nafasi ile tuweze kulizungusha liwe na usalama zaidi.

Pia basi pale katika jengo lile kuna kompyuta moja tu, sasa Mhe. Spika, kompyuta moja itafanya kazi vipi katika hali ya udhibiti wa nyaraka zetu za serikali. Sasa hili Mhe. Spika, pia nimuombe Mhe. Waziri ajaribu kutafuta kompyuta za kutosha ili tuwe na kumbukumbu za kutosha. Kwa sababu karatasi zinaweza kuchangia wakati wowote, mtu anaweza kuichukua kaificha, lakini tunapopewa data tukaziweka kwenye kompyuta Mhe. Spika, data ile haitoki bado inakuwa *in saved hand*. Kwa hivyo, Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako ajitahidi atafute kompyuta za kutosha katika idara ile.

Lakini pia pana tatizo la elimu kwa wafanyakazi katika idara ile. Zamani ilikuwa utunzaji wa nyaraka tunaona kama si kitengo muhimu, pengine mtu ambaye hajasoma sana ndiye anayewekwa kwenye kutunza nyaraka. Kwa

hivyo, namuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana wafanyakazi wetu wale tuwapatie elimu ya kutosha ili waweze kuzitunza nyaraka zetu zile kwa matuzo mazuri na matunzo ya kisasa.

Nikiendelea na mchango wangu nije katika Chuo cha Utawala ukurasa wa 28. Mimi niipongeze serikali kwa dhati kabisa kwa kujenga Chuo Kikuu kipya Tunguu. Chuo kile lengo lake kuu ni kuwaendeleza wafanyakazi wetu wa serikali, lakini kwa sasa hivi haiko hivyo, ukienda Tunguu katika kile chuo chetu utakuta wanafunzi wengi wako nje ya serikali, wafanyakazi wetu wako wachache sana kama asilimia basi unaweza kusema ni asilimia 60 wanaosoma pale ni wanafunzi kutoka nje.

Mhe. Spika, wanafunzi kutoka nje si tatizo kwa sababu ni wanafunzi wetu wa Tanzania, Wazanzibari, lakini lengo kuu la chuo kile ni kuwapatia elimu ili kuwaendeleza wafanyakazi wetu. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ajitahidi sana kuhamasisha wafanyakazi wetu wajiendeleze.
Mhe. Spika, chuo kile pia hakina vyombo vya kisasa vya kufundishia. Jengo lile ni la kisasa limejengwa zuri, lakini ukiingia ndani unakuta bado chuo kile hakina vyombo vya kisasa. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri na hili pia ahakikishe kwamba chuo chetu kile kizuri, jengo lake zuri lakini pia kiwe na vyombo vya kisasa vya kufundishia wanafunzi wetu.

Nikiendelea na mchango wangu nije kwenye ukurasa wa 84 kwenye maslahi ya wafanyakazi. Mimi nipongeze kwa dhati kabisa serikali yetu, nichukue nafasi hii kwa dhati kabisa kumpongeza rais wetu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuwafikiria wafanyakazi na kuwaongeza mishahara katika asilimia 25. Mhe. Spika, nyongeza ile kwa kweli inawapa moyo sana wafanyakazi wetu na kila unapopita basi gumzo Mhe. Rais wetu. Kwa hivyo, nachukua nafasi hii kupitia kwako Mhe. Spika, nimuombe Mhe. Rais wetu wa Zanzibar kila anapopata nafasi ya kuongeza nyongeza za mishahara kwa wafanyakazi basi atutupie jicho la huruma wafanyakazi wetu wale.

Mhe. Spika, nije katika ukurasa wa 27, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mimi nachukua nafasi hii kumpongeza Mdhibiti wetu Mkuu wa Serikali mama yetu mwanamke. Unajua Mhe. Spika, kila anapopata nafasi mwanamke mwenzetu lakini tukamuona nafasi ile anaifanya kwa uadilifu, anaifanya kwa upendo basi kwa kweli sisi kinamama huwa tunafurahika lakini pia sisi kinamama tunamuunga mkono, lakini hatumuungi mkono yeye tu, tunawaunga mkono wanawake wote ambao wameshika nafasi mbali mbali katika serikali hii na tunawaambia wajitahidi wafanye kazi vizuri na sisi tuko nyuma yao na pia wasituangushe.

Mhe. Spika, nikiendelea na mchango wangu nije katika wafanyakazi. Kuna tatizo ambalo lipo sasa hivi kubwa tu, kuna vijana wengi hapa Zanzibar wamesoma welimu mpaka ya juu, lakini vijana wale unakuta hawana kazi wanazurura ovyo. Hii inatokana na kwamba serikalini ajira zimekuwa hamna, sasa pengine inatokana na nini? Mhe. Spika, kuna wale ambao wazee wameshakuwa tayari kustaafu, lakini watendaji wale hatimaye wanaongezwa muda, lakini pia tuna tatizo labda pengine serikali tumejisahau, serikali inajua kwamba baada ya miaka miwili mfanyakazi huyu atastaafu hatumuweki kijana ambaye ashike ile nafasi kupata uzoefu na hatimaye nafasi ile inakuwa haina mtu na inapelekea mfanyakazi yule anaongezewa muda kutokana na kwamba hakuna mtu wa kushika nafasi ile.

Mhe. Spika, kweli wazee tunawahitaji tunahitaji watupe uzoefu, lakini pia ni kweli kuna sehemu nyengine za kazi ni nyeti ambazo zinahitaji wale wazoefu ili kutupa uzoefu. Kwa hivyo, Mhel Spika, labda nimuombe Mhe. Waziri kupitia kwako hili suala la wafanyakazi ambao wanafikia umri wa kustaafu basi wastaafishwe. Mhe. Spika, nje kuna vijana wengi tena wenye elimu ya kutosha, vijana wale hatimaye wanaweza kuingia kwenye madawa ya kulevya, vijana wale ndio ambao utawakuta wanakaa vijiweni tu wanapiga stori na hatimaye inawapelekea kufanya mambo ambayo hayapo katika maadili yetu.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu hautokuwa mkubwa kwa hivyo nimalizie kwa kusema kwamba naunga mkono hoja hii mia juu ya mia.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia siku hii ya leo hapa kukutana katika Baraza lake tukufu kwa madhumuni ya kujadili hotuba hii muhimu ya Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, nimpongeze sana Mhe. Waziri, Katibu Mkuu na Wakurugenzi wote, pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kutuandalia mpango huu wa mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Lakini pia nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Ali Mohamed Shein kwa kutekeleza ahadi zake ambazo alikuwa akizisema wakati ule wa kampeni.

Katika mikutano yake ya kampeni Mhe. Rais aliahidi kwamba ataimarisha mazingira bora ya kazi na maslahi ya watumishi wa umma. Lakini pia akasema kwamba ataanzisha wizara maalum ambayo itahusika na suala zima la kushughulikia utumishi wa umma. Kwa hivyo, nimpongeze Mhe. Rais kwa kutekeleza ahadi hiyo na kwa sababu sasa hivi tumeshuhudia mipango

ya serikali katika kuyafanya mazingira bora ya kazi na maslahi ya watumishi wa umma. Lakini pia ile wizara ambayo ametuahidi tayari ameiunda.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu unaweza ukafanana na michango ya wajumbe wengine lakini kwa misemo tofauti. Kwa hivyo, naomba univumilie kidogo na kwa sababu Waswahili wamesema "Papo kwa papo kamba hukata jiwe". Sasa kila tukisugua sugua pale mambo yatakwenda vizuri.

Mhe. Spika, nianze kuhusu maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametueleza hapa katika kitabu chake kwamba wafanyakazi hawa wa kima cha chini wamepandishiwa mshahara wao kwa asilimia 25. Mhe. Spika, niipongeze serikali kwa hatua hii ya kuongeza asilimia 25 katika kima cha chini. Lakini pia ametueleza kwamba atakuwa anaangalia zaidi *scheme of service.*

Sasa Mhe. Spika, mimi nije hapa katika suala zima la *scheme of service* ambapo Mhe. Waziri ametueleza katika kitabu chake naomba nimnukuu anasema kwamba "Ili kutekeleza ahadi ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na kutatua matatizo yaliyotajwa hapo awali ya kuzuia wataalam kuacha kufanya kazi katika utumishi wa umma, serikali imepitia upya miundo ya utumishi serikalini."

Hapa Mhe. Spika, ndipo ambapo nataka kuzungumzia. Mhe. Spika, Mhe. Waziri ametoa *statement* hii nzuri lakini kama alivyotangulia Mhe. Makame Mshimba Mbarouk asubuhi alipokuwa akichangia kwamba Mhe. Waziri ametubana sana ametuweka kona. Kwa sababu ametoa maelezo tu lakini hakutoa ufafanuzi wa kutosha kujua namna gani ameweza kuboresha maslahi haya ya hizi *scheme of service* hasa katika baadhi ya maeneo.

Kwa mfano Mhe. Spika, kumekuwa na kilio sana cha wataalam wetu hawa madaktari jinsi wanavyotukimbia na kufuata maslahi zaidi. Mhe. Spika, pia umeshuhudia wawakilishi wako wamekuwa wakiwazungumzia sana hawa. Kwa sababu pamoja na kwamba watumishi wote ni muhimu lakini madaktari ni muhimu zaidi na sote hapa tunahitaji kuangaliwa afya zetu na siku hizi maradhi yamekuwa mengi. Kwa hivyo, madaktari kuja kusomeshwa na kuondoka kwa kweli inakuwa haipendezi na afya zetu zinakuwa hatarini. Kwa hivyo, ningemuomba sana Mhe. Waziri hebu atuelezee kwa muhtasari hasa hawa madaktari katika bajeti yake hii amewaangalia vipi.

Mhe. Spika, pamoja na kwamba hatuwezi kujifananisha sana na wenzetu Tanzania Bara kulingana na uchumi wao, lakini madaktari wa Bara kwa mwezi wanalipwa shilingi 889,000. Sasa tukiwaangalia madaktari wetu hapa

wanalipwa kwenye shilingi laki tatu na kidogo kwa hivyo utakuta ni tofauti kubwa sana.

Leo Mhe. Spika, kuna madaktari wanaitwa *internship* ambao wanapata majaribio yao katika hospitali mbali mbali. Wanashindwa kuja katika hospitali ya Mnazi Mmoja kufanya majaribio hayo kwa sababu wale walimu wao tayari viwango vyao vya mishahara ni vidogo kuliko hao wanafunzi.

Kwa sababu Tanzania Bara madaktari wa aina hiyo wanalipwa shilingi laki saba. Sasa kwa kweli Mhe. Spika, pana tofauti kubwa kati ya wenzetu wa Bara na wetu wa huku. Mhe. Spika, ningependa Mhe. Waziri atakapokuja hapa kwa muhtasari tu hebu atueleze jinsi bajeti hii ilivyowaangalia madaktari ili turidhike tumpitishie bajeti yake hii bila matatizo.

Mhe. Spika, jengine Mhe. Waziri ametuelezea juu ya hatua mbali mbali ambazo zinachukuliwa katika kufanyia mapitio ya maposho mbali mbali, nayo katubana bana hakutupa uwazi maposho haya yatakuwaje.

Kwa mfano Mhe. Spika, katika jimbo langu la Magomeni kuna vizee pale ambavyo tumeviweka katika nyumba za wazee Sebleni, wazee wale sasa hivi wanalipwa shilingi 25,000 kwa mwezi kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao yote. Kiwango hichi ni kidogo mno pamoja na hali yetu ngumu, lakini ni kiwango kidogo kwa mtu kumuweka pale na kumlipa ili aweze kukidhi mahitaji yake. Sasa wazee wale nao wanahitaji kuangaliwa. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuelezee wazee wale wa nyumba za wazee Sebleni ambao tumewaweka pale bajeti hii itawaangalia vipi kutokana na kiwango walicho sasa. Pia mmewapangia vipi katika bajeti hii ili tuweze kupitisha bajeti.

Lakini pamoja na hayo kuna wale wazee waliostaafu ambao wenzangu hapa wamewazungumzia na wao wanahitaji kuangaliwa kwa umakini sana. Viwango vyao vya viinua mgongo ni vidogo mno pamoja na pencheni ambavyo vinahitaji kuangaliwa ili viendane na wakati. Kwa sababu wazee hawa wametumikia sana nchi hii, michango yao ilikuwa mikubwa, kwa hivyo na wao wanahitaji kuboreshewa maslahi yao ili na wao waende na wakati. Kwa sababu pamoja na kwamba wamestaafu lakini bado wanahitaji kuishi.

Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atupe kidogo kwa muhtasari tu tumewaangalia vipi hawa wazee wetu waliostaafu viinua mgongo vyao na pencheni zao ambazo wanazipata.

Mhe. Spika, jengine suala la wafanyakazi wa serikali kupokelea mishahara benki. Mhe. Spika, niipongeze sana serikali juu ya suala hili ambalo

wamejaribu kufanya utaratibu ili watumishi wa umma waweze kuchukulia fedha zao benki. Ni utaratibu mzuri na kwa sababu utaratibu huu unaweza kusaidia kuondosha hawa wafanyakazi hewa ambao mwenzangu hapa amezungumza.

Lakini Mhe. Spika, kumekuwa na tatizo kwa wenzetu wa benki wanasema wakati mwengine wanapopelekewa zile *payroll* kwa ajili ya malipo kunakuwa na tofauti ama namba ya akaunti ya mtumishi au jina limebadilika jambo ambalo linawapa usumbufu wafanyakazi wa serikali. Anapokwenda benki kuchukua fedha anakuta pale akaunti yake pengine imepelekwa namba sio, namba moja imebadilika au jina moja limebadilika, maana yake sasa inabidi arudi aanze upya. Kwa hivyo, hili linatokana na hii Idara ya Mipango na Rasilimali Watu nadhani na kama sivyo basi Mhe. Waziri atanieleza wapi ambapo kitengo kinachohusika na mipango hii.

Mhe. Spika, kwa kweli eneo hili linahitaji kuangaliwa na linahitaji uangalifu wa hali ya juu. Mhe. Spika, inasikitisha kuona mfanyakazi anakwenda benki ameshamwambia mama watoto weka maji jikoni nakwenda benki kuchukua pesa nitakuja na sembe, matokeo yake kule anaambiwa pesa hazijaingia kwa sababu kwenye orodha ile ambayo imepelekwa kule ina hitilafu. Kwa hivyo, hapa panahitaji kuangaliwa kwa makini, watumishi wetu wanaoandaa zile payroll zinazopelekwa benki kwa ajili ya kulipwa mishahara wanatakiwa wawe na uangalifu wa hali ya juu ili kuondosha tatizo hili.

Mhe. Spika, jengine la mwisho ni suala la Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Spika, afisi hii imepewa pongezi nyingi sana na Waheshimiwa Wajumbe na inaonekana inafanya kazi vizuri. Kwa hivyo, nichukue nafasi hii niipongeze afisi hii.

Lakini moja ambalo Mhe. Waziri ametueleza hapa katika kitabu chake kwamba kumekuwa na mafanikio. Ripoti ya mwaka 2008/2009 imeonesha mafanikio kwa kiasi fulani katika jinsi ya fedha hizi za umma zinavyotumika. Sasa kwa kweli sisi tumeona kuna *quiry* nyingi sana, kumekuwa na matatizo mengi sana ya fedha za umma, lakini kama ni mafanikio pengine inaweza kuwa kuna mafanikio zaidi kuliko nyuma. Kwa hivyo Mhe. Spika, Mhe. Waziri anahitaji kukaza kamba ikazike ili kuona kwamba matatizo yanayojitokeza katika taasisi hizi za serikali katika kufuata zile taratibu za kifedha zinachukuliwa.

Kwa sababu tutakuwa tunatwanga maji katika kinu, kila siku wataalam wanakwenda katika maofisi, kamati zetu zinakwenda, ripoti zinakuja, lakini hakuna hatua zozote zinazochukuliwa baada ya ripoti zile kuwasilishwa. Mhe. Spika, ningependa Mhe. Waziri afanye kila linalowezekana kuona

kwamba hili jambo linakoma kabisa, ripoti zinazokuja hapa basi zioneshe mafanikio zaidi kuliko hizi taarifa tulizozipata.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naunga mkono hoja ya Mhe. Waziri na nimuombe yale maeneo ambayo nimemuomba atupatie maelezo angalau kwa muhtasari wakati atakapofanya majumuisho, basi apite kwa muhtasari tu ili tuweze kujua nini kinachoendelea. Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Spika, mchango wangu kwa siku ya leo si mkubwa na mimi nakwenda hapa hapa kwenye kidonda.

Mhe. Spika, nizungumzie maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Spika, nashukuru kilio cha muda mrefu cha wafanyakazi kimesikilizwa na naipongeza serikali pamoja na wizara kwa juhudi walizozifanya.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri katika kitabu chake ametuainishia kwamba maslahi ya mfanyakazi wa kima cha chini ni asilimia 25, hichi ni kiwango kidogo sana. Lakini la kusikitisha zaidi ni kwamba naichangia bajeti hii na hapa ndipo walipoongezwa katika kima hichi lakini bado wanaambiwa kitatumika mwezi wa 10.

Mhe. Spika, jambo hili halitufurahishi kwa sababu bajeti hii ndio iliyowapangia na leo hii pana miezi mitatu hapa imeruka hatujui kuna nini. Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuweke sawa.

Mhe. Spika, pia naipongeza tena serikali pamoja na wizara husika kwa kuongeza viwango vya mishahara ya wafanyakazi kwa kutumia vigezo, sifa, uzoefu na elimu yao. Jambo hili linaweza likatusaidia katika ile dhana ya wafanyakazi wetu kukimbia na kwenda nchi mbali mbali kutafuta ajira kwa maslahi yao. Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri hili alichukue na kama tunavyofahamu mwanzo mgumu, lakini baadae wapate tija zenye maslahi. Bila ya kufanya hivyo basi bado tutakuwa na ile kadhia kila siku wasomi wetu kwenda kutumikia taifa jengine ambapo taifa la Wazanzibari halifaidiki. Mhe. Spika, tunaomba wafanyakazi hawa pamoja na maslahi madogo yaliyopo ya nyongeza lakini iwe endelevu isiwe ni mwisho hapa.

Mhe. Spika, kwa kuzingatia muda kwa haya machache nasema ahsante sana nakushukuru.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii tena ili kuweza na mimi kushiriki katika kuchangia hotuba ya Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, kwanza nikupongeze wewe binafsi kwa kuweza kutujali katika uchaguzi wako na kutupa nafasi na hasa nahisi kwamba anapokuwa anasimama mwanamke mara nyingi unampa nafasi. Kwa hiyo, naona kama kidogo unatujali, lakini wenzetu katika utendaji wa kazi hawatujali kama unavyotujali wewe.

Mhe. Spika, napenda nimpongeze Mhe. Rais kwa kutimiza ahadi zake alizozitoa kwenye kampeni, katika ilani ya uchaguzi na katika hotuba aliyoitoa wakati wa uzinduzi wa awamu ya nane ya Baraza la Wawakilishi. Mhe. Spika, Mhe. Rais aliahidi kuimarisha mazingira bora ya kazi na maslahi ya watumishi wa umma ili waweze kutoa huduma bora kwa wananchi. Tunamshukuru ametimiza ahadi yake hiyo.

Mhe. Spika, pia napenda nimpongeze Mhe. Waziri wa Wizara hii pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri waliyoifanya. Mhe. Spika, kabla sijaanza na mchango wangu naunga mkono hotuba hii mia kwa mia.

Mhe. Spika, mimi ni mwanagenzi katika kuendesha wizara, lakini kuna mambo ambayo nimeyabaini nahisi kwamba labda Mhe. Waziri atusaidie ili tuweze kufanya kazi vizuri. Katika wizara wafanyakazi wanasoma, kuna wale wanaoajiriwa wapya ndio kwanza wamesoma na kuna wale walioko kwenye kazi halafu wanakwenda kupewa mafunzo ya kuongeza ujuzi. Mimi sielewi kama kuna mwongozo au hakuna, kama upo mwongozo sifahamu. Lakini ninachokiona kwamba mwanafunzi kaingia chuoni kamaliza kusoma hajaanza kazi kaajiriwa kapewa mshahara baada ya siku mbili kaondoka kenda kusoma. Unaweza ukakuta mtu yule ana miaka 10 anasoma na kusoma kazi hajafanya na mshahara analipwa. Kigezo kiko wapi mimi sielewi.

Lakini si hivyo tu, kuna wale wanaosoma mtu katoka *degree* ya kwanza kaenda kusoma miaka mitatu *degree* ya pili, akirudi pale anaongezwa shilingi 3,000. Kwa miaka mitatu mizima ya kuongeza *degree* ya kwanza mpaka ya pili shilingi 3,00o kweli aliyemuacha huku hakusoma akirudi ameshapata *increment* hata ya zaidi ya shilingi 10,000. Kwa hiyo, mimi naona hapo kidogo kama haki haitendeki.

Mhe. Spika, sasa hivi kuna utaratibu tunafikiri labda wafanyakazi wakipokelea mshahara benki kwa kiasi fulani tutapunguza wafanyakazi hewa. Inawezekana ni hivyo, lakini ninaloliona mimi kuna wengine wanapeleka pesa benki wanaondoka kazini hawajulikani walipo miaka na miaka pesa zinakwenda benki. Kwa hiyo, tuangalie utaratibu huu tunapolifanya hilo ili tuwe tunalifuatilia vizuri tusipoteze tu pesa benki halafu tena wengine hawazifanyii kazi na wanapokea.

Mhe. Spika, pia kitu kimoja ambacho mimi nahisi kwamba labda kingekuwepo kingetusaidia kuwe na *pay in slip*. Mhe. Spika, ninavyojua wizara zote lazima ziwe na *pay in slip* lakini utaratibu huo mimi siuoni, ukiitaka mpaka uende sehemu ya hesabu ukaiombe pale unapotakiwa. Kwa nini kusiwe na *pay in slip* kila mtu akapata yake mwisho wa mwezi unapofika. Nafikiri huo ni utaratibu mzuri kila mtu atajua kama kapunguziwa au kakatwa na kakatwa kwa nini kitajionesha pale.

Mhe. Spika, kitu chengine ambacho sikukiona na ningependa nipewe mwongozo. Hivi katika mawizara huwa hakuna *projection* maalum hasa kuhusu wafanyakazi, mimi nafikiri kungekuwa na utaratibu tukawa na *projection.* Wizara kubwa kama ya Afya tukiomba wafanyakazi waajiriwe tunaambiwa kila siku mnaajiriwa nyinyi tu mmejaa tele, lakini ukija ukitutazama unakuta tuna mapengo tele. Kama kungekuwa kuna *projection* tukajua kwamba katika wizara yetu kazi tulizonazo ni hizi, nafasi ndio hizi, kwa kipindi cha miaka mitano hawa wanaingia, hawa wanastaafu, nafikiri hilo lingekuwa jambo la maana tungekuwa tunajua wapi tunakokwenda.

Lakini jengine Mhe. Spika, kuna utaratibu ambao mimi siuelewi. Mhe. Spika, maisha yetu yanakwenda kwa *shift*, mtu anakwenda kumuaga bosi wake bado siku tatu mimi kesho nasafiri nakwenda kusoma. Utakwendaje kusoma wakati mimi sina taarifa, ulipoomba hukuniaga, umepata vipi sijui, leo unaondoka mtu yule aifanye kazi vipi, nafasi yake mtu yule aijaze vipi. Kwa hiyo, inaonekana kwamba huku kwenye mawizara yetu hakuna utaratibu maalum nani anayeondoka, anaondoka vipi, kwa kipindi gani, hicho hakipo. Kwa hiyo, mimi nafikiri tupewe miongozo ili tuifuate turekebishe hilo.

Mhe. Spika, pia tutajitahidi tutawasimamia watendaji wetu kwa kazi baada ya marekebisho ya mishahara hasa na hiyo *value for money* japo kidogo ionekane, isiwe *value for money* kwa majengo tu na manunuzi na hata katika kazi. Hicho kidogo tunachopewa basi tuoneshe *appreciation* kwa kile kilichoongezwa angalau kile tunachopewa tukifanyie kazi ionekane maana hilo sidhani kama lipo la kutosha.

Mhe. Spika, jengine ambalo nimeliona kwa kipindi kifupi si kila mfanyakazi anajua *government order* inasemaje unakuja kuiona siku ya kuadhibiwa imesema hivi, imesema vile. Mimi nafikiri wafanyakazi wapewe nafasi wafundishwe kila mtu ajue kwamba *GO* iko hivi, ukifanya hivi ni kosa, ukifanya hivi si kosa, ukifanya hivi umepunguziwa haki yako na ukadai lakini si mara nyingi hilo linatendeka.

Mhe. Spika, jengine ni malalamiko. Katika wizara yetu mara nyingi wateja wetu wanatulalamikia ukenda Wizara ya Afya kuna hivi, kuna vile, lakini na sisi wanatufanyia mambo hatuna kwa kwenda kulalamika. Wanafanyakazi wanapigwa pale mlangoni, wanapigwa vibao huko juu, wanatikiswa, mtu atataka kuingia hasa, ukimwambia mimi sie atakutikisa atakwambia hunijui mimi nani, mimi mkubwa. Mhe. Spika, nafikiri kuwe na kitengo cha wanaolalamikiwa na walalamikaji ili sote twende tukalalamike. Sisi tukitendewa mabaya tupate pa kulalamika jamani nyinyi tumepigwa atafutwe aliyepiga na haki itendeke.

Mhe. Spika, limezungumzwa suala la nyaraka, nakubaliana na Mhe. Mjumbe aliyesema kwamba kule kitengo waliokuwa wanapewa ni wale walioonekana hawana elimu kwa sababu walihisi kwamba hakina thamani. Hakujulikani nyaraka ya siri kule wala ya dhahiri, yote tu ni mtiririko usioeleweka. Kwa hiyo, mimi nafikiri wasomeshwe wenye uwezo na wale wakaelimishwe waliopo kwenye mafunzo wote wapewe mafunzo. Hawaelewi wanachokitenda tuwasaidie ili wafanye kazi vizuri kwa sababu tulichagua watu tukawapa dhamana bila ya kuwaelimisha.

Mhe. Spika, pamezungumzwa Makumbusho. Mhe. Spika, makumbusho tu si historia, ukenda nchi zilizoendelea makumbusho ni kitega uchumi na chanzo kizuri cha mapato kwa watalii. Mhe. Spika, makumbusho yetu yametupwa, ukenda pale majani yameota mpaka yanataka kuingia kwa madirishani. Mimi nafikiri tuyarudishe katika hali nzuri ili tupate kipato. Achilia mbali hiyo historia tunayoitafuta na watoto wetu baadae kuja kuona kilichotendeka nchini kwetu.

Mhe. Spika, nataka nizungumzie maslahi ya wafanyakazi. Mhe. Spika, tunapozungumza maslahi ya wafanyakazi si mishahara tu. Kwa mfano Wizara ya Afya call allowance na overtime kwa watu ambao wanafanya kazi pengine unamkuta mtu anafanya kazi masaa 64 badala ya masaa manane na nusu. Nafikiri hayo ni maslahi, pale ambapo wafanyakazi pana upungufu watu wako tayari kufanya kazi masaa mengi lakini basi walipwe. Maana mtu wa kawaida anafanya kazi masaa manane na nusu tu kwa siku, mtu anaingia shift labda wiki tatu, usiku na mchana kwa mshahara ule ule hatumpi overtime hatumpi on call allowance. Nafikiri kwa maslahi hilo wafanyakazi wetu wa afya watazamwe.

Tukija likizo kila kituo nilichokwenda Unguja na Pemba iwe wodi iwe kituo cha afya. Jamani wafanyakazi wa afya kitu likizo na pesa ya likizo hawajawahi kukiona. Mimi nimefanya kazi pale tangu mwaka 1979 nimeondoka mwaka 2006 sikuwahi kupata pesa ya likizo hata shilingi. Sasa sijui wanaopewa wanapewa kwa msingi upi labda kwa kuwa sisi hatuzalishi tunatoa huduma, lakini nafikiri ni haki yetu kupewa likizo.

Kwa hiyo, naomba marekebisho yatakayofanywa msitupe arrears lakini tuanze kupewa pesa za likizo tena zinazolingana, msikae mkafikiria kwamba anataka chukua shilingi 10,000 mpe, elfu kumi sio pesa ya likizo tupewe kulingana na mishahara yetu.

Mhe. Spika, jengine uniform kwa wafanyakazi wa afya ni haki yao ya msingi. Hatuwezi kuwa-control watu kuwaambia vaeni uniform, hatuwezi kuwaambia vaeni hivi kwa sababu kifungu cha uniform hakipo. Kwa mfanyakazi wa afya uniform ni haki yake. Polisi wanapewa, JKU wanapewa, afya kwa nini hakuna kifungu ambacho kiko maalum kwa ajili ya uniform. Mtu atavaa mtandio unamning'inia hospitali pale maradhi chungu nzima anakaa anavyotaka, yule kavaa dira, halafu unaiita ile uniform. Kama tutawapa kweli pesa zinazostahiki ukawaambia kwamba sasa shona mshono wetu ndio huu, unataka kufanya kazi hospitali huu ndio mshono, madhali unampa utam-control, lakini kama humpi atavaa anavyotaka atashona anavyotaka. Kwa sababu pesa anaitoa kwenye huo mshahara wake mdogo kwa hiyo inakuwa ngumu.

Mhe. Spika, kitu chengine ambacho nilikuwa naomba pale tunapochagua watu kwenda nje wataalam tuwahusishe kwa karibu. Wataalam kama kuna mtu wa malaria mnakwenda kwenye malaria waoneeni huruma nao wapewe.

Mhe. Spika, nimpongeze Mkaguzi Mkuu wa Serikali kweli ni mwanamke jasiri. Mimi nilikuwa simjui lakini nilipomuona mara ya kwanza nikajua kwa nini watu wanampongeza. Ni mwanamke kweli hodari anafanyakazi yake vizuri, kwa hivyo tunapaswa tumpongeze.

Mhe. Spika, sio hivyo tu, panapokuwa na wanawake wenye uwezo hata huko serikalini tuwape nafasi. Kwa sababu tunachotafuta ni asilimia 50 sio kwenye Baraza tu la Wawakilishi na hata makazini pia. Ahsante kwa kunipa nafasi hii napenda nikushukuru na kuiunga tena mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Nakushukuru Mhe. Spika, kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Awali ya yote kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu, ambaye bado ananikirimu pumzi zake nikaweza kufika hapa na kusimama, ingawa nina malaria yaliyonizonga, lakini pia namshukuru kuniwezesha kufika ili kuja kuwatumikia wananchi ambao wamenileta hapa. Mhe. Spika, pia nampongeza waziri pamoja na watendaji wake, kwanza naunga mkono hoja.

Mhe. Spika, juzi nilipokuwa nikijibu swali la nyongeza ambalo lilitokana na swali nambari 124 tarehe 24/06/2011 nilisema kuwa Wizara yetu ya Elimu na Mafunzo ya Amali inakusudia kuajiri katika mwaka huu wa bajeti wa 2011/2012, tumekusudia kuajiri walimu 800, wakiwemo kati yao walimu 500 wa sayansi na walimu 300 wa *art*.

Mhe. Spika, nazungumza hivi kwa sababu kumejitokeza hoja hapa ya Mhe. Ussi Jecha Simai aliyesema ni kwa nini wale walimu wa vyeti hatuwaajiri. Mimi nilisema Mhe. Spika, tunakusudia kuwaajiri baada ya bajeti na walimu ambao tutawaajiri ni walimu wa digrii, diploma na vyeti.

Mhe. Spika, tutaanza na hao walimu 800 lakini tuna mahitaji mengi tu ya walimu, tuna skuli 21 ambazo ni mpya zinahitaji walimu, ni karibu walimu 552 ambao tunawahitaji. Pia katika skuli zetu hizi tuna mapengo ya walimu hususan wa sayansi tunahitaji kuwaajiri.

Kwa hivyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe hii ni taarifa kwenu na wananchi wetu huko, waombe ajira hizi zitakuwepo na tutaanza kuajiri hao walimu 800, lakini tutawaajiri tena Mhe. Spika, kila hali itakapoturuhusu kwa sababu tuna mahitaji ya walimu wengi.

Mhe. Spika, mchango wangu ulikuwa ni huo tu na kwa sababu ya afya yangu, kwa hivyo naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Kwanza kabisa nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia leo hii tukawa na afya njema na salama. Pia niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kutekeleza wajibu wake kwenye utumishi wa umma. Vile vile nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake kwa kukaa pamoja na wakatafakari kuendeleza juhudi za utawala wa umma.

Mhe. Spika, kwa sababu jioni hii kuna wachangiaji wengi basi sitaki niendeshe mjadala mkubwa, isipokuwa naichangia hotuba hii kwa kuiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Pia nachukua nafasi hii kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na wizara kwa kuweza kutekeleza jukumu lake walilopewa.

Vile vile niipongeze serikali kwa kuweza kuongeza mishahara kwa watendaji wake. Naipongeza serikali pamoja na wizara kwa kuwajali wastaafu kwa kuwapa kipaumbele kilichokuwa hakina kifani.

Mhe. Spika, nasema hivyo kwa sababu ya kujua kuwa serikali inawajali wananchi wake hatua baada ya hatua. Mhe. Spika, naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia kwa mia, kwa niaba ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo na kwa niaba ya Mkoa wa Kaskazini Pemba kwa asilimia mia kwa mia, ahsante. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naomba kwanza nikushukuru sana kwa kuweza kushiriki kwenye mjadala huu wa leo. Kwa sababu jana Mhe. Spika, hukuwepo lakini malaika wako walikuwepo.

Mhe. Spika, mimi pamoja na wenzangu kutoka wizarani tunamshukuru kwanza Mwenyekiti aliyekuwepo jana akikuwakilisha katika kuliongoza Baraza hili na bahati nzuri leo wewe mwenyewe umesema humtumi mtoto umekuja, nakushukuru kwa hilo.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia afya njema na uzima na namuomba pia awajaalie wale wote waliokuwa wagonjwa awaponyeshe ili waweze kuendelea na majukumu yao na kujenga taifa letu.

Mhe. Spika, vile vie nachukua fursa hii kukushukuru tena wewe Mhe. Spika, kwa kunipa fursa nyengine ili kutoa maelezo na kujibu hoja mbali mbali za Waheshikiwa Wajumbe. Mhe. Spika, pia nichukuwe fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wajumbe wote wa Baraza lako tukufu, hususan wale waliopata fursa ya kuchangia hotuba yangu na wale ambao hawakupata fursa.

Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe, walitoa hoja na maswali mbali mbali waliyoniuliza na wengine walichangia kwa maandishi. Michango yao itaijengea uwezo wa kiutendaji ofisi yangu ili kuhakikisha huduma bora kwa wananchi wa Zanzibar zinatolewa na kuwafikia kwa wakati.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena napenda kuishukuru Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi. Kwa aina ya pekee napenda kuishukuru Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika ya Baraza la Wawakilishi, ambayo imekuwa ikifanya kazi bega kwa bega na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali pamoja na taasisi zote za umma.

Mhe. Spika, kwanza napenda nieleze furaha yangu ya kuona kwamba wajumbe wako wote wa Baraza hili tukufu, kila aliyepata kuchangia kwa kusema hapa Barazani na wale waliochangia kwa maandishi, na wale ambao

nimepata kuzungumza nao kwenye *cordon*, basi wana thamini uungwana wa Rais wetu mpendwa Dk. Ali Mohammed Shein kwa kutekeleza ahadi ambazo alizitoa.

Mhe. Spika, napenda niwahakikishie kwamba huyo ndiye Dk. Ali Mohammed Shein, ana wajali ana wadhamini na kuwapenda sana wananchi wake wa Zanzibar. Kwa kiasi kile alichonacho kwa kupitia serikali yake, ndio hiki ambacho ameamua kuwatunuku watumishi wa umma.

Mhe. Spika, hotuba yangu imechangiwa na jumla ya wajumbe karibu 25, wale ambao nilikuwa nimewaweka hapa ni wajumbe 21, lakini bahati nzuri wengine wameongezeka hapa ambao nilishindwa kuwaweka kwenye orodha, kwa sababu taarifa uliyoitoa ilinionesha kwamba wachangiaji walikuwa ni wale 21. Lakini hata hivyo nitawataja na wale ambao sikuwaweka kwenye orodha yangu.

Mhe. Spika, hotuba yangu imechangiwa na wajumbe wafuatao;

Mhe. Ismail Jussa Ladhu Mwakilishi wa Jimbo la Mji Mkongwe ambaye alitoa maoni ya kamati kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Ali Abdalla Ali.
Mhe. Hija Hassan Hija
Mhe. Omar Ali Shehe
Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando
Mhe. Mgeni Hassan Juma
Mhe. Ussi Jecha Simai
Mhe. Rashid Seif Suleiman
Mhe. Panya Ali Abdalla
Mhe. Wanu Hafidh Ameir
Mhe. Hamza Hassan Juma
Mhe. Mohammed Khalid Haji
Mhe. Fatma Mbarouk Said
Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
Mhe. Salma Mussa Bilal
Mhe. Salmin Awadh Salmin
Mhe. Raya Suleiman Hamad
Mhe. Dk. Sira Ubwa Mamboya
Mhe. Zahra Ali Hamad
Mhe. Bihindi Hamad Khamis
Mhe. Hassan Hamad Omar
Mhe. Abdalla Juma Abdalla

Mhe. Spika, wajumbe wote hawa wamechangia hotuba hii kwa nia moja tu, ya kuimarisha na kurekebisha na kutusahihisha pale ambapo walihisi wao

waturekebishe. Napenda niwahakikishie wajumbe wote kwamba yale yote ambayo wametuambia tumeyasikia. Kwa bahati nzuri mengi yalikuwa ni ushauri na pongezi. Hata hivyo, Mhe. Spika, uwezo wa Mwenyezi Mungu nitajitahidi kuzitolea ufafanuzi hoja mbali mbali za wajumbe na maswali waliyouliza na maelezo yangu yatalenga moja kwa moja katika hoja za wajumbe badala ya kujibu hoja za Mhe. Mjumbe mmoja mmoja.

Katika kujibu hoja hizo ikiwa itajitokeza hoja ya mjumbe kutojibiwa basi isionekane kwamba ni suala lililofanywa kwa makusudi bali hoja hiyo itakuwa imetolewa ufafanuzi katika maelezo yangu ya jumla.

Mhe. Spika, katika hoja ambazo zilijitokeza namba niziseme na ufafanuzi wake kama hivi ifuatavyo. Lakini Mhe. Spika, kabla sijaendelea naomba radhi kwa kumsahau Mhe. Assa Othman Hamad kwamba na yeye alichangia kwa maandishi.

Mhe. Spika, hoja ya mwanzo ilikuwa ni kuhusu suala la mishahara mipya. Uko ushauri ambao ulitolewa na mimi nataka nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati kwa ushauri alioutoa, wa wafanyabiashara kutokuigeuza hatua njema ya serikali ya kupandisha mishahara kuwa kichocheo cha tamaa binafsi kwao na kupandisha bei za bidhaa. Mwenyekiti wa kamati ndiye aliyetoa ushauri huo. Maelezo na ufafanuzi kama hivi.

Mhe. Spika, katika kipengele chicho serikali itawasimamia wafanyabiashara na kuhakikisha kwamba hakuna mfanyabiashara atakayetumia nia njema ya serikali kujinufaisha yeye mwenyewe binafsi. Nadhani taasisi zinazohusika na maeneo hayo wanatusikia na watafuatilia mwenendo wa bei ambao utawekwa na wafanyabiashara wetu.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni kipindi cha mishahara mipya, kianze mwezi Julai badala ya Oktoba. Hoja hii mheshimiwa imeelezwa na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando, Mhe. Mohammed Khalid Haji na hii leo imezungumzwa pia na Mhe. Salmin Awadh Salmin na wachangiaji wengine.

Mhe. Spika, naomba nitowe maelezo yafuatayo. Ili kutekeleza malipo mapya ya mishahara ya serikali inahitaji kujipanga vyema kimapato kwa kubuni na kuviimarisha vyanzo mbali mbali vya mapato, kwani mishahara hii mipya itagharimu TShs. 126 bilioni kutoka mishahara iliyolipwa mwaka jana ya TShs. 80 bilioni. Hiyo ndio sababu ya msingi ambayo inatuwezesha sisi tusifanye pupa ya kuweza kusema tutalipa mishahara Julai, wakati tukijua kwamba kuna *deficit* ya mishahara iwapo kama tutaanza Julai.

Mhe. Spika, ongezeko hilo la mishahara limeongezeka kwa asilimia 57.5 ya nyongeza zote ambazo zinahitajika zilipwe kwa watumishi. Vile vile

tumejifunza kutokana na makosa yaliyotokezea nyuma. Hatutaki leo tunaanza kufanya zoezi hili tunawalipa wafanyakazi Ofisi ya Rais na Utumishi wa Umma Julai, ofisi nyengine tunakuja kuwalipa Oktoba na ofisi nyengine tunakuja kuwalipa Disemba, hapana. Tunataka tukianza zoezi hili serikali nzima, watumishi wote wa umma walipwe mishahara yao kwa mujibu wa kiwango ambacho kimerekebishwa, pamoja na zile nyongeza ambazo zilikosekana katika kipindi chote cha miaka ambayo zimekuwa hazitolewi nyongeza hizo na serikali.

Mhe. Spika, sababu nyengine pia ni jambo la busara kuanza kulipa mishahara hiyo wakati serikali imeshabaini idadi sahihi ya watumishi wa umma, ili upandaji huu wa mishahara usije ukatoa ufrsa ya ubadhirifu wa fedha za umma.

Waheshimiwa Wajumbe hapa wengi sana wametia shaka ya kuwepo kwa wimbi la mishahara hewa. Katika kipindi cha miezi mitatu tuna zoezi ambalo tunalifanya. Nafikiri huko mbele nitapata nafasi ya kuweza kulitolea ufafanuzi. Hizo ndio sababu za msingi.

Mhe. Spika, kuhusu kipindi cha mishahara mipya kianze mwezi wa Julai badala ya Oktoba nimeshalizungumza. Lakini kuhusu zoezi la kupandisha mishahara liwe ni la kila mwaka. Hili lilipendekezwa na Mhe. Omar Ali Shehe. Mhe. Spika, naomba nitowe maelezo yafuatayo.

Mhe. Spika, upandishaji wa mishahara hutegemea na ukuaji wa uchumi wa nchi na mapato ya serikali. Hivyo kadiri mapato ya serikali yatakavyo ongezeka, ndivyo maslahi ya watumishi wa umma ikiwemo mishahara yatakavyoimarika. Kwa hivyo, nawaomba watumishi wote wa umma wafanye kazi kwa juhudi na maarifa, ili hatimaye uchumi wa nchi yetu uwe imara na mapato yaongezeke na kupelekea maslahi yao kuwa bora zaidi.

Mhe. Spika, hoja nyengine iliyojitokeza ni suala zima la kukwepa majukumu ya kutangaza mshahara. Hoja hii ilitolewa na Mhe. Hamza Hassan Juma, ambayo ilijieleza kwa wale wambao walikuwa wanafuatilia mjadala, alieleza kwa nini jukumu hili Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo wasitangaze wao mishahara.

Mhe. Spika, naomba nitowe maelezo yafuatayo. Kazi ya kutangaza ongezeko la mishahara kwa watumishi wa umma ni ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mujibu wa sheria ya utumishi wa umma ya mwaka 2011. ni mazowea kwamba huko nyuma tulilipa jukumu hili Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. Lakini katika kuzingatia suala lile lile la utawala

bora, hawezi kuwa mtu anatafuta, yeye anatumia na anafanya kila kitu. Kwa hivyo, yeye kazi yake azitafute fedha halafu anipe mimi nizitumie.

Katika muundo wa serikali kuna uhusiano wa utekelezaji wa majukumu katika uhusiano huu, jukumu la Ofisi ya Rais Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo ni kukusanya mapato, wakati jukumu la Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kupanga maslahi ya watumishi, hili lipo kwa mujibu wa sheria.

Hoja nyengine Mhe. Spika, ilikuwa ni suala la ubunifu. Ushauri ulitolewa Idara ya Mipango Sera na Utafiti kuzidisha ubunifu, kuandaa mapendekezo ya miradi na maeneo mengine yanayohitajika kufanyiwa utafiti na sera na kufikishwa kwa washirika wa maendeleo. Hoja hii ilitolewa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu kwa niaba ya kamati. Ushauri huo uliotolewa na kamati umepokelewa.

Aidha, mazungumzo na serikali ya Norway kupitia ubalozi wao uliopo Dar es Salaam umefikia hatua nzuri, tunategemea watatusaidia katika maeneo mbali mbali ya utawala bora.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni ripoti za haki za binadamu. Ushauri kuzifuatilia ripoti zote zinazotolewa kuhusu haki za binadamu. Nao ushauri huu ulitolewa kwa kupitia aliyemwakilisha Mwenyekiti, Mhe. Ismail Jussa. Ushauri unapokelewa na tutaufanyia kazi.

Hoja nyengine Mhe. Spika, ni Mamlaka ya Kuzuwia Rushwa na Kusimamia Maadili ya Viongozi. Kuharakisha kuanzishwa kwa mamlaka na taasisi ya kuzuia rushwa. Nayo hii ilitolewa na kamati kwa kupitia Mhe. Ismail Jussa. Ofisi imo katika jitihada za kuanzisha mamlaka hiyo, kwa sasa mswada wa sheria hiyo umeshaandaliwa na utawasilishwa kwenye kikao kijacho cha Baraza la Wawakilishi cha mwezi wa Oktoba.

Mhe. Spika, ushauri mwengine uliotolewa kuhusu Kamati za Utawala Bora kuwa na uwakilishi wa taasisi zote. Nao ushauri huo ulitolewa na Mwenyekiti wa Kamati, suala hili tumelizingatia katika kuunda kamati hiyo. Kwa hivyo, tunaendelea kulifanyia kazi.

Mhe. Spika, hoja nyengine ni matumizi ya fedha ya mamlaka ya kuzuia rushwa na kusimamia maadili ya viongozi. Kulionekana kuweko kiasi fulani cha fedha kilichojionesha kwenye bajeti iliyopita cha kiasi ya milioni 4. Sasa je fedha hizo zimetumika au namna gani wakati hii taasisi haijaundwa. Hoja hii ilitolewa na Mhe. Hija Hassan Hija.

Fedha hizi kweli zilikuwemo kwenye bajeti au kwenye makadirio ya matumizi ya mishahara kwa kipindi cha Machi hadi Juni 2011. Lakini kwa kuwa Mamlaka hiyo haijaanzishwa fedha hizo hazijatumika na wala hatukuziomba. Kwa hivyo, fedha hizi zimebakia katika hazina ya serikali kwa sababu haja ya kuziomba ilikuwa haipo.

Hoja nyengine Mhe. Spika, ilikuwa ni ya uwajibikaji wa watumishi wa umma. Ushauri uliotolewa ni kuhakikisha kuwa wizara zote zinatekeleza wajibu wao kama ilivyoagizwa kwa mujibu wa sheria.

Hoja nyengine Mhe. Spika, ilikuwa ni kuweka mkakati wa kuwafanya wafanyakazi wawajibike na hoja hizi zilitolewa na Waheshimiwa Wajumbe watano; Mhe. Omar Ali Shehe, Mhe. Mbarouk Wadi Mtando, Mhe. Ashara Abdu Haji, Mhe. Nassor Salim Ali mabao walichangia kwa maandishi na Mhe. Rashid Seif Suleiman.

Mhe. Spika, ushauri unachukuliwa. Hata hivyo Ofisi imejitayarisha kuweka mkataba wa kutoa huduma kwa wananchi na mfumo wa upimaji wa utendaji kama nilivyoeleza kwenye hotuba yangu.

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni elimu ya uraia. Ushauri ulitolewa kuwa wananchi wapatiwe elimu ya uraia na hoja hii ilitolewa na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa Mtando. Mhe. Spika, maelezo ni kwamba zoezi hili limepangwa kutekelezwa kwa kuwafikia wananchi wote hadi katika ngazi ya shehia kwa kutumia mikutano ya wanavijiji katika shehia zao. Njia nyengine zinazotumika ni pamoja na majukwaa ya kiutamaduni na michezo ya kuigiza. Kwa hivyo, napenda kukuhakikishia Mhe. Spika, pamoja na Baraza lako tukufu kwamba utaratibu tumeuweka kwa ajili ya Elimu ya Uraia kuwafikia wananchi. *(Makofi)*

Hoja nyengine ilikuwa ni utaratibu wa kuwasilisha malalamiko. Kwa kweli hoja ilikuwa ni kuhusu wapi malalamiko yanatolewa na utaratibu upi unatumika kwa kutoa malalamiko na hoja hii ilikuwa ya Mhe. Mbarouk Wadi Mussa. Mhe. Spika, malalamiko yanapokelewa wizarani, kwa maana ya Wizara inayohusika na Utawala Bora. Utaratibu unaotumika ni kumuandikia Katibu Mkuu kwa malalamiko yanayohusu uwajibikaji katika Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Kwa hivyo, hapa naomba nitoe ufafanuzi zaidi, kwamba tunapozungumzia Utumishi wa Umma isieleweke au maana yake ni kwa Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, lakini taasisi yoyote ya serikali ina majukumu ya kuwatekelezea wajibu na kuwafanyia haki wananchi. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo, kita taasisi ni Taasisi ya Utumishi wa Umma, lakini malalamiko hayo yanaletwa kwa Katibu Mkuu Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa nini, kwa sababu yeye ndiye mwenye taasisi ya kupima hivyo vigezo vya uwajibikaji, utawala bora, Haki za Binadamu pamoja na mambo mengine.

Mhe. Spika, Katibu Mkuu atayashughulikia kwa taratibu ziliopo. Aidha walalamikaji wanayo haki wakipenda kupeleka nakla za malalamiko hayo kwa viongozi wengine, ili kuepusha hofu ya kutoshughulikiwa ipasavyo malalamiko yao, ikitokezea kwamba yule aliyepelekewa yale malalamiko pengine yeye yatakuwa yanamhusu. *(Makofi)*

Kwa hiyo, mwananchi anapotengeneza barua ya malalamiko anayo haki na fursa ya kumuandikia mhusika kwa mujibu wa utaratibu na nakla anaweza kuzisambaza kwenye taasisi nyengine.

Sasa ikiwa lile lalamiko linahusu taasisi nyengine, basi si vibaya anaweza kuipeleka, lakini na viongozi wa juu wanayo haki ya kuweza kupata taarifa hizi na hatimaye viongozi wa juu wanao uwezo wa kutuagiza kufuatilia malalamiko hayo. Kwa kweli hata kama yule ambaye amepelekewa lile lalamiko itakuwa lina mgusa. Lakini kwa sababu suala la kushughulikia malalamiko ni la umma tena la serikali, basi suala lake litashughulikiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Mhe. Spika, eneo jengine ni Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na jambo hili limejitokeza kwenye mjadala wetu. Kwa hivyo, swali lililouliza ni kuhusu hatua zinazochukuliwa na serikali kwa mapendekezo yanayotolewa katika Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Katika hili napenda nimshukuru sana Mhe. Omar Ali Shehe (Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC*). *(Makofi)*

Kwa kweli itakumbuka kwamba suala hili lilijitokeza wakati wa Kipindi cha Maswali na Majibu katika Mkutano wa Baraza uliopita. Lakini pamoja na kwamba nilitoa maelezo katika majibu yale, napenda tena nitoe maelezo yafuatayo:-

Mhe. Spika, napenda kuwahakikishia Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hivi sasa serikali imeichukulia hatua ya kuifanyiakazi na kwa mara ya kwanza ripoti hiyo imepelekwa na kujadiliwa katika Kikao cha Baraza la Mapinduzi na kuamuliwa kila wizara iliyoguswa na ripoti hiyo, basi ichukue jukumu la kurekebisha kasoro hizo zilizojitokeza katika taasisi zao. *(Makofi)*

Kwa kuwa wizara yangu ndio inayosimamia ukagusi pamoja na uwajibikaji, basi wizara yangu itahakikisha kwamba inazikumbusha wizara na kutoa taarifa katika Baraza lako tukufu Mhe. Spika. *(Makofi)*

Vile vile kuhusu muongozo wa maposho na matatizo ya wafanyakazi hewa. Suala hili lilijitokeza la wafanyakazi hewa, pia kuhusu muongozo wa maposho, kwamba nani anayetoa muongozo wa maposho. Mhe. Spika, wafanyakazi hewa katika Utumishi wa Umma inaonekana bado wapo, ni vyema serikali ikachukua hatua za makusudi, ili kudhibiti fedha za umma. Ushauri huu ulitolewa na Mhe. Hija Hassan Hija, Mhe. Mgeni Hassan Juma pamoja na Mhe. Omar Ali Shehe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

(a) Wizara yangu itatoa Muongozo uliowazi kwa Taasisi namna ya Zoezi zima la Marekebisho ya Mishahara na jinsi lilivyozingatia elimu na uzoefu wa watumishi, isipokuwa kila mfanyakazi aelewe utaratibu uliotumika;

(b) Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora ndio yenye madhamana ya kutoa muongozo wa namna ya maposho mbali mbali kwa Watumishi wa Umma.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako napenda nitumie nafasi hii kusema yafuatayo. Kwa nini tumelazimika kufanya vile. Kwanza tumelazimika kufanya vile kwa sababu sheria ndivyo inavyotaka. Lakini hivi sasa kama mtachunguza kuna wimbi la wafanayakazi kutaka kuhama kutoka taasisi moja kwenda taasisi fulani.

Kwa kweli kuna taasisi ambazo maombi ya uhamisho yamekuwa mengi sana na inatokana na huu ushawishi, kwa sababu pengine wao wanao uwezo wa kujipangia wanavyotaka, kwa hiyo wanajipangia maposho na wala hayalingani na Watumishi wa Umma katika taasisi nyengine.

Kwa hivyo, katika hili nataka niseme jukumu hili nimepewa mimi kupitia Wizara yangu ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, hivyo sitamvumilia mkuu wataasisi yoyote ambaye ataamua kujipangia maposho anavyotaka yeye, maana yake kama mimi sitamvumilia basi na Baraza tukufu halitamvumilia. *(Makofi)*

Sasa lazima kama tunafanya marekebisho ya Utumishi na kutaka watumishi wetu wawe na moyo wa kuitumikia nchi yao, basi lazima tuangalie kama kuna vishawishi vinavyoweza kumfanya mfanyakazi akafanya kazi yake vizuri, basi iwe kwa wote na sio kwa taasisi moja na nyengine ikakosa. Mhe.

Spika, naomba hili nilibainishe wazi. Kwa kweli nakiri kwamba hayo yapo serikalini, lakini hatua hizi zitatufanya tuweze kuchukua hatua ya kuweza kuweka usawa katika kuandaa na kutoa muongozo wa kutoa maposho mbali mbali katika Taasisi za Umma.

(c) Mhe. Spika, nakubaliana na maelekezo ya Mhe. Omar Ali Shehe kuhusu tatizo la kukimbiwa na wataalamu katika Utumishi wa Umma, tatizo ambalo kwa kiasi kikubwa linachangiwa na maslahi madogo.

Mhe. Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kuwa serikali imechukua hatua za makusudi katika marekebisho haya ya mishahara ya kunyanyua mishahara ya Wataalamu kwa kiasi kikubwa, ili kuwashawishi kubaki katika Utumishi wa Umma hapa Zanzibar. Suala hili pia alilizungumza Mhe. Salmin Awadh Salmin (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi ambaye ni Katibu na Mnadhim wa CCM ndani ya Baraza hili). *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda nimpongeze kwa kuchukua nafasi hiyo, nadhani atalanda miguu yangu katika kuitumikia nafasi hii. *(Makofi)*

Kwa kweli tunachokifanya na yeye amezungumzia suala niseme madaktari tumewaweka wapi. Lakini mimi nataka niseme kwamba tumezingatia maslahi ya wataalamu wote. Sasa katika kuzingatia vigezo hivyo na madaktari wamo.

Mhe. Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kuwa kiwango cha juu cha wataalamu kwa mujibu wa sifa pamoja *qualification* walizonazo kimepandishwa mpaka kwa asilimia 50, ili nisijenikajibu tena, isipokuwa watapishana kutokana na uzoefu pamoja na muda ambao mtu amepata ile *qualification*. *(Makofi)*

Nadhani tumejitahidi kuweka mazingira mazuri kwa wataalamu wetu, kwa kujua kwamba wataalamu wetu walikuwa wanatukimbia. Mhe. Spika, tutakumbuka kwamba vigezo hivyo pamoja na takwimu hizo ambazo amezieleza Mhe. Salmin Awadh Salimn, basi mimi kwa makusudi kabisa nimezifuata kwenye wizara husika ya *Management* ya Utumishi wa Umma na hivyo ndivyo vilikuwa vigezo, haidhuru hatutavifikia viwango vile.

Lakini nafikiri ukizingatia hali ya ugumu wa maisha wa Tanzania Bara na Zanzibar ukiwa na tofauti ya asilimia 5, ukizingatia uzalendo wa nchi yako, sidhani kwamba utakubali kuondoka nchini kwa kufuatilia ziada ya asilimia 5 katika nchi ambayo si yako au haikushiriki kikamilifu katika kukupatia ujuzi wako. *(Makofi)*

Mhe. Spika, katika hili nawaomba wataalamu wetu watulie na tumewatengezea maslahi yao, imani yangu kwamba kuanzia sasa tunaanza ukurasa mpya nafikiri wataalamu wetu wataendelea kubakia nchini. *(Makofi)*

Mhe. Spika, suala jengine ni kuhusu Ajira kwa Wazanzibari katika Taasisi za Muungano. Kwa kweli jambo hili lilikuwa ni miongoni mwa hoja zilizoulizwa na tumetakiwa kutoa ufafanuzi na hoja hii iliulizwa na Mhe. Omar Ali Shehe. Kwa hivyo, naomba nitoe maelezo yafuatayo.

Suala la Ajira katika Taasisi za Muungano linashughulikiwa kupitia vikao vya Mashirikiano kati ya Ofisi zetu zenye majukumu yanayofanana ya SMT na SMZ. Mhe. Spika, tayari tumeshakubaliana juu ya Zanzibar kuwa na sehemu maalum kwa kuzingatia idadi ya nafasi za ajira.

Kwa hivyo, Timu ya Wataalamu watakaoshughulikia utaratibu wa namna mgao wa ajira utakavyokuwa umehusisha wajumbe kutoka pande zote mbili za Muungano. Aidha *Secretariat* ya Ajira ya Muungano imeshaleta maombi yake ya kufungua ofisi Zanzibar, ili kutoa fursa zaidi za ajira kwa Wazanzibari katika Taasisi za Muungano. *(Makofi)*

Mhe. Spika, naomba nieleze badala ya kusuburi kusifiwa bora nijisifu mwenyewe. Katika kipindi kifupi tokea tumekuwepo Madarakani Awamu ya Saba jambo hili tumelikuta kwamba ni kero, Wizara yangu na Wizara ya *Management* ya Utumishi wa Umma chini ya Usimamizi wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na Ofisi ya Makamu wa Rais na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungnao wa Tanzania, tumekuwa na mazungumzo na hili tayari tumeshalimaliza.

Kwa hivyo, tunachokifanya sasa ni kutafuta ofisi hata ya kukodi, ili *Secretariat* hii ije hapa na itakuwa ikifanya maamuzi. Hivyo, kutakuwa na watu wawili kutoka Zanzibar na wawili kutoka Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, watakaokuwa wanashughulikia maombi na *interviews* zitakazofanyika kwa Wazanzibari, yaani kwa mujibu wa zile nafasi zitakazokuwa zimetengwa kwa ajili ya Zanzibar.

Mhe. Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba jambo hili sasa tumefikia pahala pazuri, hivyo muda si mrefu Wazanzibari watafaidika katika nafasi za ajira kwenye Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa mujibu wa taratibu ambazo tumekubaliana. *(Makofi)*

Hoja nyengine Mhe. Spika, ni kuhusu Umri wa Kustaafu Kazi kwa Watumishi wa Umma na hii ilitolewa na Mhe. Mgeni Hassan Juma, hasa

ilizungumzia suala la kwa nini wanawake wameekewa kiwango cha kustaafu mapema kuliko wanaume. Mhe. Spika, naomba nitoe maelezo yafuatayo.

Kabla ya mwaka 2005 hapakuwa na uwiano wa umri katika kustaafu kazi baina ya watumishi wakike na wakiume, ambapo watumishi wakiume walitakiwa kustaafu kazi kwa lazima watakapofikia umri wa miaka 60 na wafanyakazi wakike walitakiwa kustaafu watakapofikia umri wa miaka 55. Kwa mujibu wa kifungu Nam. 44 cha Sheria ya Ajira ya mwaka 2005, imeweka bayana umri wa kustaafu kazi kwa lazima kuwa ni miaka 60 kwa watumishi wakike na wakiume, ili kuwa na uwiano sawa wa kijinsia. *(Makofi)*

Kwa hivyo, lile ambalo alililokuwa akilizungumza Mhe. Mjumbe lilikuwa la sheria za zamani na sheria hiyo tayari imesharekebishwa na hivi sasa tumezingatia uwiano wa kijinsia. Mhe. Spika, hata Sheria yetu ya Utumishi wa Umma imeelezea hilo pamoja na kufafanua, yaani inatambua kuwepo kwa uhusiano na uwiano wa kijinsia katika nafasi za Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mhe. Spika, hoja nyengine ilikuwa ni kupandisha daraja kwa Watumishi wa Umma nalo lilikuwa na Mhe. Mgeni Hassan Juma, naomba nitoe maelezo yafuatayo.

Wakati nilipowasilisha Hotuba ya Makadirio na Mapato nilieleza kwamba ofisi yangu imetayarisha miundo ya utumishi, yaani *Scheme of Services* kwa kada zote kwa Watumishi wa Umma. Moja miongoni mwa kazi ya miundo ya utumishi ni kutoa muongozo wa kiutumishi juu ya namna ya watumishi watavyopanda daraja, muongozo ambao unatoa fursa sawa kwa watumishi wa jinsi zote.

Mhe. Spika, napenda kulithibitishia Baraza lako tukufu kuwa miundo ya kiutumishi kwa kada zote tayari imeshawasilishwa katika mawizara yote pamoja na taasisi za serikali.

Vile vile hoja nyengine ilikuwa ni kukamilisha jengo lililonunuliwa kwa ajili ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Spika, ilielezwa kwamba ofisi iwezeshe Ofisi ya Kadi kukamilishi ujenzi wa jengo hilo na hoja nyengine ilikuwa ni ufafanuzi kuhusu fedha za maendeleo ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hoja hizi zilitolewa na Mhe. Omar Ali Shehe na Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Naomba nitoe ufafanuzi ufuatao Mhe. Spika.

Serikali na ofisi inakubaliana na mapendekezo hayo, kwa ajili ya kupunguza ufinyu wa ofisi uliopo hivi sasa. Aidha Kamati ilitaka ufafanuzi juu ya fedha

za kazi za maendeleo zilizoingizwa kimakosa katika kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ambazo ni shilingi 196,350,000/-.

Mhe. Spika, naomba nilifahamishe Baraza lako tukufu kwamba hizi ni fedha za mkopo kupitia Mradi unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika unaodhibitiwa na Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, ambapo fedha hizo zimepangwa kutolewa kwa Ofisi ya Mdhibiti kupitia hesabu ya miradi ya Wizara hiyo ya Fedha kwa shughulikia mambo mbali mbali ya mipango ya maendeleo ya Ofisi ya Mdhibiti pale ambapo itakapohitajika.

Kwa hiyo, Wizara ya Fedha ndio inayosimamia, lakini kimsingi fedha hizi baadaye na kwa sababu tayari ziko kwenye *vote* ya Wizara ya Fedha basi hatuwezi tena tukazionesha kwenye *vote* yetu ya Utumishi wa Umma.

Suala jengine ni kuhusu Bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pengine labda serikali izingatie suala zima la kuipa umuhimu na kupandisha au kuongeza Bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Spika, Waheshimiwa Wajumbe wameitaka serikali iongeze Bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na iwe inaipatia fedha zote zilizoidhinishwa. Hoja hii imeletwa na Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Omar Ali Shehe. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba tayari serikali imeshalichukulia hatua suala hilo kwa kipindi cha miaka mitatu sasa. Kwa kweli serikali huongeza Bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kila mwaka na ofisi hii hupatiwa fedha zake zote zilizoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, kila hali itakaporuhusu, basi serikali itaendelea kumuongezea Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali fedha au mafungu, ili aweze kutekeleza majukumu yake vizuri. Kwa mfano, fedha zilizonunuliwa jengo la ziada la Mdhibiti, kwa sababu tayari serikali imejua kwamba sehemu yake ya kufanyiakazi ni finyu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, napenda kuliarifu Baraza lako tukufu kwamba fedha zilizonunuliwa jengo la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ambalo limeombewa fedha hapa na Waheshimiwa Wajumbe pamoja na sisi wenyewe tutajitahidi litengenezwe, ili waweze kuhamia na wala fedha hizi hazikuwemo kwenye bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. *(Makofi)*

Lakini kwa kuzingatia uzito wa kazi za Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, basi serikali imetoa fedha kwa ajili ya kununulia

jengo hilo kwenye kasma maalum iliopo pale Wizara ya Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo. *(Makofi)*

Kwa hivyo, serikali itaendelea kufanya hivyo kila pale haja itakapotokea, lakini hivi sasa Bajeti ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka jana na ile ya mwaka huu basi mtaona kwamba imeendelea kukua. *(Makofi)*

Mhe. Spika, pia kuna hoja kuhusu Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, iwezeshwe na ihakikishiwe kufanya ukaguzi wa kisasa unaohusiana na ukaguzi wa thamani, yaani *value for money*, ukaguzi wa mazingira pamoja na *computers*, hoja hii ilielezwa na Mhe. Hija Hassan Hija na Mhe. Omar Ali Shehe. Mhe. Spika, naomba nieleze yafuatayo.

Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, tayari imeshaanza kufanya aina hizo za ukaguzi na tunategemea ripoti mbili za ukaguzi zitakazowasilishwa muda mfupi ujao kwenye Baraza la Wawakilishi, ambapo matayarisho yake yapo tayari.

Kwa kweli imezingatia ukaguzi yakinifu, zitatoka pamoja na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2009/2010, ambapo ripoti hizo kwa pamoja zitawasilishwa katika Baraza hili tukufu, kwa sababu ziko kwenye hatua za mwisho. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nia ni kwamba tunataka twende na wakati kama Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi walivyotushauri katika Mkutano uliopita wakati tulipokuwa tukijadili Ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* na michango mbali mbali ilionesha hivyo. *(Makofi)*

Serikali ya Awamu ya Saba yenye Mfumo wa Umoja wa Kitaifa inayoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein inajali sana kupokea ushauri unaotolewa na Baraza hili tukufu na inazingatia suala la Utawala Bora na Uwajibikaji. Mhe. Spika, kwa kuelewa majukumu ya Baraza la Wawakilishi ndio pale nyuma nilisema kwa mara ya kwanza serikali kupitia Baraza la Mapinduzi imejadili ripoti ile, hivyo ushauri wote uliotolewa na Baraza umezingatiwa. *(Makofi)*

Aidha katika kuhakikisha aina hizo za ukaguzi zinapewa kipaumbele Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, imetayarisha Mpango Mkakati mpya, yaani *Strategic Plan* ambao kwa kiasi kikubwa umezingatia aina hizo za ukaguzi. Mpango huo utakuwa wa miaka mitatu kuanzia mwaka huu wa fedha ulioanza leo.

Mhe. Spika, hoja nyengine ni suala la ufafanuzi kuhusu tarakimu za fedha zilizooneshwa tofauti baina ya kiwango kilichooneshwa baina ya hotuba na mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi na hoja hii ililetwa na ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija. Kwa kweli usahihi wa fedha hizo ni kama ulivyojitokeza katika kitabu cha Mswada wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ambazo ni shilingi bilioni 1 milioni 284/- kwa mwaka wa fedha huu.

Mhe. Spika, hiyo inatokana kama tunavyojua tatizo hili haliko katika wizara yangu tu, isipokuwa limejitokeza katika wizara nyingi za serikali, kwamba kuna mparaganyiko na ndio maana Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alitoa *statement* kwamba atatoa kitabu chengine ambacho kitaonesha uhalisia wa mafungu yalivyo. *(Makofi)*

Hoja nyengine ni kujua serikali ina mpango gani katika kuhakikisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, inapata uwanachama katika Jumuia tofauti za Wakaguzi Afrika na duniani kwa jumla zikiwemo *AFROSAI* na *INTOSAI*. Mhe. Spika, hoja hii ilizungumzwa na Mhe. Omar Ali Shehe ambaye ni ndugu yangu Mtumbatu anayeishi Pemba kama alivyo Mhe. Hija Hassan Hija Mtumbatu anayeishi Mwambe. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Spika, mazungumzo ya kuomba uwanachama katika Jumuia hizo yanaendelea katika Ofisi na *Secretariat* ya Jumuia hizo. Hata hivyo, kwa hivi sasa ofisi hiyo inaendelea kufaidika na Jumuia hizo kwa kushiriki mikutano na mafunzo yote yanayotolewa na Jumuia hizo kupitia kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aidha Mhe. Omar Ali Shehe alitaka kujua nafasi ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kufanya ukaguzi kwenye Taasisi za Muungano.

Mhe. Spika, wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar, tayari imeshapanga utaratibu wa kuzungumza na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Jamhuri ya Muungano, ili kuona utaratibu gani utatumika kushirikisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Zanzibar katika kukagua ofisi hizo za Muungano zilizopo hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, kama tunavyojua kuwa suala hili lipo kwa mujibu wa sheria. Sasa kama suala lipo kwa mujibu wa sheria hatuwezi tukakurupuka, lazima tufanye mazungumzo na halafu tuone namna gani tunaweza kukubaliana na jinsi gani ofisi yetu ikashiriki katika kufanyakazi hii.

Kwa kweli wazo hili ni muhimu na wala serikali hatuwezi kulipuuza, kwa sababu litatuongezea ufanisi wa kujua maovu na mazuri yanayofanyika katika Taasisi za Muungano zilizopo hapa Zanzibar, hasa kwa kuwa fedha zile zinazokusanywa hapa ni mapato yanayotumika kwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na wala si Serikali ya Muungano. *(Makofi)*

Hoja nyengine ni mazingira magumu ya Ofisi Kuu Pemba, yaani Ofisi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Spika, Ofisi Kuu Pemba kuchukua hatua ya makusudi kuona ofisi hiyo inapata mahitaji yake ya msingi kwa ajili ya kuweza kufanikisha utekelezaji wa majukumu. Hoja hii ilitolewa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu ambaye ni rafiki yangu kwa niaba ya kamati. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni kweli wakati walipotembelea kamati napenda nikiri kwamba wizara yangu Pemba ilikuwa na chumba kimoja unusu labda niseme hivyo na hiyo ilitokana na mgawanyiko kati ya Wizara ya Katiba na Sheria na Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Hali hii imejitokeza kutokana na kwamba Ofisi ya Utawala Bora ilikuwa ndani ya Wizara ya Katiba na Sheria, sasa ulipotokea mgawanyiko au mpangilio huu kweli lilijitokeza tatizo la ufinyu wa nafasi.

Sasa hatua gani serikali imechukua. Kwa sasa ofisi imefanikiwa kupata jengo la kukodi lenye ghorofa tatu, ambalo limepangiwa wizara tatu na kila wizara imepata vyumba vinane, ingawa haikidhi haja, lakini ni afadhali kuliko ilivyokuwa wakati ule na ushauri wa kamati tunaupokea.

Lakini hatuishii hapo kwamba ndio tumeridhika lakini kuna mpango madhubuti wa kuimarisha Ofisi za Serikali, kwa hivyo wizara yangu na wizara nyengine tunaratajia kujenga jengo ambalo litakidhi mahitaji ya kukaa Wizara tatu kwa pamoja katika eneo la Gombani kule Chake Chake Pemba.

Hoja nyengine ilikuwa ni ya utendaji wa Idara ya nyaraka na kumbu kumbu za taifa, hoja ilikuwa kubwa ni suala la nyumba binafsi zinunuliwe kutoa nafasi zaidi kwa taasisi ya nyaraka, Mwenyekiti wa Kamati alilisema hili kupitia Muwakilishi wake Mhe. Ismail Jussa Ladhu lakini na wajumbe wengine wameonesha nia yao ya kupenda na kuithamini taasisi hii ya nyaraka na umuhimu wake. Wazo hili Ofisi imelipokea na kulifanyia kazi kwa sasa Idara kwa kushirikiana na Wizara imeonana na muhusika, kilichojitokeza ni kuwa ujenzi ulifanyia zamani mnamo miaka ya 1970 yaani ujenzi ule usionekane kama kwamba umefanyika jana, ujenzi ule umefanyika kwenye miaka ya 1970 mimi sijamaliza skuli bado na baadhi ya wamiliki wanazo hati miliki za eneo lile.

Hata hivyo wameeleza kuwa wako tayari kuondoka ikiwa serikali itawalipa fidia inayolingana na soko, kwa hivyo kazi ya kufanya mazungumzo taasisi ya nyaraka kwa kushirikiana na wizara yangu tumeshamaliza kazi hiyo tunachosubiri ni kupeleka mapendekezo yetu serikalini ili kuona kwamba hilo jambo linapatiwa ufumbuzi.

Hali mbaya ya makumbusho hili jambo limeelezwa na Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando) na Mhe. Mgeni Hassan na hata Doctor Sira Mamboya nafikiri na yeye ameligusia suala la makumbusho, lakini amelizungumza kwa namna nyengine, napenda nilielezee Baraza lako tukufu kwamba idara ya Makumbusho kwa sasa haipo tena katika wizara yangu kufuatia muundo mpya wa serikali, idara maalum inayoshughulikia makumbusho na mambo ya kale imehamishiwa Wizara ya Habari Utamaduni Utalii na Michezo. Kwa hivyo naomba wajumbe mawazo yao wasubiri siku ya Wizara ya Habari Utamaduni Utalii na Michezo ndio inayohusiana na masuala ya makumbusho ili waje wapate ufafanuzi wa kina juu ya hoja ambazo waliziuliza.

Mhe. Spika, nyaraka za Zanzibar ziliopo nje ya nchi hoja ilikuwa ni kuzirejesha nyaraka za Zanzibar ziliopo nje ya nchi, hoja hii ilitolewa na Mhe. Mgeni Hassan Juma kwanza tunamshukuru kwa makusudi mazima alipopata kwenda Ujerumani na kufika kwenye jengo la nyaraka, hiyo inaonyesha kwamba yeye ni mtu ambae anathamini sana masuala haya ya nyaraka tunakupongeza sana.

Hata hivyo napenda nitoe maelezo yafuatayo katika mazingira mazima ya kuona umuhimu na hili limezungumzwa pia na Mhe. Amina Iddi Mabrouk, serikali itafanya kila njia kudhibiti nyaraka zake za kihistoria tulizokuwa nazo kwa kuweka mitambo maalum ya kufuatilia mwenendo mzima wa ndani ya jengo la nyaraka kwa kuweka CCTV, hii kazi namuongezea sifa tena ili na nyinyi mjue umahiri wa kazi inafanywa kupitia wataalam tulionao pale kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, hatuhitaji mtaalam kutoka pengine wala hatuhitaji *consultant* wa kumlipa mapesa kufanya kazi hii, tutaifanya kazi hii kupitia wataalam wetu ambao wapo pale katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hiyo ni kuonyesha kwamba umakini wa serikali katika kulipa uzito suala la udhibiti wa nyaraka.

Aidha juhudi zitafanywa kwa kufuatilia nyaraka zilioko nje hasa katika nchi zilizokuwa na mahusiano ya karibu na Zanzibar kama vile Oman, Uingereza, India, Urenu, Goa na kadhalika, hata hivyo nyaraka zilioko nje zina sura nyingi. Baadhi yao zimetokana na mawasiliano rasmi yaani *official correspondence* na asili yake ni nchi husika, nyaraka ambazo ama wakati wa vita, wizi au nchi inapogawika hizi ni mali ya nchi husika serikali itazidisha

juhudi katika eneo hili kwa kuzitafuta kumbu kumbu zetu zote popote zilipo. Baada ya kuzibaini tunawahakikishia kwamba tutazifuatilia sio kwa ubabe hatuna helkopta kama zile za NATO za kwenda kutua kwenye jumba la nyaraka tukaweza kuzichukua, lakini tutafanya mawasiliano na nchi husika tutafanya mazungumzo ya kidiplomasia ili tuweze kuzipata hizi nyaraka zetu ambazo tuna wasi wasi wa kuwa zimetoweka.

Hoja nyengine Mhe. Spika, ni mafao ya wastaafu, ilitoka hoja kwamba mafao ya wastaafu yaangaliwe na kuongezwa na hoja hii imetolewa na Mhe. Mohammed Haji Khalid na wachangiaji wengine wa jioni wamo ambao wamegusia nafikiri Mhe. Salma Mussa Bilali amechangia hoja hii. Suala hili serikali imeshalitolea maamuzi kwamba maslahi yale ya wastaafu yazingatiwe na yaongezwe, Wizara husika ambayo ni Wizara ya Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo italitolea maelezo mazuri wakati wa bajeti yake utakapofika.

Idara ya Utumishi na uendeshaji hoja zilitolewa kwamba Idara ya Utumishi na Uendeshaji ziliopo katika Wizara na Taasisi mbali mbali za umma ziratibiwe chini ya Afisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora, tunamshukuru aliyeleta hoja hii Mhe. Rashid Seif Suleiman Muwakilishi wa Ziwani, ushauri ni mzuri na unakwenda sambamba na masharti ya sheria ya utumishi wa umma, hivyo ndivyo inavyotakiwa kwa maelezo zaidi kama vile ilivyo wahasibu wakuu na watunza fedha na watu wa takwimu huwa wanasimamiwa na Wizara ya Fedha na hawa nao watapata miongozo inayotokana na sheria ya utumishi kutoka Wizara ya Utumishi wa Umma na utawala bora. Ili kuepusha lile suala la kila mmoja kuondoka na vyake lazima watumishi wote waende kwa mfumo ulio sawa unaozingatia maslahi na tija kwa wananchi tunaowatumikia.

Mhe. Spika Tume ya Utumishi kuhusu tume ya utumishi kuna madai ya kufukuzwa kazi kinyume na utaratibu na kutojibiwa kwa malamiko yanayopelekwa kwenye tume, hoja hizi zilielezwa na Mhe. Moh'd Haji Khalid na Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, maelezo ni kwamba waliohusika na kadhia hiyo walishawasilisha madai yao kwenye tume maalum ambayo ilipitia malalamiko yote na kuyatolea maamuzi na wahusika walipewa taarifa rasmi na hatua za kuchukuliwa, sasa kama hizo hatua hazijachukuliwa inawezekana pengine kutakuwa kuna sababu za msingi ambazo zitakuwa hazijachukuliwa. Lakini kila mmoja alipata ufafanuzi na maelezo na hatua ambazo zinatakiwa zichukuliwe.

Suala jengine kuhusu kutojibiwa malalamiko kwanza kwa ninavyoliangalia lalamiko la kijana wa Mhe. Makame Mshimba Mbarouk ambae amelisema ili mwananchi wake pale ajue kwamba amemtetea, suala hili jana lilizungumzwa kwa kina na Mhe. Waziri wa Nchi Afisui ya Rais na

Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, lakini kwa utaratibu wa sheria ya utumishi wa umma suala hili linashughulikiwa na tume ya utumishi ya Idara maalum, alikuwa ni askari ambae amefukuzwa kazi bila ya kuelewa utaratibu uliotumika. Hata hivyo suala hili linashughulikiwa na Tume ya Utumishi Idara Maalum na wakati utakapofika wa kuundwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma ambayo ndio itakayokuwa chombo kikuu cha hizi Tume nyengine, kitakachokuwa na uwezo wa kupokea rufaa kutoka hizi tume nyengine basi kama litakuwa halijafikia hatua namshauri Mhe. Makame Mshimba kwa kushirikiana na huyu kijana basi lipelekwe kwenye tume au kamisheni ya utumishi wa umma ambayo ndio itakuwa inashughulikia rufaa za watumishi wote wa umma, kwa maana mpaka Mahakama baada ya tume zao kushindwa lakini baada ya kuyashughulikia haya na kama wakishindwa kutoa ufumbuzi.

Kwa hivyo tume nyengine ya kamisheni itakayohusika kwa wakati huo itakuwa ni kamisheni ya utumishi wa umma, lakini nahisi hili jambo bado linashughulikiwa na tume ya utumishi ya idara maalum kwa mujibu wa sheria.

Mafunzo ya watumishi. Ulikuja ushauri kupatiwa takwimu za kijinsia kwa watumishi waliopata mafunzo na hili lilielezwa na Mhe. Hija Hassan Hija, lakini na Mhe. Mgeni Hassan Juma pia alilieleza hili suala, watumishi wa umma waliopatiwa mafunzo ya muda mfupi jumla ya watumishi sitini na mbili wamepatiwa mafunzo, kati ya hao 22 wanawake na 40 wanaume.

Kwa upande wa mafunzo ya muda mrefu jumla ya watumishi 21 wamepatiwa mafunzo kati ya hao 7 wanawake 14 wanaume, Mheshimiwa ukihitaji majina na orodha tunazo tutakupatia lakini kwa hapa naomba nitoe takwimu zinazoonyesha uwiano na jinsi hizi shughuli zilivyoshughulikiwa.

Waajiri kutokuwalipa watumishi ada ya mafunzo nalo hili lilizungumzwa na Mhe. Mgeni Hassan Juma maelezo yake ni kwamba ofisi imetaka kila taasisi kuandaa mipango ya mafunzo, ili kuandaa mpango wa kitaifa wa mafunzo na ofisi itasimamia na kuhakikisha kwamba watumishi wanaokwenda masomoni wanahudumiwa ipasavyo na taasisi zao.
Utaratibu uliokuwepo kulikuwa na vurugu mechi kila mtu anafanya anavyotaka, sasa idara ya mafunzo ya watumishi wa umma iko chini ya Wizara Nchi, Afisi ya Rais na Utumishi wa umma ipo kwa mujibu wa sheria na kazi zake zimeelezwa katika sheria, ikiwemo hii ambayo Mheshimiwa ametushauri kuifanya.

Mwisho Mhe. Spika, mapato na matumizi ya Chuo hili lilielezwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, napenda nilihakikishie Baraza na Mheshimiwa Ismail Jussa Ladhu kwamba maelezo ya mapato na matumizi ya chuo yapo yale ya

mwaka 2010/2011, kiasi cha fedha kilichokusanywa kilikuwa ni Shs. 253,670,000 na matumizi ni Shs. 222,568,000 kwa hivyo mapato yalaiyokusanywa yapo, lakini kwa sababu huwa hayaingii hapa moja kwa moja na wakati tulipokuja kwenye kamati bahati mbaya ni kwamba tulikuwa hatukuelewa hasa suala lilivyoulizwa. Lakini napenda kukuhakikishia kwamba hayo yapo na ni kama hivi nilivyoyataja.

Mhe. Spika, mambo mengine ambayo yamesemwa katika wachangiaji wa jioni kwanza napenda nimshukuru sana Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kunisaidia kujibu hoja ile ya uajiri wa walimu, nadhani sina haja ya kurejea. Lakini yamaejitokeza mambo haya namshukuru pia Mhe. Raya Suleiman Hamad yale yote aliyoyaeleza napenda nimhakikishie kwamba tumeyazingatia na tunayafanyia kazi, ndio maana hotuba yangu imejieleza vizuri juu ya suala la watu wenye virusi vya ukimwi, juu ya suala la watu wenye ulemavu na uwiano wa ajira utakavyofanyika kwa mujibu wa sheria.
Kwa hivyo yale yote aliyoyaeleza Mhe. Raya Suleiman Hamad tunayajua na tumeyazingatia na hivi sasa tunaendelea kuyafanyia kazi.

Yale mambo mengine uliyoeleza ni muhimu na nataka nikuhakikishie kwamba tutayafanyia kazi vizuri .

Mhe. Salma Mohammed Ali mambo mengine yale nimeshayaeleza katika hoja ambazo waheshimiwa wengine ambazo wameshaeleza na yale mengine nimeshayajibu katika hoja zilizotangulia mwanzo.

Mhe. Amina Iddi Mabrouk nafikiri na yeye vile vile suala la umuhimu wa kutunza nyaraka nafikiri nimeshalieleza, kupata eneo na vitendaa kazi Mhe. Amina Iddi Mabrouk yeye nafikiri alikuwa ni Mjumbe wangu kamati ya Katiba Sheria na Utawala katika awamu iliyopita, wakati ule tulipokuwa tunatembelea taasisi ile hali ilikuwa hivyo alivyoieleza naomba kulihakikishia Baraza lako tukufu kwamba tumepiga hatua, sio kama vile nilipokuwa nikienda mimi kukagua shughuli za serikali tukishirikiana na Mhe. Amina na wajumbe wengine wa Kamati ya Katiba Sheria na Utawala, pamoja na Mhe. Abdalla Juma na wengine. Sasa hivi hali sio vile ambavyo ameieleza sivyo ilivyo kuna mabadiliko, hata hivyo katika bajeti yetu tumelizingatia hilo la kutaka kuimarisha.

Lakini pia vile vile lilijitokeza suala la ufinyu wa jengo napenda kutumia fursa hii kusema kwamba mwenyekiti aliligusia anasikia wkamba tuna mpango ni kweli Serikali nzima ina mpango wa kujenga Ofisi za Serikali, ukitaka nionyeshe kwangu nitashindwa kwa sababu bajeti ile iko Wizara ya Fedha, kwa nini uko uzoefu unaonyesha kwamba kuna taasisi ziliingiziwa fedha za ujenzi lakini mpaka mwaka wa matumizi unamaliza fedha zile bado

hazijatumika. Lakini pengine kunaweza kuwepo taasisi nyengine ambayo ipo tayari na haikupangiwa bajeti, kw hivyo ikaonekana ni busara pesa zile zibakie kwenye fungu maalum kwenye fedha za mitaji ya umma.

Kwa hivyo ni kweli Wizara yangu inao mpango huo na kwa taarifa ya baraza lako tukufu napenda niwahakikishie kwamba michoro hiyo ipo tayari, tunasubiri tupitishe bajeti tupeleke michoro yetu serikalini ili tuone mahitaji yanayohitajika, mkakati wa serikali angalau kila jengo likae Wizara mbili au tatu na kwa sisi tulivyo basi Wizara yangu itakuwa na Ofisi ya Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, na taasisi nyengine ambazo ziko chini ya usimamizi wa wizara hizi mbili. Katika hili tunataka kuifanya ile Ikulu iwe ni ikulu ya kufanya kazi Rais na Afisi yake ya faragha na wengine tumpe nafasi Mhe. Rais pale tukae kwenye maeneo yetu na sisi tufanye kazi kwa mujibu wa taratibu wa kawaida.

Mhe. Spika, suala la Mhe. Salmin Awadha Salmin nimeshalitolea ufafanuzi lakini nataka unipe ruksa nimalizie moja tu ambalo limezungumzwa na Mhe. Naibu Waziri wa Afya, sisi kazi yetu ni kutengeneza maslahi ya watumishi, mishahara na maposho na kuangalia uwajibikaji wa taasisi husika kama inazingatia masharti ya kuwatendea haki watumishi.

Sasa nimuombe Mhe. Naibu Waziri lile la mavazi liko ndani ya uwezo wa Wizara yake ya Afya kwa hivyo kama amelipanga vizuri kwenye bajeti yake watumishi watapata sare, kama amelisahau basi kabla hajawasilisha hapa bajeti yake pengine basi afanye mazungumzo na Waziri anayesimamia fedha ili aweze, lakini nataka nimhakikishie yale mengine yote ya usimamizi nani anataka kwenda masomoni ni kweli sisi tunaratibu. Lakini mipango ile na ndio maana tumesema kila taasisi itaweka mpango wake kwa miaongozo tutakayowapa sisi, sasa watu kwenda masomoni kiholela hilo litakuwa ni jukumu lao lakini sisi tutatoa miongozo.

Mhe. Spika, kwa sababu ya muda kwa wale ambao sikuwajibu naomba waelewe kwamba sikuwajibu kwa sababu tu ya muda, naomba sasa kwa heshima na taazima nitoe hoja, waheshimiwa wajumbe kuyakubali makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Katiba na Sheria: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Tunakushukuru Mhe. Waziri kwa jitihada kubwa ya kufafanua hoja mbali mbali. Sasa niwahoji wale wanaokubaliana na hoja hii ya makadirio ya Mapato na Matumzi ya Wizara ya Nchi (AR) Utumishi wa

Umma na Utawala Bora wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Uatawala Bora: Mhe. Spika, kwa kuwa baraza limeyakubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora sasa naliomba Baraza lako tukufu likae kama kamati ya matumizi, ili kuvipitisha vifungu vya matumizi ya Wizara yangu.

Mhe. Spika. naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI FUNGU 11 AFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESBU ZA SERIKALI

Kifungu 0201	Utawala Unguja	5,000,000
Kifungu 0201	Utawala Unguja	1,025,546,000
Kifungu 0301	Afisi Kuu Pemba	258,454,000
Jumla ya Fungu		**1,284,000,000**

FUNGU 44 WIZARA YA NCHI (AR) UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Kifungu 0101	Idara ya Utawala Bora	115,526,000
Kifungu 0111	Idara ya Miundo ya Taasisi Utumishi na maslahi ya watumishi	61,453,000
Kifungu 0301	Afisi Kuu Pemba	

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti nakushukuru na namshukuru Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri na fasaha. Naomba kauli yake ndogo tu katika majibu yake kwa hoja ya Kamati inayohusu Pemba. Alisema kwamba limepatikana jengo ambalo atakuwa anashea na wizara nyengine. *Concern* moja ya kamati hasa ilikuwa ni pale eneo ambapo Idara ya Nyaraka kwa upande wa Pemba ilipo hivi sasa katika eneo la Ngome.Nilitaka kuhakikishiwa tu kwamba je, katika hili jengo jipya ambalo ofisi itakuwa inatumia pia litaingiza ile Idara ya nyaraka au hii inaendelea kutafutiwa Afisi yake mbali kwa upande wa Pemba.

Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mheshimiwa katika nafasi iliyopatikana hivi sasa bado Idara ya Nyaraka au Taasisi ya Nyaraka iko kwenye lile lile jengo iliopo. Lakini kutokana na

juhudi hizo hizo ambazo tumezifanya kwa kutatua tatizo la Ofisi Kuu ilikuwa haina pahala, vile vile tunajua kwamba tuna tatizo kwa sababu taasisi ya nyaraka hivi sasa ipo kwenye jengo la Makumbusho.
Kwa hiyo katika mwaka huu wa fedha tutahakikisha kwamba tunajitahidi ili na Afisi ya Nyaraka nayo tuipatie pahala pake.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mheshimiwa tuendelee.

Kifungu 0301	Afisi Kuu Pemba	182,770,000
Kifungu 0401	Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	

Mhe. Salmin Awadh: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kujitahidi kujibu masuali mengi. Lakini kuna moja hili nilimuuliza sijui kwa haraka haraka sikuweza kupata jibu.

Wakati nikichangia nilizungumza juu ya maposho haya ambayo wizara yake ndio inamamlaka ya kuyapanga kwa mujibu wa sheria. Nikauliza juu ya vizee vyangu katika nyumba za wazee Sebleni ambapo wao huwa wanalipwa posho la Shs. 25,000/- kwa mwezi ni kama mshahara wao kwa sababu ndio wanaotegemea kwa ajili ya kujikimu. Mhe. Waziri hili kidogo limempitikia, nilitaka kujua ni jinsi gani wamezingatia hawa wazee wa nyumba za wazee Sebleni. Ili kuona wanaweza na wao kuishi vizuri kama tunavyoishi sisi. Nilitaka kidogo ufafanuzi ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi Afiri ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, bahati nzuri yeye Mhe. Salmini kwa sababu ni Mnadhimu alikuwa ananionesha wakati kwa hivyo katika kunionesha muda katika mambo ambayo niliyawacha kujibu ni pamoja na hilo.
Sambamba na kama nilivyolijibu la Wizara ya Afya, nilivyolijibu la Wizara ya Fedha nalo hilo serikali imelitolea maamuzi. Mheshimiwa namuomba asuburi siku ya Bajeti ya Wizara ya Wanawake na Ustawi wa Jamii amsikilize Mhe. Zainabu atakavyomwaga vimondo hapo.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Nitamsubiri Mhe. Bi Zainab.

Kifungu 0401	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	203,033,000
Kifungu 0402	Chuo cha Utawala wa Umma	470,000,000
Kifungu 0501	Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu	159,559,000
Kifungu 0601	Idara ya Mafunzo na Maendele ya Watumishi	58,887,000
Kifungu 0701	Idara ya Mipango na Rasilimali Watu	78,985,000
Kifungu 0801	Tume ya Utumishi Serikalini	141,265,000
Kifungu 0901	Idara ya Utawala na Rasilimali Watu	
		525,525,000
Jumla ya Fungu		**1,997,003,000**

(Vijifungu vilivyotajwa hapo juu vyote vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

FUNGU LA 44 – WIZARA YA NCHI OFISI YA RAIS UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Kifungu 040	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	1,544,315,000
Jumla ya Fungu		**1,544,351,000**

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vyote vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Uchumi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya Fedha ya Wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoja kwamba Baraza liyakubali makisio hayo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa kwanza niwashukuru kwa kazi nzuri na mashirikiano makubwa tuliyoyaonesha katika shughuli zetu za kila siku. Kabla ya kuakhirisha nimeombwa nitoe ukumbusho wa semina zetu.

Waheshimiwa wajumbe tunakumbushwa kwamba ile Semina ya *(PBZ)* Benki ya Watu wa Zanzibar. Kuhusu Islamic Banking itakuwepo kesho hapo Zanzibar Beach Resourt. Tunategemewa tuanze semina hiyo saa 3:00 asubuhi lakini usajili utaanza saa 2:30 asubuhi. Sote tunaalikwa. Ile Semina nyengine ya vitambulisho itakuwa *Zanzibar Ocean Veiw* muda kama huo saa 2:30 asubuhi usajili, saa 3:00 kuanza semina.

Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe. Baada ya hayo naakhirisha kikao hichi hadi tarehe 4 mwezi wa 7 mwaka 2011, saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 1:40 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 04/07/2011 saa 3:00 za asubuhi)